ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari

	Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

35.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.

69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 30Juni, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi (Kny. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, napenda kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Najma Khalfan Juma (Waziri Kivuli Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Upande wa Upinzani Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2010/2011.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 51

Kero ya *TRA* Kutoza Ushuru Mara Mbili

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu wananchi wa Zanzibar hususan wafanyabiashara wamekuwa wakitoa malalamiko yao juu ya mwenendo wa *TRA* wa kuwatoza kodi mara mbili wakati wanapoingiza bidhaa zao Tanzania Bara. Huku wakitoa kilio hicho wenzao wa Tanzania Bara hutozwa kodi mara moja tu, pale wanapoingiza bidhaa kama hizo hapa Zanzibar.

(a) Kwa kuwa jambo hili liliingizwa katika kapu la kero za Muungano

kwa muda mrefu, nini ufumbuzi wake hadi sasa?

(b) Iwapo tatizo hili limepata ufumbuzi. Je, Wazanzibari waliolipa kodi mara mbili kwa muda wote watarejeshewa fedha zao?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali hili napenda nitoe ufafanuzi kwa ufupi kwamba, jukumu kuu la Mamlaka ya Mapato Tanzania (*Tanzania Revenue Authority – TRA*) ni kukusanya kodi mbali mbali ikiwemo ushuru wa forodha kwenye bandari za Zanzibar na Tanzania Bara. Ni kweli kwa muda mrefu wananchi za Zanzibar hususan wafanyabiashara, wamekuwa wakitoa malalamiko yao juu ya mwenendo wa *TRA* wa kuwatoza kodi mara mbili wakati wanapoingiza bidhaa zao Tanzania Bara.

(a) Mhe. Spika, suala hili ni miongoni mwa mambo ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyawasilisha kwenye Kamati ya Kutatua Kero za Muungano kwa muda mrefu kama alivyosema Mhe. Mwakilishi chini ya Uenyekiti wa vikao vyetu hivi Mhe. Makamo wa Rais. Kupitia majadiliano katika kamati hio, tayari imeshakubaliwa kwamba bidhaa zinazoingizwa nchini na kukamilisha taratibu zote za kiforodha, kupitia kituo chochote rasmi cha forodha, zitahesabika kuwa zimeingia ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(b) Utekelezaji wa maamuzi haya ya serikali mbili, utamaliza kero hii ya muda mrefu. Haya ni matumainio yetu na tumeshakubaliana sasa tutarekebisha labda taratibu za kikanuni kwenye huu utendaji wa *TRA*. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri ningeomba nisisitize swali langu la (b) ambalo kwa kweli jibu lake lilikuwa silo. Sasa naomba nimuulize na kutaka kujua kwa sababu Wazanzibari walikuwa hawafanyiwi haki, walikuwa wakitoa kodi mara mbili. Je, wale ambao walikuwa hawafanyiwi haki na fedha zao walikuwa wakitoa kinyume na utaratibu zitarejeshwa. Kama zitarejeshwa ni lini.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa kweli

tutalifuatilia kwa kina suala hili kuona hasa kama kweli wamedhulumiwa. Unajua pesa ya serikali ikishaingia tena kutoka tabu, lakini tutaandaa utaratibu maalum labda kwengine kuweza kuwasaidia hawa ndugu zetu.

Lakini kama nilivyosema, hili itabidi tufanye uchunguzi wa kina kwa sababu sote tutakubaliana kidogo lazima tukubali baadhi ya mambo na wafanyabiashara wetu wana mizengwe yao. Kwa hivyo, mimi nakubali kwamba haya yametendeka na tutafanya uchunguzi wa kina na tutawasaidia.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri nina swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kweli *TRA* imebeza na inaviza shughuli za kibiashara kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Pia wanafikiria labda Zanzibar hatuna uwezo wa kuzalisha bidhaa iliyo bora na kuweza kupata soko Tanzania Bara.

Kwa mfano Mhe. Spika, Kiwanda cha kutengenezea madirisha na milango ya vioo, wafanyabiashara walikuwa wakipeleka Bara. Lakini sasa hivi wameshindwa kuuza huko wanaambiwa mambo haya hamkuweza kutengeneza bidhaa hii imetoka nje.

Je, Mhe. Waziri juu ya suala hili la bidhaa ambazo sisi tuna uwezo wa kuzitengeneza Zanzibar na kutaka kupata soko Bara, tatizo hili watalitatua vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, nakubaliana na *observation* za Mhe. Haji Mkema kwamba ni kweli wenzetu siku nyingi za nyuma huko walikuwa kidogo wakiwa-*fast rate* wafanyabiashara wetu. Wanafika hata kuwaambia hasa kwa nini msiagize moja kwa moja mkaleta huku mnapitia Zanzibar? Hiyo ni kweli kauli hizo zilikuwepo na kwa kweli mara nyingi nilikuwa nasema hii sio sera ya viongozi ni watendaji wakorofi tu. Kwa sababu hakuna msimamo wa serikali kuwa wafanye hivyo.

Sasa tumeshakutana wenyewe viongozi, tumeshaweka msimamo kwamba msimamo uwe ni huu. Ni muhimu sana kuelekeza uende tunakotaka sisi na sisi tutausimamia kwa juhudi zote. Hizi ni kero ambazo kweli tulikuwanazo siku nyingi Mhe. Spika, lakini sasa naona tumeshazitafutia dawa.

Mhe. Juma Duni Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi leo mapema. Namuuliza Mhe. Waziri kwamba, nadhani kuanzia kesho tarehe 1/7/2010 hizi ndio zimeanza kuwa na soko la pamoja. Na kwamba sasa kutakuwa na ruhusa kila jambo kupita katika nchi yoyote. Hivyo hatuoni kwamba tumekubaliwa kwa sababu sasa haliwezi kuzuilika kutokana na makubaliano ya Afrika Mashariki.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ingekuwa haya mazungumzo yameanza jana au juzi ningekubaliana naye. Lakini haya ni mazungumzo yamechukua muda mrefu, takriban Waheshimiwa humu nakumbuka mara nyingi sana mlikuwa mkituhimiza, mkitwambia na sisi tunasema tunalishughulikia.

Tuliunda kamati yetu ya watendaji kupitia Wizara ya Fedha yetu na Wizara ya Fedha ya kule, tukawapeleka watendaji wetu wakuu wakakaa chini mpaka tukaweza kufikia hapa tulipo. Kwa hivyo, kwa upande mmoja niseme hiyo Jumuiya inatuhusu sote Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda, Burundi, hilo ni la muda mrefu limefanyiwa kazi. Lakini hili letu ni la ndani.

Mhe. Spika, nataka kusisitiza hata kama kuna suala la jumuiya lakini kama Zanzibar mara nyingi kabisa tunalinda *iterest* zetu na tumekuwa tukiomba baadhi ya mambo mengi tu. Kwa mfano, hii leo tu bei za sukari au mchele tuna-*subsidize* na tunawaambia wenzetu jumuiya mchele Unguja ni siasa, tukifuata *rate* zenu tutaharibikiwa. Sasa tunawaambia na wanatukubalia na tunakwenda. Sio sisi tu, wenzetu hata Kenya wao wanafika kusamehe maelfu ya tani za sukari, ili na wao hivyo hivyo wapate manufaa na *stability* iwepo nchi mwao na kulinda biashara zao. Kwa hivyo, haya mambo yako *very flexible* yanazungumzika.

Nam. 52

Huduma ya Wateja *PBZ*

Mhe. Ashura Abeid Faraj (Kny. Mhe. Ali Denge Makame) – Aliuliza:-

Pamoja na kuingia kwa Benki nyingi hapa Zanzibar, wananchi walio wengi wa Zanzibar bado wanaitegemea *PBZ* kwa huduma za kifedha. Lakini utoaji wa huduma wa Benki hiyo una kasoro kadhaa, ikiwemo kuwepo misururu mirefu ya wateja wanaosubiri huduma, hasa siku za mwisho wa mwezi ambapo baadhi ya wafanyakazi huwa wanachukua fedha zao za mshahara.

Je Mhe. Waziri, *PBZ* ina mkakati gani wa kuboresha huduma zao ili wasikimbiwe na wateja wakati huu ambapo Sekta ya Benki Zanzibar inakabiliwa na ushindani mkubwa?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika, namshukuru sana mama yetu na kwa idhini yako naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, ni kweli kwamba pamoja na usumbufu na ushindani uliopo wa mabenki nchini mwetu, bado *PBZ* inaendelea kuwa chagua la Wazanzibari wengi. Benki hii imepiga hatua kubwa katika miaka ya hivi karibuni. Kutokana na hili basi, idadi ya wateja imeongezeka hivyo kusababisha foleni kuwa kubwa kwa baadhi ya wakati hasa wakati huu wa mishahara. Ili kuondoa usumbufu unaojitokeza sasa hivi, *PBZ* imejiwekea mikakati ifuatayo:

- Kuanzisha mtandao wa mashine za kutoa fedha (*ATM*) ambao umeunganishwa na mtandao wa *Umoja Switch*. Mtandao huo unaruhusu mteja wa *PBZ* kupata pesa zake katika mashine yoyote Tanzania. Mtandao wa *ATM* unatarajiwa kwa kiasi kikubwa sana kupunguza msongamano ndani ya matawi ya benki. Mtandao uko tayari na unatumika. Kwa kuanzia vituo viwili vimeshafunguliwa huko Uwanja wa Ndege na Darajani. Benki imo katika kuendeleza ufunguzi wa vituo zaidi;

- Kuanzisha huduma kwa wateja wakubwa (*premium banking*). Huduma hii itawawezesha wateja wote wakubwa kupata huduma maalum wakiwa katika mazingira yaendeyo na hadhi zao. Kwa sasa huduma hii itakuwa ni ya kipekee kwa Zanzibar na tayari matayarisho ya jengo yanaendelea. Itakapo anzishwa huduma hii itasaidia kupunguza idadi ya wateja wanaohitaji huduma hii;

- Kuanzia kituo cha huduma kwa wateja wa makampuni *(Corporate Center)*;

- Kuanzisha vituo vya huduma *(Service Centers)* katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba, kama nilivyoulizwa jana swali la nyongeza;

- Ukarabati wa Jengo la Benki Tawi la Chake Chake; na

- Huduma kupitia mtandao wa "*Internet*".

Mhe. Spika, hiyo ndio mikakati ambayo Benki yetu ya *PBZ* imejiandaa na imeanza ili iweze ku-*cock* na hii *volume* kubwa ya wateja. Lakini kwa kweli mimi nawashukuru sana Wazanzibari wote kwa kuipa au kuitukuza benki yetu na kuiamini na kuwekeza pale. Ahsante.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naoma kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa Benki

ya Watu wa Zanzibar imekuwa na wateja wengi, lakini zaidi inaonekana kwamba *PBZ* ina kituo kimoja tu kwa huduma zote za kibenki yaani kwa Zanzibar nzima. Lakini hapo nyuma *PBZ* iligundua kwamba utafika wakati iwe na wateja wengi. Na ikajaribu kujenga majengo katika wilaya mbali mbali ili kupunguza msongamano na mambo mengine. Hivyo naomba nielezwe nia ile imefikia wapi na yale majengo ambayo yako na yangesaidia sana kuondoa msongamano, yamenywa vipi kwa sababu hatuna taarifa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba *PBZ* Mhe. Spika, huko nyuma baada ya kufikiria kwamba wateja wanakuwa wengi zaidi ikajaribu kutanua wigo na kujenga majengo. Nakumbuka kwa upande wa Pemba Wete na hata Mkoani na Micheweni pia. Kwa Unguja Makunduchi, Mkwajuni na Chwaka. Hiyo hasa ilikuwa madhumuni ni kuweza kuweka matawi ili wateja wapate huduma.

Baada ya kujengwa majengo yale ajabu kabisa kwamba, ndio huduma kwa wateja kwa upande ule zikaporomoka kabisa, ikawa kwa kweli vituo vile havina kazi. Ujanua benki ni benki inaendesha kifaida, sasa ukiwa unaweka tawi hakuna wateja inabidi ulifunge, uzingatie mahapa ambako kuna faida, ndio ilisababisha kwa wakati ule vituo vile vifungwe na hata yale majengo yakawa yanaporomoka na kuwa magofu. Serikali au benki wakaona bora wayauze ili wazidishe mtaji kwengine. Hivyo ndivyo hali ilivyokuwa, lakini hali hiyo imepitwa na wakati.

Sasa *Alhamdulillah* watu wote wameamua kuweka pesa zao benki na huduma zote sasa zinapitia benki. Kwa hivyo, sasa imebidi lazima benki nayo niseme labda ijenge tena au sasa hivi inaanza kujenga tena. Labda tungeweza kuona wakati ule miaka 50 hali itakuwaje tusingefanya hivyo, lakini unajua mambo ya uchumi lazima uwe *flexible* kuweza kurekebisha hali inavyotokezea.

Mhe. Najma Khalfan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. kwa sababu shughuli za kibenki zimeongezeka hapa Zanzibar na Benki ya Watu wa Zanzibar imepanua wigo mkubwa kwa wateja wake na imediriki kufungua Benki ya Kiisilamu.

Swali langu la kwanza. Je, wananchi wa Zanzibar wanaitumiaje benki hii na vile vile huduma zake ni zipi. Je, wananchi wameshafahamu kwamba kuna Benki ya Kiisilamu na wanaitumia vipi.

Swali la pili, ni kwamba benki kweli zilikuwepo katika vijiji na sasa hivi zimeuzwa, lakini huduma za kibenki bado zinatakiwa na wanavijiji. Je, kuna utaratibu wowote wa kuanzisha ile benki ya gari kuwafuatia wanavijiji huko

waliko kwa kuwapa huduma.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kesho kuna swali zima Nam. 69 la Benki ya Kiisilamu. Lakini ili kunyokoa tu kidogo ningeweza kusema kwamba tumeshajitayarisha na tuko tayari, lakini nitalijibu kwa urefu kesho kwa sababu tusimnyime raha huyu aliyeuliza. Naomba Mhe. Najma Khalfani nilijibu vizuri kesho.

Pili kuhusu hizo *mobile* tumeshajitayarisha. Tulikuwa na matatizo ya magari tumeshayatayarisha na hayo magari yatapatikana kuweza kurahisisha huduma zetu. Lakini kama nilivyosema katika jibu langu mama kwamba, tumejaribu ku-*strengthen* kama nilivyosema Chake Chake, lakini pia watu wanaoweza kutumia *internet* waweze na pia hivi vituo vya *ATM* tunavyosambaza, ili yote kuondoa ule usumbufu wa msongamano.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. tunasikia kwamba hivi sasa benki yetu hii ya Zanzibar imetanua wigo na kufungua matawi Tanzania Bara. Je, hatua hiyo ishafikiwa na matawi mangapi washayafungua.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba benki yetu baada ya kuona kuna wananchi wetu wengi sana walioko Tanzania Bara na wafanyabiashara wanakwenda na kurudi, sasa kumekuwa na shida za usafirishaji wa pesa na hata uwekaji. Kwa hivyo, tukaamua kwa makusudi kufungua matawi. Tulifikiria twende kwenye miji mikubwa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, lakini kwa sasa tukasema acha tujikite kwa Dar es Salaam.

Mhe. Spika, nafikiri hatua zimekwishakamilika, tulikuwa na matatizo kidogo ya kupata jengo katika sehemu za biashara. Unajua sehemu zile Kariakoo, Lumumba, Mnazi Mmoja ndiko kwenye biashara. Sasa pale kulipata jengo sote tunafahamu lazima mfuko utononoke, umuondoshe mtu kwa mamilioni ndio upate jengo. Sasa tulikuwa na tabu kidogo ya kupata jengo lakini sasa hivi tumeshalipata nafikiri hatua ziko mwishoni kukamilisha ufunguzi.

Nam. 83

Wataalamu wa Fani ya Ujenzi wa Barabara

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi (Kny. Mhe. Mkongwe Nassor Juma) –

Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zake katika kuhakikisha kuwa mawasiliano ya barabara yanakuwa katika hali nzuri hapa nchini. Miongoni mwa jitihada hizo ni kukuza viwango vya wataalamu katika fani ya ujenzi wa barabara ili kujitosheleza kwa wataalamu wazalendo.

(a) Mhe. Waziri, katika kulifikia lengo hilo la kujitosheleza kwa wataalamu, wizara yako ina mpango gani thabiti wa kutoa mafunzo kwa wataalamu wake?

(b) Mafunzo hayo yanatolewa nje au ndani ya nchi?

(c) Kutokana na mahitaji ya sasa ya wataalamu wa ujenzi wa barabara, wizara yako ina ziada au upungufu wa wataalamu hao?

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi) – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 83 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza tunamshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa kutupongeza kutokana na juhudi zetu za kuweka mawasiliano ya barabara kuu kuwa katika hali nzuri.

Mhe. Spika, wizara imekuwa na mipango mizuri ya kusomesha na kukuza vipaji vya wafanyakazi wa sekta mbali mbali, mafunzo hayo yakiwa ni ya ndani na nje ya nchi, kwa kupitia Mfuko wa Serikali na Washirika wa Maendeleo.

Kwanza napenda ieleweke kwamba, kila siku zikienda mahitaji ya wataalamu yanazidi kuongezeka hasa kutokana na teknolojia mpya zinazovumbuliwa. Wizara yangu imeajiri vijana wapya waliomaliza *FTC* au Kidatu cha Sita na hivi sasa wanaendelea na Shahada ya Kwanza katika fani ya ujenzi wa barabara katika vyuo mbali mbali hapa nchini na nje ya nchi vile vile. Pia tuna utaratibu wa kuwapeleka wafanyakazi wetu nchi mbali mbali kukuza ujuzi wao chini ya mpango maalum unaogharimiwa na Benki ya Dunia.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamojana majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, mimi kwanza niwapongeze wenzetu wa UUB kwa kazi nzuri wanazofanya katika ujenzi wa barabara zetu mbali mbali. Kwa mfano, barabara ya kutoka

Mahonda – Mkokotoni, Mshelishelini – Pwanimchangani, Kwa Biziredi – Amani, Magomeni, Kwahani na Kwaalinato ambazo zinaendelea sasa hivi na nyenginezo. Hivyo pamoja na utaalamu huu waliokuwanao hawa wenzetu na kwa kuwa kazi zao zinaendelea vizuri. Wizara ina mpango gani wa makusudi kuhakikisha kwamba nyezo zinaongezeka ili barabara zetu zilizobakia ziende kwa haraka.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi): Mhe. Spika, kwanza kwa mara nyengine tena tunaendelea kupokea pongezi zetu za dhati. Lakini tunamshukuru sana Mhe. Ali Suleiman kwa ustahamilivu wake hasa kwa muda mrefu kupiga kelele kwamba barabara ya Kwahani ilikuwa haijajengwa. Lakini naamini mchakato unaoendelea sasa hivi katika barabara ile nadhani utazidi kumuongezea nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani kwa sababu kelele zake hapa Barazani zilisaidia sana kuweza kuhakikisha kwamba barabara ile inajengwa.

Kwa hivyo, pongezi hizo tunazipokea, lakini vile vile kwa pongezi alizozitoa kwa barabara ya Magomeni ambapo Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni kwa nguvu zote na yeye alikuwa inapofika bajeti ya Wizara ya Mawasiliana na Uchukuzi hatuna raha. Mpaka sasa hivi barabara hiyo ya Magomeni inaendelea kujengwa na karibu itamalizika na yale matatizo yameanza kupungua.

Vile vile pongezi za ziada tunategemea si muda mrefu na barabara inayotokea Darajabovu kuja Shaurimoyo, nadhani vile vile ikimalizika kujengwa basi shhukurani zitazidi na wananchi wa Jimbo la Kwamtipura watapata kufaidika vile vile.

Pili Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi ameuliza kwa kuwa jitihada ambayo tunaiona sasa hivi, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara tuna mpango gani serikali wa kuhakikisha kwamba tunawaongezea nyezo.

Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka nitoe pongezi zangu maalum kwa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa Unguja lakini pia na Pemba. Kwa upande wetu sisi serikali kupitia fedha za msamaha wa madeni, tumeweza kuhakikisha, hilo lilikuwa ni agizo la Mhe. Rais mwenyewe ambapo alisema kuwa tuhakikishe katika fedha hizi za msamaha wa madeni tunatafuta nyezo kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Amehakikisha kwamba anataka asione kiraka chochote katika barabara zetu na ndio maana sasa hivi baada ya kupatiwa pesa zile tumeongezea nyezo Wizara ya Mawasiliano kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, ndio maana barabara hizo zinajengwa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, bado kasi ya serikali iko pale pale, tukiweza kupata

fedha nyengine basi tutaongezea hizi nyezo ili kuhakikisha kwamba barabara zetu zote za
mijini na vijijini zinapitika bila ya usumbufu wowote.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri na ahsante sana vile vile kwa kumsaidia Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura asije akauliza swali.

Mhe. Moh'd Ali Salim: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, utaalam wa barabara na taalam nyengine kunakuwa na fani mbali mbali. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atueleze hao aliowapeleka masomoni ni wa utaalam gani na gani katika ujenzi wa barabara.

Lakini (b) tuliambiwa katika Baraza hili kuwa katika ujenzi wa barabara mradi wa barabara sita za kusini Pemba, miongoni mwa mambo yatakayofanywa na mradi ule ni kuombwa wataalam kutoka nje waletwe hapa kusaidia UUB katika ujenzi wa barabara zile. Ni wataalam wangapi walioletwa na wenye fani gani.

Swali © Mhe. Spika, hapa Zanzibar wakandarasi walipewa mafunzo ya ujenzi wa barabara kama vile utiaji viraka na mambo mengine. Je, wakandarasi wale waliopewa mafunzo yale, ni kazi ngapi wamepewa mpaka hivi sasa na ni kazi gani.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi): Mhe. Spika, Mhe. katika fani ya ujenzi wa barabara kuna utaalam wa aina nyingi. Mhe. Spika, kwa kuwa sikuchukua kumbukumbu hivi sasa kwa hiyo hawa waliopelekwa katika mafunzo tutakuja kuwaelezea kwa maandishi. Lakini pia kupitia katika bajeti ya Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi tutakuja kuweza kutoa ufafanuzi wa kutosha kabisa. Mhe. Spika, kwa hili namuomba Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi.

Mhe. Spika, jibu (b) Baraza hili ni chombo cha kutunga sheria lakini tunatakiwa kila tunachozungumza basi kiwe na usahihi. Mhe. Spika, kazi hii tayari tumeifanya lakini kama nilivyojibu swali la mwanzo kwamba tutakapokuja kusoma hotuba yetu ya bajeti ya Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi tutaweza kutoa ufafanuzi wa kutosha Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi.

Jibu © Mhe. Spika, ni kweli mafunzo haya yameshaanza kutolewa na kwa sababu sasa hivi tumo katika maandalizi ya uboreshaji wa barabara zetu, basi wakati wowote hawa ambao waliopatiwa mafunzo wataanza kupewa hizi kazi. Mhe. Spika, mfano mzuri ambao tutaanza kuuona ni katika barabara ya Magomeni pale, nadhani nyinyi wenyewe mkipita mnaiona kazi inafanyika

vizuri.

Mhe. Spika, nafikiri mwaka huu atakayekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni hatopata tabu sana kwa sababu lile kero la barabara ya Magomeni litakuwa limeondoka.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu jibu alilomalizia Mhe. Waziri ni kuwa atajibu hilo swali kwa maandishi ni dhahiri kwamba pengine atampa mjumbe mmoja tu. Sasa ni utaratibu upi utatumika ili Wajumbe wa Baraza zima waweze kufaidika na majibu hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi): Mhe. Spika, nadhani nilipokuwa nikijibu swali la nyongeza la Mhe. Moh'd Ali Salim (Mulla) nilielezea kwamba nitamjibu kwa maandishi lakini vile vile wakati tutakapokuja kusoma hotuba yetu ya bajeti ya Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi tutakuja kulitolea ufafanuzi wa kutosha. Kwa hiyo, Mhe. Mulla kwa kuwa yeye ndio aliyeuliza swali hili tutamjibu kwa maandishi lakini waheshimiwa wengine watafaidika katika ile jawabu ya jumla ambapo tutalitolea ufafanuzi wa kutosha.

Mhe. Spika, kama ingelikuwa bajeti ya Wizara ya Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi imeshasomwa basi ningelimuahidi Mhe. Mwakilishi tungeliisambaza jawabu ile kwa waheshimiwa wote. Lakini kwa kuwa bajeti bado mimi naamini kwamba swali litaweza kupatiwa ufafanuzi mzuri kabisa. Mhe. Spika, pia kwa yale yanayohitaji visaidizi tutaweza kusaidiana.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 – Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Lakini kama tunavyoelewa kwamba majumuisho ya hotuba hii tunategemea tuyafanye kuanzia saa tano. Sasa kwa muda uliopo nafikiri naweza kupata wajumbe kama watano hivi na wengine itabidi watusamehe. Kwa hiyo, naomba niwataje wafuatao kwamba ndio watakaopata nafasi na wengine basi wakishajijua tena watayarishe utaratibu wa kuweza kumuandikia labda kwa maandishi au kadri watakavyoona inafaa.

Watakaopata nafasi ni Mhe. Hasnuu Moh'd Haji, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Abass Juma Muhunzi, Mhe. Bihindi Hamad Khamis, pamoja na Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin. Tutakwenda mpaka baadae anaweza kubahatika mwengine.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo kuchangia kidogo tu sina mengi katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kufika hapa asubuhi ya leo.

Mhe. Spika, leo nitaanza kwa tofauti kidogo na nitaanza kwa kusema kwamba bajeti hii naikubali nusu na nusu siikubali. Kwa maana hiyo, siikubali mpaka waziri atakaponielezea nikafahamu mambo yafuatayo.

Mhe. Spika, mambo yenyewe ni matano. La kwanza katika ukurasa wa 31 nitausoma pamoja na ukurasa wa 32 hapa tunazungumzia mradi wa uimarishaji mikarafuu. Pia katika ukurasa wa 71 kuna kiambatisho namba 11 kinachozungumzia masuala ya karafuu.

Mhe. Spika, naomba waziri anambie na serikali itoe *statement*. Je, karafuu zinatakiwa au hazitakiwi? Je, karafuu sasa zimeshabinafsishwa au bado? Kwa sababu miaka mingi nyuma tulikuwa tukiambiwa hapa kwamba serikali inaanza mchakato wa kuzibinafsisha karafuu. Lakini leo Mhe. Spika, karafuu hazikuwekwa kwamba ni zao ambalo lenye thamani kwa taifa hili. Kwanza katika kitabu kizima humu hakuna mavuno ya karafuu yaliyoelezewa na hakuna jambo lolote lililosema kwamba ni kiasi gani karafuu imetoa kwa pato la taifa.

Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira na serikali kwa ujumla kwamba hawana haja nazo. Kwa sababu wangelituelezea humu kwamba vuno la karafuu angalau kwa miaka mitatu nyuma ilikuwa ni tani kadhaa na kiasi kilichopatikana ni hichi, tungeliweza tukaongeza nguvu zetu tukapata kiasi kadhaa. Mimi nafikiri hivyo ndio bajeti itakavyoandikwa lakini humu hamna.

Mhe. Spika, ingawa ilielezewa kidogo katika Wizara ya Fedha mwanzo katika bajeti lakini ile ni ya ujumla humu ndimo mnamohusika. Kwa hivyo, hilo ni moja ambalo ningelipenda nikalifahamu.

Lakini ukitazama katika ukurasa wa 71 wanasema wachangiaji wa masuala haya ya karafuu ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Shirika la Biashara ya Taifa *(ZSTC).* Haikuelezwa SMZ inatoa kiasi gani na *ZSTC* wanatoa kiasi gani.

Mhe. Spika, malengo ya mwaka 2009 walisema wanajaribu kuzalisha mikarafuu laki tatu, lakini kwa mwaka 2010/2011 kuzalisha vile vile miche laki tatu, wakati miche hasa iliyozalishwa ni 185,000. Mhe. Spika, naomba tujue kuna matatizo gani mpaka hii nakisi iliyopatikana haikuweza kupatikana na lengo hili la mwaka 2010/2011 litafikiwa namna gani.

Mhe. Spika, pia kuna gharama za mwaka 2010/2011, zimeandikwa tu gharama kwa mwaka 2010/2011 ni shilingi milioni 80. Gharama hizi ni za nini, ni za kuzalisha miche, ni za mafunzo, ni za kufanya utafiti. Maana yake anasema shilingi milioni 80 hizi kuna mambo kiasi sita ambayo yatafanywa na serikali au na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Sasa kweli kama tunataka kuongeza pato la karafuu shilingi milioni 80 ndio kweli zinatosha, ndio kweli tunalipa umuhimu zao hili la karafuu au tunakuja tukifanya masihara tu, au ndio kama hili nililosema kwamba sasa zao la karafuu halitakiwi.

Mhe. Spika, la muhimu ni kwamba wanafanya utafiti wa vifo vya mikarafuu midogo. Sasa utafiti huu mimi naomba uwe ni wa kweli kweli. Kwa sababu hapa mwanzo tulielezewa kwamba kuna dawa imevumbuliwa sasa ya wadudu wa embe. Sasa dawa ile ambayo wanasema wanajaribu kutafuta kwa masuala mengine, isije ikawa utafiti huu wa dawa za wadudu wa embe ni sawa sawa na ule utafiti uliofanywa nyuma huko kwa suala la mikarafuu *dieback* na *suddenback* ambao baadae ulituletea maafa mengi kwa mikarafuu.

Mhe. Spika, hili naomba nilipatie *statement* ya serikali kuhusu hasa zao hili tumeliweka katika misingi gani. Nikipata *statement* hiyo ile *tick* yangu moja ya kuikataa hii bajeti naweza nikaikubali, lakini vyenginevyo sitovumilia kwamba kila siku wakulima wa Donge na wakulima wa Pemba wa mikarafuu wanadanganywa kwamba mikarafuu itabinafsishwa na hakuna *statement* yoyote iliyotoka katika serikali.

Mhe. Spika, la pili liko katika ukurasa wa 68 Program ya Udhibiti wa Kichaa cha Mbwa. Mhe. Spika, hapa naomba nielimishwe tu katika malengo yamwaka 2010/2011 kuna kutoa elimu kwa wafugaji mbwa 360 na wasiofuga mbwa 360 katika wilaya zote za Unguja na Pemba. Sasa nilikuwa nauliza ipi iliyo muhimu zaidi, wale ambao wanafuga mbwa au wale wasiofuga mbwa. Mimi nafikiri kwanza tungeliwaelimisha hawa walio na mbwa na ambao wanataka kuelimishwa kuhusu maradhi haya, baadae tena likaja suala la kwamba ikiwa yeye hana mbwa anaweza akaelimishwa.

Mhe. Spika, ukurasa wa 6 ambao huu nitausoma pamoja na ukurasa wa 52 ambao unazungumzia takwimu za uzalishaji wa mazao. Mhe. Spika, kwanza naomba wizara i-*clarify* kwa sababu ukurasa wa 6 inaonesha kwamba hakuna upungufu wa vyakula ambao upo katika Zanzibar kwa mujibu wa statement hii.

Kwa sababu ukisoma kuanzia ukurasa wa 5 ni kwamba uzalishaji wote umepanda, kwa mfano viazi vitamu vimeongezeka kutoka tani 50,000 mpaka 53,000 na mambo mengine.

Lakini Mhe. Spika, ukitazama kiambatisho namba 1 hapa viazi vitamu vimepungua wakati kwenye *statement* wanasema vimezidi, ndizi zimepungua, mtama umepungua, njugunyasa zimepungua. Sasa mimi nilikuwa naomba nipate *clarification* ya jadweli hii ambayo imetolewa na ile *statement*. Lakini zaidi ni kusema kwamba ukitazama hii jadweli tuliyoletewa hapa Takwimu za Uzalishaji wa Mazao katika mazao manane yaliyopo hapa mazao matano yamepungua kutoka mwaka jana na mwaka huu.

Kwa mfano, mtama mwaka jana ilikuwa tani 610 wakati mara hii ni tani 453, ndizi ilikuwa tani 100,000 mara hii ni tani 90,000, viazi vitamu ilikuwa tani 55,000 mara hii ni 53,000 na kadhalika. Sasa hapa ni dhahiri kwamba hivi vitu vimepungua na *statement* waliyotoa huku katika maelezo yao ni kwamba vitu vyote vimezidi. Sasa kwanza tunataka tujue ipi ni kipi, imepungua au imezidi.

Lakini la pili ni kwamba ikiwa utachukua takwimu hizi ina maana kwamba Zanzibar uzalishaji umepungua sana. Kama umepungua sana je, kweli ndio tutafikia lengo la kwamba wananchi wote watakuwa ni *self sufficient* kwa chakula. Mimi nina wasi wasi kwa mujibu wa tarakimu hizi ambazo tumepewa. Mhe. Spika, nilikuwa naomba nipate maelezo kuhusu suala hilo. Halafu huu upimaji unakuwa namna gani, ukisiaji wa tani kama hizi, isije ikawa kama wale watu wa Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, watu wa Shirika la Umeme wakijua tu kwamba hii ni nyumba ya Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu kwa sababu wanamjua kwamba ni mwakilishi, kwa hivyo bila ya kwenda kutazama ile mita watajua ana kuka, ana friza na mambo mengine watatia tu makisio kwa mwezi ni shilingi laki moja wakati si kweli. Sasa sijui kama Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ndio wanageuka kama Shirika la Umeme sasa wana-*estimate* kwa njia hiyo, hawaendi wanakaa tu wanaona Gando kuna ndizi nyingi kwa hivyo watasema tani 20,000 kitu ambacho pengine safari hii ndizi hazikuzaliwa. Hebu tupeni ni utaratibu gani hasa ambao mnafanya ili kujua ni tani ngapi zilizopatikana kwa mwaka huu au kwa mwaka jana.

Lakini zaidi Mhe. Spika, katika jadweli hii nataka nijue madhumuni ya jumla ni kitu gani. Kwa sababu hapa wameandika kwa mfano ndizi mwaka 2005 ni tani 22,000, mwaka 2006 ni tani 88,000, mwaka 2007 hivyo hivyo mpaka mwaka 2009 kwa ujumla ni tani 305,000. Sasa jumla hii ina maana gani. Kwa sababu hizi ndizi kila siku zinaliwa, mwaka zililiwa, mwaka juzi zililiwa, sasa hii jumla inalenga kitu gani.

Mhe. Spika, ukiacha hilo nakuja katika ukurasa wa 35 kuhusu suala la uvuvi ambalo sina mashaka nalo sana. Lakini Mhe. Spika, nilikuwa naomba katika ile *dot* ya tatu na ya nne hizi zana za hawa watu ambao wanataka kupelekwa katika kina kirefu cha maji, basi wizara iharakishe ili watu hawa tuwaweke katika *position* nzuri ya kupata mazao haya. Mhe. Spika, najua kwamba idara inajitahidi na suala hili wanaweza wakalichukulia kwa uzito wake.

Mhe. Spika, la mwisho ni suala la vipando vidogo vidogo kwa mfano kama ilivyozungumzwa jana masuala ya embe, machungwa, tungule, shokishoki mbona hamna katika hii wizara. Haikuelezwa utaratibu gani ambao tutafanya na utaratibu gani tutakaowafanyia wakulima wetu ili kujiimarisha zaidi. Haiwezekani kwamba mpaka leo hata mtu akitaka tungule au nyanya tuagizie kutoka Tanzania Bara. Embe hizi ambazo zipo nyingi kwa nini hatuwahamasishi hawa wakulima na wao wakapata angalau motisha ya kuweza kuzalisha sana na tukaweza kuuza nje.

Sasa vitu kama hivi Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba tuelezewe wana mpango gani Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Kwa mfano, miwa inazalishwa sana siku hizi lakini haikuelezewa wazalishaji miwa watakuwa na motisha gani ya kufanya na nini watasaidiwa ili waweze kufanya mambo haya. Mhe. Spika, mimi nilikuwa nafikiria kwamba Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ingelijielekeza huko hasa kwa vipando kama hivi ambavyo vinaweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati mimi naomba nimalizie hapo lakini kama nilivyosema mwanzo ni kwamba bado mimi nabakia kama yule nahodha aliyemuuliza *chief officer* wake kwamba je, hii meli iko namna gani katika ujazo wa mizigo. *Chief officer* akasema *is half empty,* nahodha akamwambia si kweli *is half full*. Kwa hivyo, wote wakaanza kugombana yule anasema *is half empty, is half full*. Sasa Mhe. Spika, mimi nafikiri hii bajeti ni *half empty*.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Hasnuu Moh'd Haji: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuchangia machache katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Mhe. Spika, mimi moja kwa moja nakwenda ukurasa wa 19 Huduma za Utibabu wa Mimea. Mhe. Spika, kuna maradhi sasa hivi yameingia katika migomba na kwa hivi sasa zao linalowapatia wananchi wetu tija katika nchi yetu hususan kule Pemba ni migomba.

Lakini Mhe. Spika, matibabu ya mti huu wa mgomba kwa kweli sijayaona, ninachokiona kule wataalam wanapofika katika mashamba ya wakulima

matibabu makubwa wanayowaambia migomba ing'olewe ipandwe mingine. Mhe. Spika, inayopandwa ni ile ile kwa sababu mbegu zinazalishwa lakini mbegu ya mgomba sijapata kuiona kuzalishwa na wakulima wakapatiwa mbegu hiyo.

Mhe. Spika, pia utakuta jengine wanalowaambia kwamba wayakate majani yale yanayonyauka. Sasa kama utibabu wenyewe utakuwa ni huo sijui tutafikia wapi kwa wale wakulima ambao wamejikita katika kulima kilimo cha migomba kama hawakupewa dawa sahihi ya kuweza kuiponesha migomba watafikia wapi. Mhe. Spika, sijui wizara inafanya utafiti gani kwa sababu yale maradhi yanaonekana kila ikinyesha mvua kubwa basi ikipita mvua migomba inaharibika.

Lakini pia Mhe. Spika, kuna matatizo ya mbegu za mihogo. Mhe. Spika, katika kitabu hichi wizara imetwambia wamefanya utafiti wa mbegu za muhogo mpya lakini tayari mbegu hizo zipo. Mhe. Spika, nina imani kuenea kwa mbegu hizo mpya za muhogo katika nchi yetu mpaka zikienea na wakulima wakapata kulima sawa sawa kama wanavyolima ni muda mrefu. Mhe. Spika, sasa hivi wakulima wanataka kulima na wanaendelea kulima wanahangaika. Kwa nini ile mbegu ambayo wakulima wanalima na inazaa sana dawa yake tunaambiwa ikionekana ina matatizo ya ugonjwa ikatwe katwe na itolewe shamba ichomwe moto.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha atueleze haya matibabu ya mimea wanayofanya wanafanya vipi. Kwa sababu tunaona kuna dawa zinazopulizwa kwenye mahindi, mhindi ukianza tatizo basi Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kuna dawa unakwenda kununua unapuliza na wadudu wale waharibifu wa mhindi wanaondoka na unapata mazao.

Mhe. Spika, muhogo ndio chakula chetu kikubwa kwa Zanzibar lakini hukuti dawa inayoletwa kwa wakulima au mabwana shamba hawaji wakatuambia kwamba muhogo umeingia wadudu huu au una matatizo ya maradhi, tafadhalini tumieni dawa fulani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze hebu haya matibabu ya mbegu za mihogo au migomba yakoje, tupate kufahamu.

Vile vile kuna utafiti wa tani za vyakula, Mhe. Abubakar Khamis kasema. Pia Waziri atueleze utafiti huu unafanyika Unguja tu. Kule Pemba kuna mabonde mengi ya mpunga. Nilimuuliza Mhe. Mkuu wa Mkoa mmoja, akaniambia kuna bonde la kibokwa na mabonde mengine aliniambia hapa, wataalamu huenda pale wakaangalia mapolo ya mpunga yanayovunwa, wakishaangalia pale ndio wakapate hesabu zao.

Mhe. Spika, kule kwetu kuna mabonde mengi sana na hao wataalamu hawafiki kuja angalau kuangalia tu, sasa hizo tani kwa nchi hii zinapatikana hapa Unguja tu, kule Pemba hazipatikani au hakuna.

Jengine Mhe. Spika, suala la kilimo, inaonekana vilimo vilivyopewa kipaumbele katika nchi yetu ni watu wanaolima katika ardhi tambarare tu. Wale wakulima wanaolima kwenye ardhi za mawe na ukiangalia watu wanaolima kwenye ardhi za mawe wanaweza wakazalisha zaidi na zaidi kulikoni wakulima wanaolima katika ardhi za tambarare. Kwa sababu Mhe. Spika, kama waziri atakubaliana na mimi kwenye ardhi za mawe ukipanda hindi linakuja, ukipanda viazi mviringo vinakuja, ukipanda viazi vitamu vinakuja, kwa baadhi ya sehemu migomba nayo inakuja, ukipanda keroti zinakuja. Viungo vyote tunavyotumia hapa kama vitunguu thomu, vitunguu maji na vyengine vyote vinakuja. Lakini wizara na wataalamu wake waliopo inawasaidiaje wale wakulima walioko katika ardhi za mawe.

Mhe. Spika, katika jimbo langu ninaloishi mimi kuna sehemu inaitwa Pujini. Mhe. Waziri kama wizara yako inafahamu, naweza kuthubutu kusema kwamba katika ukanda wa Dumbi wenyewe wanaita, kuna maeneo yasiyopungua hata ekari 40,000 na kuzidi hayana mtu na wananchi wanakwenda kuyakata kata kidogo mtu analima kiasi robo au nusu heka basi utamkuta kavuna hindi la ajabu lakini hana utaalamu aliopewa.

Vile vile ukijaribu kupanda hivi viazi mviringo, sifikirii kama watapewa utaalamu unaostahiki hasa, wananchi wetu wataweza kupanda majahazi tena na kwenda Tanga wakihangaika na baadhi ya nyakati majahazi kuzama na wakafa. Wanastahiki wapewe utaalamu wa kutosha, ili na sisi tuweze kufaidika hapa.

Mhe. Spika, Pemba kwa sasa hivi tunategemea utalii uliopo Unguja huenda na Pemba ukafika na karibu ukawa sawa sawa, kwa sababu sehemu za utalii zipo na utalii tunategemea kwa kupatikana umeme wa uhakika basi wanaweza wakafika Pemba kwa wingi tu. Sasa wakulima waliopo kule kama watapewa taaluma nzuri ya kilimo, nafikiri kwa muda mfupi tu, basi wananchi waliopo katika kisiwa cha Pemba wanaweza kufaidika.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana katika wizara yake wataalamu wa kilimo waende. Mhe. Spika, tugeuze kauli au maneno ya kuzungumzia mpunga, migomba na muhogo. Tuangalie pale na tuzungumzie sasa viazi mviringo, vitunguu maji, vitunguu thomu na hizo keroti ili waweze kufanya na wawe na moyo wa kufanya hilo. Unapomfunza mtu kitu akifahamu, basi huwa na hamu sana ya kulitekeleza lile suala ambalo umemfunza.

Mhe. Spika, naomba nije kwenye ukurasa wa 25 kuhusu maendeleo ya mifugo.

Mhe. Spika, katika bajeti iliyopita nilizungumzia suala la ng'ombe pamoja na mbuzi walioletwa kusaidiwa wananchi katika vijiji. Moja kwa moja nilisema kwamba wale ng'ombe hawakupewa wananchi kwa kuwaondolea matatizo ya umaskini, bali walipewa wananchi kwa kuwaongezea umaskini. Sasa nataka nimuulize Mhe. Waziri atuambie ni mafanikio gani yaliyopatikana kwa kipindi chote walichopewa wananchi wale ng'ombe.

Vile vile Mhe. Waziri aje atuambie ni wananchi wangapi ambao wameshazalisha ng'ombe na tayari wamepewa wale ng'ombe. Mhe. Spika, katika kipindi kilichopita walinipa tabu sana wale, kwa sababu nazungumza hapa basi wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira siku ya pili haraka walikwenda nyumbani kwangu na kuwaangalia hao ng'ombe wenyewe. Sikuzungumza kuwa ng'ombe wale ninao mimi, isipokuwa nilizungumza kuwa ng'ombe wale wako kwa wananchi. Mimi ninaye ng'ombe kama yule lakini sikumpata katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Ng'ombe yule nilimnunua kwa pesa zangu na uzalishaji aliokuwa nao ni mzuri kupita kiasi. Kwa maana hiyo nilikuwa nawazungumzia watu ambao wapo pale kijijini kwangu na ng'ombe wale wanao.

Lakini Mhe. Spika, kwa taarifa tu, nafikiria sijafanya utafiti sawa sawa. Katika ile shehia yangu wale ng'ombe hawakupungua 14 au zaidi, lakini nataka nikupe taarifa Mhe. Waziri kuwa sasa hivi, sifikirii kama wale ng'ombe watano wanafika waliokuwa wako hai sasa hivi. Wale ng'ombe waliokuwa nao kwa kulinganisha na hali ilivyo, basi mimi ningeishauri wizara ijaribu kutumia mbinu za aina yoyote, ikiwa wana lengo la kuwasaidia wakulima basi wajaribu kuwabadilishia ng'ombe wale. Kinyume na hayo watakwenda na wao wataendelea kufa wala maslahi yoyote yatakuwa pale hayapatikani.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa suala la kumuuliza tena Mhe. Waziri. Mhe. Rais aliahidi kwamba wawakilishi wote waliomo ndani ya Baraza lako tukufu wapewe sehemu za kilimo. Lakini Mhe. Spika, tunamaliza miaka mitano sijamuona wala kusikia mwakilishi yeyote ambaye kapewa angalau eka 2 za kilimo.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri Je, kauli ile aliyoitoa Mhe. Rais kaishughulikia kwa kiasi gani na kama keshaishughulikia hawa wawakilishi watapata sehemu za kilimo, hizo sehemu za kulima kwa muda gani. Ikiwa sasa hivi imebakia miezi minne, ikimaliza miezi minne Baraza hili lako tukufu watakuwa watu hata dalili pengine hawaonekani tena. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nina mambo machache tu katika kuichangia wizara hii.

Mhe. Spika, kwanza ni maelezo ya jumla ingawa yatakuwa ni machache tu. Tulipokuwa tukijadili bajeti hii mwaka jana, sehemu kubwa ya maelezo ilikuwa ni namna ambavyo uchumi wa dunia umekuwa umetiribuka kutokana na soko la fedha. Hivyo ikaelezwa kwamba ili kurekebisha athari hizi zisije zikawa kubwa katika nchi zetu, kilimo kitapewa kipaumbele.

Mhe. Spika, nilitarajia katika bajeti hii basi kwa sababu kulikuwa kuna mipango na mikakati mbali mbali ambayo ilitayarishwa katika kukabiliana na hali hii ya uchumi wa dunia, nilitarajia basi bajeti hii ingeeleza angalau ni kwa kiasi gani Zanzibar imeweza kupunguza athari hizi za maharibiko ya uchumi wa dunia katika kukiimarisha kilimo.

Mhe. Spika, nilichokiona hapa ni kuongezeka kwa idadi ya matrekta mpaka imefikia asilimia 83 ya malengo ambayo walikuwa wamejiwekea. Lakini matrekta peke yake tu kama ilikuwa ni malengo basi ilikuwa ni vizuri na kuelezwa uchumi au kilimo kwa ujumla kimeongezeka kiasi gani kutokana na hayo matrekta yaliyoongezeka.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na maoni kwenye zile takwimu ambazo zilitajwa hapa na Mhe. Abubakar Khamis. Takwimu hizi ukiangalia maelezo ya ukurasa wa 6 kwenye kifungu cha 2.2.1 ambayo ina-*refer* moja moja kwenye kiambatanisho nambari 1, kuna tofauti za *figure* hizi za 2008. Kwa hivyo, hapa nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri kuwa ni haya maelezo kwenye ukurasa wa 6 au ni yale maelezo ya kwenye kiambatanisho cha ukurasa wa 52. Kwa sababu *figure* hizi za 2008 zote ziko tofauti na maelezo haya.

Mhe. Spika, zaidi kwenye kifungu cha 2.2.3 katika ukurasa huo huo wa 6, sijui kama hili nalo ni tatizo la kimahesabu au ni kusahau. Kwa mfano, nitanukuu Mhe. Spika, uvuvi wa samaki kwa mwaka 2009 umeripotiwa kuwa ni tani 25,399 ambazo zina thamani ya bilioni 47. Lakini mwaka 2008 tani 24, ni tofauti ya tani 1,000 tu thamani yake ni shilingi milioni 36. Sasa inawezekana hapa ni kosa la kimahesabu lakini imo katika bajeti, nadhani ilikuwa maelezo yatolewe ili tuone ni *figure* ipi iliyokuwa sahihi katika hizi.

Mhe. Spika, nikiendelea kuchangia, nadhani malengo yanaonekana kuwa mazuri katika wizara hii. Mchango wa asilimia 31 katika pato la taifa, limeongezeka kidogo ukilinganisha na asilimia 28 ambayo ilikuwa ikichangiwa hapo kabla. Kwa hivyo, naweza kusema hayo ni mafanikio makubwa na tunawajibu wa kuipongeza wizara kwa mafanikio haya.

Mhe. Spika, bado kuongezeka huku kwa mchango wa kilimo katika pato la taifa, hakujatuhakikishia wananchi kwamba sasa tunaweza angalau kupata mahitaji japo nusu tu ya mahitaji yetu ya chakula katika nchi.

Mhe. Spika, tulikuwa tukifikiria sana ingekuwa ni busara kwa wizara, kila inapokuwa inatueleza basi itueleze hasa mahitaji yetu ni kiasi gani na sisi wenyewe tunajitosheleza kwa kiasi gani, ili tuone ni namna gani Zanzibar inatumia sekta ya nje katika kusafirisha chakula. Hili ni jambo muhimu Mhe. Spika, kwa sababu athari hii ya miripuko ya masoko ya fedha na athari hii ya usafirishaji kutoka nje kuingiza chakula na matumizi mbali mbali, siku zote yana athari ya kuongezeka kwa bei katika soko letu.

Kwa hivyo, Mhe Spika, haya ni maelezo ambayo vile vile tulikuwa tukiyahitaji ili tuone ni kwa kiasi gani angalau sio tu tunajitosheleza, lakini tunaepukana na utegemezi wa kuagizia chakula ili kujinasua na kuongezeka kwa *inflation* kila mara hasa katika chakula.

Mhe. Spika, nilipoona *data* hizo kwenye ukurasa wa 5 imetajwa mwani na mwani hapa inaonekana kuwa uzalishaji, pamoja na kwamba kulikuwa na safari za kuwapeleka watu Indonesia. Ni mpango mzuri huu na tunaupongeza huu, lakini bado zao la mwani limeshuka uzalishaji wake.

Mhe. Spika, nadhani serikali ina wajibu mkubwa sana ilivyokuwa tumeona kuwa sasa zao la mwani ni muhimu katika biashara zetu na uchumi wetu, hasa kwa vile washiriki wengi wa zao hili ni akina mama, basi zao hili lingepewa nafasi kubwa sana kuendelezwa.

Mhe. Spika, nasikitika sana kwamba bado msimamo wa serikali katika zao la karafuu haupo. Hapo mwanzo tulikuwa tukizungumzia hatua pole pole ya ubinafsishaji na sasa hivi suala hili halizungumzwi tena wazi wazi. Kwa hivyo, sisi tulichokuwa tukikihitaji ni kauli ya serikali tu, isikae njia panda katika zao la karafuu, ikawa hadithi ni kubinafsisha pole pole lakini huku utekelezaji hauonekani hata hatua ambayo inapigwa. Kwa hivyo, ni vizuri ieleweke na kuwe na uwazi iwapo serikali haina *interest* na suala la ubinafsishaji katika karafuu basi tujuwe tunajitayarisha vipi. Mhe. Spika, hayo ni mapungufu ambayo tunayaona bado yanaendelea katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Mhe. Spika, tumefarajika sana kuona mpango huu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, katika kufanya mageuzi ya kilimo. Wamesema humu kuwa mageuzi haya yanafanywa kutokana na mabadiliko ya soko la ndani, kuongezeka kwa mahitaji ya chakula hasa kwenye soko la utalii, lakini vile vile *emphasis* inaonekana sasa hapa ni kuongeza ushiriki wa vijana, ambayo ndani ya Baraza humu ilikuwa ikizungumzwa hata maalim Suleiman jana alikuwa hapa kwamba kilimo bado kimeachiwa wazee.

Mhe. Spika, azma hii ni nzuri na inaleta faraja. Lakini ni kwa kiasi gani wizara imejitayarisha kuwatoa vijana katika biashara ya kuuza mitumba, ambayo sasa hivi inaongezeka na kuuza machungwa. Lakini kwa ujumla ni katika biashara ambako ndio wamezama sana na kuwapeleka katika kilimo. Nadhani hilo ndio suala ambalo serikali ilikuwa imejidhatiti na imejipanga vipi.

Mhe. Spika, sisi tunahisi kwamba iwapo kilimo kitatekelezwa katika misingi ya kisasa ya utumiaji wa nyenzo ambazo ni za kisasa, hili linaweza likawezekana. Lakini iwapo mageuzi bado yatategemea zana zile zile za kizamani na ikawa tija yake haionekani kuongezeka, basi bado vijana tutawakosa katika kilimo.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo linaonekana na ikiwa wizara itali-*focus*, ni kukichanganya kilimo na haya masuala ya ufugaji yakawa yako pamoja. Ufugaji wa kuku, ng'ombe na samaki kama ambavyo imetajwa humu.

Mhe. Spika, nina mfano wa bwawa la samaki ambalo humu limetajwa la Chambani, namna ambavyo limewakusanya vijana katika ufugaji wa samaki. Lakini vijana sasa hivi mipango yao ni kuona katika mkusanyiko ule wanaitumia vipi ardhi ili kuendeleza kilimo.

Mhe. Spika, hii ni faraja kwa sababu ardhi ile ambayo sasa hivi wanafikiria kuitumia ni ardhi ambayo ilikuwa inatumiwa zamani na wazee wetu. Lakini kwa kukosekana miundombinu kule ya kilimo pamoja na miundombinu ya kijamii, umeme na maji basi ilikuwa ni lazima kuwe na *shifting* ya watu kutoka maeneo yale ya kilimo na kufuatia umeme barabarani.

Kwa hivyo, kuwarejesha vijana katika maeneo ya kilimo, maana yake ni kuirejesha miundombinu. Tunahitaji sana Mhe. Spika, katika sehemu zile tuzingatie namna ambavyo tutapeleka maji, umeme na kutengeneza *access* za barabara, angalau iwe unaweza ukaenda na ukarudi japo kwa baskeli na kwa gari za ng'ombe.

Mhe. Spika, nadhani tukifanya hivyo tutaweza kuwakusanya vijana katika kushughulikia kilimo pamoja na ufugaji. Mimi nilipoangalia katika idara ya ushirika hapa kwenye kazi zao za usajili wa vyama vya ushirika, nikaona kwamba kwa mwaka uliopita, usajili ulikuwa vikundi kama 366, lakini vikundi 265 sawa na asilimia 72 ni vikundi vya kilimo na mifugo.

Mhe. Spika, hii ni ishara ya kwamba vijana na wananchi kwa ujumla bado wanakikumbatia kilimo, wangependa wakitekeleze kilimo katika njia ya ushirika kuliko kwenda mmoja mmoja. Sasa Mhe Spika, tukiiona ishara hii, kwa hivyo hapa kuna haja serikali kujidhatiti ku-*focus* namna ya kuisaidia idara ya ushirika kuviimarisha vikundi hivyo, sio tu kuvisajili, lakini kuvipa uwezo.

Kwa sababu tunapoona vikundi vinajengwa baada ya muda huona vikundi hivi navyo vimeyayuka, kutokana na kupoteza ama matumaini katika uzalishaji hasa kwa vile wanaona labda kipato hakipatikani, lakini vile vile ni vikundi ambavyo vinakusanyika bila ya kuwa na uwezo wa kuzalisha ingawa wana azma nzuri ya kuzalisha.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, idara hii ya ushirika itakuwa ni idara muhimu sana ya kuangaliwa na kuongezewa bajeti ili iweze kuviangalia na kuvisimamia vikundi hivi.

Mhe. Spika, imezungumzwa humu katika mambo ya uendelezaji wa misitu. Zamani tulikuwa tukipata *data* za uindaji, siku hizi sijui kama bado zimo. Mimi huwa najiuliza Mhe. Spika, wakati misitu inakatwa sana, pamoja na kwamba kuna upandaji, lakini bado uharibifu na ukataji wa misitu ni mkubwa sana kutokana na watu kujiingiza katika zile shughuli za uchongaji na kusafirisha biashara hizi za magogo, lakini bado inaweza kuambiwa kuna uindaji.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nafikiria kwamba badala ya kuiweka hii *concept* ya uindaji katika nchi yetu, mimi sikioni kinachowindwa zaidi ya wale paa wachanga wachanga ambao mmoja ni bora kuku mmoja kuliko wale paa. Mimi nilikuwa na mawazo tofauti, tuimarishe misitu yetu sambamba na kuwekeza, kuzuia na kuwahifadhi wanyama badala ya kuwawinda.

Mhe. Spika, hatuwezi kuwa hapa na mbuga za wanyama kama simba na nyumbu, lakini hawa hawa paa ambao ndio tumewaridhi na kuwaona katika misitu yetu, basi Mhe. Spika, wangepata hifadhi sasa hivi, tukazuia angalau kwa muda uindaji ili tukaona kwamba nchi yetu hivi sasa tunapata nafasi na vizazi vyetu vinakwenda katika hivyo vipori vyetu kuona wanyama katika nchi yetu, kuliko kuona kila siku kuna paa wameuliwa na kupelekwa marikiti wala hamna kitoweleo wala chochote.

Mhe. Spika, sambamba na hilo jambo moja bado tumelidharau kidogo, hili ni suala la ufugaji wa nyuki. Ufugaji wa nyuki Mhe. Spika, unatakiwa upewe kipaumbele na uimarishwe zaidi. Vijana wakikusanywa katika huu mkakati wa kuwashirikisha katika kilimo na ufugaji wa nyuki ikiwa ni moja ya maeneo hayo ya kuwashirikisha vijana, basi hili linaweza kuhamasisha na kuvutia vijana wakashiriki katika kilimo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe muda.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, namalizia kwa kutosahau kutoa shukrani sana kwa miradi hii ya *MACEMP*. Namshukuru sana Mkurugenzi wa uvuvi pamoja na waziri bila shaka amri zote zinatoka kwa waziri, katika

kusaidia bwawa la ufugaji wa samaki la Chambani kwa kuipatia boti, mashine pamoja na nyavu.

Mwisho Mhe. Spika, yametajwa humu maziwa kidogo tu na hii ndio lishe kwa ajili ya watoto wetu na sisi. Hakuna maendeleo ya maziwa humu, isipokuwa inasema serikali inatarajia kuendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazochukuliwa na wizara kuongeza maziwa. Tumefikia wapi na tunazalisha vipi maziwa, Mhe. Spika, ni jambo ambalo halikuzungumzwa.

Mhe. Spika, kibaya zaidi hapa kulikuwa kuna kiwanda ambacho kilikuwa kinatengeneza chakula cha mifugo na kiwanda hiki baadae kilitoka mikononi mwa serikali nadhani kilipewa ama itakuwa ni ushirika au mtu binafsi. Lakini taarifa tulizokuwanazo sasa hivi kiwanda kile kimegeuzwa kuwa ni ghala la saruji. Mhe. Spika, kiangaliwe kiwanda hiki kama hili linalokwenda lilikuwa ni kinyume na lengo letu basi alopewa kiwanda hiki kama hakiwezi basi kitafutiwe watu wengine ili lengo hili la kujiimarisha na kutoshelezeka kwa maziwa liende sambamba na kukiimarisha kiwanda kile.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafsi hii na baada ya kupata maelezo kidogo ya hizo *data*, basi naunga mkono kwa asilimia 75 bajeti hii na asilimia 25 naziwacha hadi hapo nitakapopata maelezo. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin: Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha asubuhi hii kuendelea na shughuli zetu za Baraza kwa kujadili Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Pia nichukuwe nafasi hii kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, kutokana na uchache wa muda wako nitazungumza kwa kifupi sana katika sehemu ambazo nimezikusudia kuzizungumza. Sehemu ya kwanza napenda kuzungumzia Idara ya Mazingira. Tumeelezwa kwamba katika ukurasa wa 37 kifungu cha 10.1.1.1 kwenye alama ya mwisho kwenye kidoto cha pili kutoka mwisho yaani wamefanya tathmini ya maeneo yenye kuingia maji ya chumvi kwa Unguja na Pemba, kazi hiyo inaendelea kwa Kisiwa cha Unguja.

Mhe. Spika, naomba kuumuliza Mhe. Waziri baada ya tathmini hii kufanyika na wakaona hicho ambacho watakiona. Je, kuna hatua gani ambazo zitachukuliwa na wizara yake, ili kuweza kuyasaidia maeneo hayo ambayo yanapata athari ya kuingiliwa na maji ya chumvi. Kutokana na maji ya chumvi yanapoingia kwenye mashamba, ambayo yanatumiwa na wananchi kwa ajili ya kilimo.

Kwa mfano, kwenye jimbo langu kuna maeneo mawili makubwa ambayo yanaathirika na suala hili, kama vile sehemu ya Usiambini ambayo iko Kengeja, hali kadhalika na kwa Mgogo. Kwa kweli wakulima katika maeneo haya wanaathirika sana.

Mhe. Spika, niliwahi kuwasiliana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira Pemba na wataalamu walikwenda na kuangalia hiyo hali, lakini mpaka hivi sasa hakuna chochote kinachoendelea na wakulima wa maeneo yale wanaendelea kuathirika. Kwa hivyo, baada ya tathmini iliyofanywa na wizara kuna hatua gani inayofuatia kwa ajili ya kuwasaidia wakulima hao.

Suala jengine kwenye Idara hii ya Mazingira. Hivi sasa Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri, tunazo hoteli nyingi sana za kitalii kwenye sehemu za fukwe na hoteli hizi zinachafua sana mazingira. Sasa sijui wizara na huku imefanya tathmini na kuona athari inayoletwa na uchafuzi wa mazingira katika maeneo hayo na hatua gani iliyochukuliwa.

Vile vile hivi sasa nchi yetu inakabiliwa na tatizo la ukataji ovyo wa miti, na hasa kwa kutumia misumeno ya moto. Kwa kweli hili ni tatizo na kama hatua za haraka hazikuchukuliwa, basi nchi yetu huenda ikawa jangwa baada ya muda si mrefu.
Kwa hivyo, ninamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kuliangalia suala hili, kwa ajili ya kuchukua hatua muafaka kwa lengo la kunusuru hali hiyo.

Mhe. Spika, kutokana na ukataji wa miti ovyo kunasababisha mabadiliko ya hali ya hewa ulimwenguni. Sasa Zanzibar kama ni sehemu ya ulimwengu nayo inaathirika kutokana na suala hilo. Hivi sasa tumo kwenye kipindi cha Kipupwe miezi hii ya Juni na Julai na baridi inakuwa kali sana. Lakini hali ilivyo hivi sasa ni tofauti kabisa, yaani wakati huu wa kipupwe watu wanatumia mafeni kwa ajili ya kupata baridi na hali hii inatokana na ukataji miti ovyo.

Kwa maana hiyo, ule uwezo wa *Ozone Layer* ulioko kwenye hewa umepungua sana kutokana na kupungua kwa *Carbon Dioxide* ambayo inatolewa na miti, yaani wakati wa kutengeneza chakula miti huwa inavuta *Oxygen* kutoka kwenye hewa na badala yake inatoka *Carbon Dioxide*, ambayo hii inasaidia sana kupunguza joto katika hewa.

Sasa kwa kuwa miti imekatwa kwa wingi inakuwa *Carbon Dioxide* inayozalishwa inakuwa ni ndogo mno, matokeo yake hali ya joto inaongezeka na baridi inapungua. Kwa hivyo, kuna haja ya wizara kuona kwamba inachukua hatua kuepusha ukataji ovyo wa miti, kwa ajili ya kunusuru

mazingira yetu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mkurugenzi wa idara kwa juhudi zake anazozichukua pamoja na kuimarisha uvuvi nchini mwetu. *(Makofi)*

Vile vile nimpongeze tena Mkurugenzi wa idara hii kwamba waliwahi kuja kutufanyia semina hapa na tulimuomba atupatie zile *CD* walizotuonesha kwenye semina ile. Kwa kweli ninamshukuru sana kuwa jana *CD* zile tumezipata. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 35 kifungu cha 9.1.1.2.1 kinazungumzia kuhusu kuwashajihisha vijana kwamba wafanye uvuvi katika Bahari Kuu. Kwa hivyo, kama vijana watashajihika kufanya uvuvi katika Bahari Kuu, sasa vijana hao wataweza vipi kwenda kuvua katika Bahari Kuu pamoja na maji mengi wakati hawana zana za kwenda huko.

Je, baada ya vijana kushajihika na kutaka kwenda kuvua kwenye hayo maji makubwa, wizara ina mpango gani wa kuwapatia zana vijana hao, kwa ajili ya kufanya hiyo kazi.

Mhe. Spika, suala jengine kwenye uvuvi kuhusu wale wavuvi ambao wako Ukanda wa Mashariki, hivi sasa wanasikitika na kulalamika sana kutokana na hali iliyojitokeza. Serikali ya Jamhuri ya Muungano imetoa vibali kwa meli nyingi za kigeni kuvua huko, sasa matokeo yake wavuvi hawa wa kienyeji wanapata matatizo, kwa sababu hawana vyombo vya kuingia kwenye Bahari Kuu. Lakini hizi meli zilizopewa vibali wanavua kwenye Bahari Kuu na mpaka wanakuja na huku juu. Kwa hiyo, wavuvi wetu wanakuwa wanapata matatizo sana. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, sasa sijui Mhe. Waziri atawasaidia vipi wavuvi waliopo Ukanda wa Mashariki. Kwa mfano, kwenye jimbo langu kuna kijiji kinaitwa Chole sehemu ya Kengeja wanalalamika sana kuhusiana na hilo. Kwa hivyo, sijui Mhe. Waziri atawasaidia vipi wavuvi hao wanaopata tatizo la kuingiliwa na meli za uvuvi za kigeni na wao kukosa sehemu za kuweza kuvua, kwa sababu vyombo wanavyotumia ni vidogo na hivyo inakuwa ni matatizo kwao.

Mhe. Spika, mtu anaweza kwenda baharini zaidi ya siku tatu anaporudi hana chochote alichopata kama alivyosema Mhe. Assaa Othman Hamad (Waziri Kivuli) wanavuna machofu badala ya samaki. Kwa hiyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, suala hili akaliona na kuweza kuchukua hatua muafaka kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi hao. *(Makofi)*

Suala jengine ni kuhusiana na kilimo cha umwagiliaji maji kwenye kitabu hili kimeelezwa katika ukurasa wa 24 kifungu cha 6.1.2.1. Hapa wameeleza kwamba kwa kushirikiana na miradi ya *TASAF* watafanya utafiti juu ya kilimo hiki cha kumwagilia maji kwa Unguja na Pemba. Lakini kwa hapa Unguja kuna mabonde ambayo tayari yameshaanza kushughulikiwa na kupatiwa miundombinu kwa ajili ya umwagiliaji.

Sasa kwenye maelezo ya kifungu hicho kuna bonde moja limetajwa ambalo liko kwenye jimbo langu nalo ni bonde la Machigini na wanasema wanatarajia kulima kama ekari 20 za umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, kwa upande wa Wilaya ya Mkoani kuna mabonde mengi, ambayo yalikuwa yakitumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji na mawili yako katika Jimbo la Chambani nayo ni Kimbuni na Mizingani. Kwa kweli hivi sasa mabonde haya yameachwa na yanaanza kuharibika. Halikadhalika kuna bonde jengine ambalo liko kwenye Jimbo la Mkoani, nalo hili sijasikia kutajwa kwenye kitabu hiki.

Hivyo, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuyaendeleza mabonde hayo ya Kimbuni, Mizingani pamoja na Giriama, kwa sababu kwenye mabonde haya wananchi walikuwa wakilima sana kwa utaratibu wa umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo linanisikitisa sana na wala sikuliona kutajwa kwenye kitabu hiki. Kweli tunataka kuingia kwenye kilimo cha umwagiliaji maji na maji tusidhani kama yanaongezeka ardhini wakati tukiyatumia, isipokuwa yanapungua. Lakini tunayo bahati ya kupata maji mengi kila mwaka na tunayaacha yakipotea bure.

Sasa ninachotaka kusema ni kwamba wizara ina utaratibu gani wa kuweza kuvuna maji ya mvua, kwa ajili ya kuyatumia kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kwa mfano, kama mwaka huu Pemba imenyesha mvua kubwa sana, kama kungekuwa na utaratibu wa kuweza kuvuna maji ya mvua, basi nadhani tungeweza kuyatumia katika mabonde haya ya kumwagilia maji. Lakini maji yale yote ya mvua yamekwenda zake habarini kwa sehemu zote mbili za visiwa vyetu, Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri awatumie wataalamu wake na waone kwamba wanaandaa utaratibu wa kuweza kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Mhe. Spika, nimalizie kwa lile alilozungumza Mhe. Hasnuu Moh'd Haji kutokana na Kauli ya Rais. Sasa kama ni Kauli ya Rais haijaheshimiwa naomba

nimuulize Mhe. Waziri. Je, kauli ya nani mwengine itaweza kuheshimiwa kama ile ya rais imeshindwa kuheshimiwa na kutekelezwa kwa lile aliloagizwa?

Mhe. Spika, jengine kwa kumalizia nasikitika sana kumwambia swahibu yangu kwamba, wizara ambazo zinazo Manaibu Mawaziri, mawaziri wao wakati wa kuwasilisha bajeti zao huwa wanawashukuru sana manaibu mawaziri wao kwa ajili ya kushirikiana nao katika kutekeleza kazi zao. Lakini nasikitika sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira amesahau kumpongeza na kumtaja Mhe. Naibu Waziri wake Ahsante sana Mhe. Spika. . *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ambayo sikuilalia wala kuiamkia, yaani ni nafasi ya upendeleo ninashukuru.

Mhe. Spika, mchango wangu ni mdogo tu nianze na wataalamu. Kwa kweli tunawaomba wataalamu wetu waache tabia ya kujifungia kwenye maafisi. Kutokana na hali hiyo, nawaomba wataalamu wetu wawe kama waandishi wa habari, kwa sababu waandishi wa habari hufuatia habari, basi na wao ninawaomba wajaribu kuwafuata wakulima na ule utaalamu wao utakua unaongezeka siku hadi siku na kuweza kufanyakazi vile inavyotakiwa. *(Makofi)*

Katika kipindi cha miezi iliyopita nyuma wakulima wengi walikuwa wakibeba mataka na kwenda kutupa kwenye mashamba yao nikiwemo na mimi. Mhe. Spika, katika mashamba yale kwa mfano, leo unamwaga mataka na baada ya kumwaga mataka unatarajia upande, sasa ikiwa muhogo au kiazi, lakini unayafanya yale bila ya utaalamu wowote.
Kwa kweli nimemwaga mbole ya mataka ndani ya shamba ile, basi muhogo au kiazi nitakachokipanda lile shina moja kama mtoto anaweza kupanda juu na kukaa, jinsi ya muhogo ule ulivyokua vizuri, michungwa pamoja na miti mikubwa kama vile miembe. Kwa mfano, kwenye shamba langu ambalo nimemwaga mataka, basi michungwa pamoja na miembe yote ilikuwa imekufa, baada ya kumwaga mataka hayo imechipua vizuri sana.

Mhe. Spika, matatizo yaliyojitokeza muhogo, kiazi nimevipanda bila ya utaalamu, kwa sababu baada ya kumwaga mataka sikupata elimu yoyote kwa ajili ya kufahamu baada ya kumwaga taka je mazao yatakuwa vipi. Kwa mfano, nimemwaga leo na kesho nikapanda.

Kwa hivyo, nadhani wataalamu baada ya kupata taarifa kwamba safari hii watu wengi wamemwaga mataka, basi wangewafuata wakulima au wakulima

wakashirikiana na wataalamu wangejua tufanye nini. Sasa tatizo lililotokea Mhe. Spika, muhogo au kiazi unaweza kung'oa na shina moja mkagawana na mwenzako kama vile Mhe. Juma Duni Haji na kuweza kula kwa muda wa siku tatu nyumbani. *(Makofi)*

Hata hivyo, wasi wasi wangu kuhusu chakula kile ambacho kimelimwa wakati ule, yaani muhogo au kiazi kile unapokuja kupika huoni ladha yoyote. Kwa maana hiyo, naiomba Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kupitia kwako Mhe. Spika, ishirikiane na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu vyakula vile ambavyo ni vingi katika mashamba mengi waliyomwaga mataka kufanyiwa utafiti. Je, havina madhara kwa afya ya mwanadamu.

Kutokana na hali hiyo, mimi binafsi ninawaomba wataalamu tukashirikiana nikawapeleka mpaka kwenye shamba langu, muhogo upo na tayari nimeshawahi kuung'oa na kwenda nao nyumbani, wakati unapokula huoni ile ladha ya kile chakula na wala hujui kama kweli huu ni muhogo, lakini unene wake shina moja unajaza kipolo. Kwa maana hiyo, wasi wasi wangu upo katika afya ya mwanadamu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hili linatokana na kwamba wataalamu hatuwaoni katika mashamba na kushirikiana na wakulima kwa ajili ya kupata utaalamu. Kwa hiyo, mashamba mengi yamemwagwa mataka na kila mmoja shamba yake inavutia, yaani ukiwa mbali unauona mgomba unavutia kwa vile ulivyokoza rangi nyeusi, lakini hali ya vyakula vile kwa afya ya mwanadamu sijui vipi.

Siku moja katika ziara za kamati Tanzania Bara, niliwahi kuuliza kwenye Kitengo cha Utafiti, kwa sababu suala hili lilikuwa likinikereketa sana, basi niliuliza je hizi taka tunazozichukua na kumwaga kwenye mashamba, baada ya kumwaga nikapata vyakula. Je, chakula kile kitatuletea madhara gani.

Kwa kweli suala hili linahitaji kufanyiwa utafiti, kwa sababu taka zile zina sumu, inawezekana taka zile unaweza kuzimwaga na zikaa muda ndio uje upande vyakula kama hivyo, lakini hatujui. Sasa leo ameanza mtu mmoja baada ya kuona mafanikio mazuri, wananchi tukaingia mbio lete magari ya taka tukamwaga.

Mhe. Spika, kutokana na hali hii naziomba Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kushirikiana kwa pamoja, kwa ajili ya kufanya uchunguzi kuhusiana na vyakula hivi ambavyo wananchi wamevilima kwa nguvu na wanavyo kwenye mashamba yao, basi vifanyiwe utafiti ili kuweza kufahamu faida na harasa kwa afya ya mwanadamu. *(Makofi)*

Suala jengine nizungumzie kuhusu misitu. Mhe. Spika, misitu yetu kweli inateketea na kukatwa kwa nguvu na kama hazikuchuliwa hatua madhubuti pamoja na kupigwa marufuku basi itakuwa hatari.

Nadhani nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kutuelimisha, kwa sababu bila ya shaka kuna siku maalum ya kukithiri kwa ukatwaji wa misitu. Kwa hivyo, ninafikiri ni vyema akatujuilisha siku gani ambazo msitu unakatwa kwa wingi. Pamoja na hayo, ninaomba wataalamu kama wanafanyakazi na *research* za kutosha basi watuelimishe.

Suala jengine nije kwa hawa wafanyakazi wa misitu. Mhe. Spika, wafanyakazi hawa wanafanyakazi katika mazingira magumu ambayo ni mazito sana.

Kwa mfano, mfanyakazi mmoja anapewa shehia tano, wakati mwengine mfanyakazi anaweza kuwa anaishi Ndijani anatakiwa atoe huduma mpaka Uzi. Vile vile mfanyakazi huyo hana hata baskeli pia azunguke kwenye shehia zote. Kwa hivyo, naiomba wizara kupitia kwako Mhe. Spika iwashughulikie wafanyakazi kwa kupatia vitendeakazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wafanyakazi hawa siku za mvua nadhani lile suala la siku gani misitu inakatwa kwa wingi linaweza kuingia hapa. Kwa mfano, siku za mvua mfanyakazi anataka kwenda kazini, basi hana hata lile *raincoat* kwa ajili ya kujikinga na mvua, hapa inaonesha wananchi wanaingia na kuharibu misitu. Kwa hiyo, naomba wapatiwe vitendeakazi angalau vya kuweza kuwasaidia.

Hata hivyo, kuna suala namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, lifanyiwe utafiti inaonesha hata hawa wafanyakazi hakuna mashirikiano na hizi Kamati za Vijiji. Kwa maana hiyo, suala hili lifanyiwe utafiti na kuweza kutatuliwa, kwa ajili ya kuwa na mashirikiano ya pamoja na Kamati za Vijiji nadhani inaweza kuwasaidi katika utendaji wa kazi.

Mhe. Spika, jengine kuna tatizo ambalo linawapata wafanyakazi. Kwa mfano, mfanyakazi anaweza kutoka na kwenda mwituni na kuona magogo yamekatwa, itabidi atoe ripoti katika taasisi husika, wakati anapotoa ripoti na magogo yapo pale.

Sasa magogo yale ataambiwa ayachukue wakati hata baskeli hana atayachukua vipi, kwa sababu anapotoa taarifa anaambiwa gari hakuna au mafuta haina na hili ni tatizo. Kwa kweli haya ndio matatizo ambayo wanayapata wafanyakazi wetu.

Vile vile kuna suala jengine ambalo sikutaka kulisema ambalo tayari limeshazungumza na Mhe. Hasnuu Moh'd Haji kuhusu Mradi wa Ufugaji. Kwa

kweli mradi huu tumewazidishia umasikini wananchi wetu, kwa sababu jana nilikuwa nikizungumza na kijana mmoja katika Shehia ya Tunguu.

Kijana huyo amesema alipewa ng'ombe, baada ya kupewa ng'ombe ambaye hali yake ilikuwa si nzuri, yaani hata siku tano hafiki dhofu, kwa bahati nzuri ng'ombe yule alikaa naye na kumshughulikia. Sasa baada ya ng'ombe kumhudumia yule kijana ikabidi yule kijana anatoa chake mfukoni kwa ajili ya kumhudumia yule ng'ombe na huko si kuzidishwa umasikini.

Mhe. Spika, baada ya muda ng'ombe yule akapata ujauzito, kijana yule alikwenda kuwaita wataalamu kwa sababu alikuwa akiumwa, aliambiwa ng'ombe tayari ameshakuwa mjamzito. Sasa ng'ombe yule alipigwa sindano baada ya kupigwa sindano mimba ile ikaharibika na matokeo yake akapata ugonjwa, alipokwenda kuwaita tena hawakupita hao wataalamu. Kwa hivyo, alitoa fedha zake kumtibu ng'ombe yule mpaka Mwenyezi Mungu akamjaalia akarudi hali.

Kutokana na hali hiyo, badala ya kupunguza umasikini akawa anazidisha umasikini kwa ajili ya kutoa chake cha akiba na kumtibu ng'ombe, *Alhamdulillah* Mwenyezi Mungu akamjaalia akapata ujauzito mwengine. Kwa hivyo, alisema nimuone mtaalamu apite hapa, kwa sababu nilihudumia mwenyewe ng'ombe huyu kwa hiyo mpaka leo hayapita mtu yeyote. Mhe. Spika, naomba hali hii ishughulikiwe na tupatiwe tathmini nzuri kwamba je mafanikio ya mradi huo yako vipi.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie kuhusu mazao ya biashara. Hapa ninalo swali naomba kuuliza, hivi wizara imechukua hatua gani kuwashajihisha wakulima wa mazao ya biashara na mafanikio yaliyopatikana yamefikia kiasi gani?

Vile vile mazao ya biashara yamekabiliwa na wadudu wa haribifu. Je, wizara ina mpango gani wa kuchukua hatua madhubuti ya kupambana na wadudu hawa?

Mhe. Spika, nakushukuru.
Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa kuna dakika 5 kufikia saa 5:00 kamili, lakini nitachukua dakika tano nyengine nimpe Mhe. Zahra Ali Hamad atumie dakika 10.

Mhe. Zahra Ali Hamad: Nakushukuru angalau kunitoa kwenye *recycle bin*, kwa sababu unajua huko majimboni kuna mchakato sasa wasiponisikia itakuwa ni mtihani kidogo. *(Kicheko)*

Mhe. Spika, mengi ya mafanikio ya Mhe. Waziri ambayo ametueleza ni

kupanda kwa bajeti kutoka mwaka 2005 kwa asilimia 4 mpaka kufikia asilima 7 kwa mwaka 2009. Ongezeko hili Mhe. Spika, linaifanya Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazotekeleza Azimio lile la Abuja la mwaka 2003. Azimio ambalo liliagiza Sekta ya Kilimo kupewa kipaumbele, kwa ajili ya kuwa na uhakika na chakula na kujikomboa kiuchumi.

Vile vile Mhe. Waziri ametueleza kwenye hotuba yake ya bajeti kwamba kwa mwaka huu Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 31 ya pato la taifa.

Mhe. Spika, mfumko wa bei za chakula unatokana na uagiziaji hususan wa chakula ambacho tunaagiza kutoka nje. Kwa kweli ukuaji wa uzalishaji wa mazao ya chakula ndio unaoweza kupunguza kasi ya ongezeko la bei ya chakula.

Chakula chetu kikubwa Zanzibar ni mchele na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha, nilimsikia asubuhi akisema kwamba sio kama ni chakula tu, lakini tunasema ndio siasa za nchi. Kwa mfano, ikiwa ndani ya nchi hapa kwetu Zanzibar hakuna mchele, basi siasa lazima zitakuwa na matatizo, wananchi watapiga kelele njaa.

Sasa nadhani imefika wakati wizara kwa kuliona hili la umuhimu wa kilimo cha mpunga. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri wizara hii inayo miradi mingi pamoja na wataalamu wake ni wengi. Kwa hivyo, nimpongeze Mhe. Waziri kwa sababu bado mpaka leo anasomesha kwani nimeona kwenye kitabu chake hiki, basi tuwatumie wataalamu wetu hawa.

Mhe. Spika, nafikiri wataalamu ambao tunao wanaandaa miradi kwa ajili ya manufaa binafsi, hawajali miradi hii kama itakuwa endelevu au itawasaidia vipi wananchi. Kwa kweli tukiangalia miradi iliomo humu ni mingi sana, lakini tujiulize ni kiasi gani ambavyo imetuondosha katika umasikini, pia kiasi gani tumeweza kwenda sambamba na lile Azimio la Abuja la kujitosheleza kwa chakula, inaonekana hali bado ni ngumu.

Sasa Mhe. Waziri awatumie wataalamu hawa wengi ambao anao, kwa ajili ya kuhakikisha hii sehemu ndogo ambayo tunayo ya kilimo inatutosheleza, ili tupungukane na huu wingi wa kuagizia chakula.

Mhe. Spika, waziri alitueleza hapa kwamba ana matrekta tayari arubaini na tano na akatueleza ni asilimia thamanini na tatu ya mahitaji yetu ambayo tunahitaji Zanzibar, asilimia thamanini na tatu ukitizama sio ndogo lakini utaona wananchi wetu wengi wanasikitika matrekta hayawafikii, lakini hata yakishawafikia hayo matrekta basi kuna mambo muhimu ambayo yanahitajika.

Mhe. Spika, pembejeo zinahitajika hata hapo wakishakulimiwa kwa sababu ardhi yetu ndio hiyo hiyo basi ipate kidogo virutubisho ambavyo itaifanya ardhi ile irutubike, lakini zaidi ya hayo wataalam wenyewe wateremke tatizo la wataalam wetu hawateremki.

Siku za nyuma tulikuwanae bwana Hasania kijana huyu alikuwa akisaidia sana na kila alipokuwa akipelekwa basi alikuwa na shamba yake ya mifano, tunaambiwa kwamba kuna mashamba darasa lakini bado haya mashamba ni machache na hayajasaidia sana, hebu tungejitahidi hawa wataalam wetu wa kilimo kila mtaalam yeye mwenyewe binafsi akawa na haya mashamba darasa ili wananchi wetu wakajifunza kutokana na utaalam ambao yeye mwenyewe anao.

Mhe. Spika, miongo pia inasaidia sana kuhuwisha kilimo chetu lakini bado haijaonekana wizara kama imekazia suala la kuwaambia wananchi juu ya miongo ya kulima wakajua kama wakati huu ni wa kulima, wakati huu wa kupalilia, huu ni wa kufilia. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana kwenye kilimo haya matrekta ambayo tumepata basi yafanye kazi.

Mhe. Spika, juzi nilimuona Pro. Sarungi nae kapeleka matrekta mengi jimboni kwake na akaahidi kwamba matrekta haya ambayo nimeyakabidhi leo kwa wananchi basi tuna hakika tutalisha Tanzania nzima, kwa hivyo na sisi tuna hamu kusikia haya matrekta ambayo tunayo yanalisha tunatamani kama vile wenzetu wanavyosema huu ni mchele wa Mbeya, huu wa Kilosa na sisi siku moja tuseme huu ni mchele wa Zanzibar unatoka katika mabonde yetu ya Cheju, Upenja, Chambani, Weni, Biriama na sisi tuweze hata kusafirisha kama tunavyochukua Mbeya tukaleta hapa na uwezo huo Mhe. Spika, tukiamua tunao. Lakini jambo lolote ni kupanga na kuchagua iwapo kama tutaamua kama kweli tunataka kilimo kitosheleze mahitaji yetu ya chakula basi kitatosheleza.

Mhe. Spika, palizungumzwa kuhusu mikakati ya Wizara moja ni kuweka karantini ni wepesi wa kuzungumza mambo lakini ufuatiliaji wetu unakuwa mdogo, kuna karantini ya mifuko hapa karibu miaka mitatu hivi mpaka leo mifuko bado ipo na hii karantini matatizo ambayo tunayo ya maradhi ya matunda, kwa mfano embe ikiingia mdugu kama ambavyo tumeelezwa na ambavyo tunaona ni mtihani na njaa kwa sababu kipato cha mwananchi wetu tunakijua kilivyo. Lakini kama Pemba kukiingia embe kule huwa ni cha mchana, chausiku na kijio humo humo na wenyewe wamesema hawa na embe wameipa jina hasa kwamba ni Tume kwamba ndio muamuzi wa mwisho, ikifika saa kumi hujakijua basi embe zinafanya kazi inakuwa ndio muamuzi wa mwisho siku hiyo.

Sasa leo likiwa lina funza haliliki ni mtihani na njaa sasa Mhe. Waziri aone

umuhimu huu wa kuweka karantini, ahsante sana Mhe. Spika, naona ili mazao ya matunda yasiingie kutoka nchi jirani tumeelezwa haya matatizo ya mafunzo yanatoka katika kisiwa cha Hawaii nimesoma katika jarida lao ambalo wametupa, lakini kutokana na kwamba milango tuliiwacha wazi, laiti tungelifunga tukahakikisha kwamba matunda hayaingii yasingetukuta haya sasa iwapo tutaendelea kuiwacha wazi matatizo yatazidi kuongezeka Mhe. Spika.

Namuomba Mhe. Waziri, hii karantini iwe ya kweli na ihakikishe kwamba inadhibiti kuingia matunda ndani ya nchi yetu, nilikuwa na mengi lakini Mhe. Spika, ananionyesha kwamba muda wangu umekwisha haya ambayo nimechangia na yale ambayo Mhe. Waziri nimempelekea kwa sababu nilijua sitokuwa na muda wa kutosha, naomba majibu na naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, waheshimiwa wajumbe ilipangwa kwamba ikifika saa 5.00 tuanze kuwaachia Naibu Waziri pamoja na Waziri kufanya majumuisho sasa kuna wajumbe wangu ambao hawakupata nafasi ningewaomba radhi muda umetukwaza kidogo, waheshimiwa hao ni Mhe. Ali Denge Makame, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Hijja Hassan Hija, Mhe. Ali Suleiman Ali, Mhe. Juma Duni Haji, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Bihindi yeye mwenyewe hayupo na Mhe. Ali Moh'd Bakari nilimwita jana ikawa hayupo yeye nafasi kaipoteza mwenyewe.

Sasa baada ya kuomba radhi naomba nimkaribishe Naibu Wazairi wa Kilimo, Mifugo na Mazingira.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo kusimama vizuri kulinganisha na hali yangu ya jana, kwa niaba yangu na kwa niaba ya familia yangu yote sina budi kwanza kumshukuru Mhe. Rais Amani Abeid Karume kwa uamuzi wake wa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa kipindi hiki chote.

Pili sina budi kumpongeza Mhe. Waziri Kiongozi, Mhe. Naibu Waziri Kiongozi kwa msaada wao wote walionipatia katika kipindi hiki cha miaka mitano ndani ya Baraza, lakini pia nawapongeza wajumbe wote ambao walinipiga masuala magumu na masuala mepesi ni sehemu ambayo wamenifunza, namuomba Mwenyezi Mungu akitujaali kurejea awajaalie na wengine wawepo katika sehemu hii waje waone uzito na ubora wake.

Mhe. Spika, nakupongeza wewe binafsi kwa kunivumilia katika kipindi kikubwa ambacho nimekuwa na pata matatizo kidogo kidogo lakini ndio

mitihani ya Mwenyezi Mungu, lakini pia na mshukuru Mwenyezi Mungu kwamba sina lile tatizo dume nakusudia UKIMWI nina maradhi mengine tu, kwa hivyo naomba Mwenyezi Mungu anisaidie nipate nafuu na sote tunaoumwa ndani ya Baraza hili Mwenyezi Mungu atujaalie tupate nafuu pamoja na waislam wote.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa umakini wako na busara zako katika kuliendesha baraza lako hili. Aidha nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira mzee wangu Mhe. Burhan Saadat Haji kwa kunivumilia kipindi kirefu sana, lakini pia nataka niseme neno moja kuna mzee wangu mmoja aliwahi kunambia baba yangu wewe vumilia, katika dunia hata Mwenyezi Mungu akikupa kitu basi kuna wengine watakuwa hawapendi hiyo ndio dunia. Katika dunia hata Mtume wetu amepata mitihani na pia kuamua kuhama katika mji wa Makka na kuhamia Madina kwa sababu kikwazo kilikuwa zaidi ni jamaa zake lakini nashukuru mwanyezi Mungu mimi sitohama na nitaendelea kuwa na nyinyi katika kipindi chote ambacho Mwenyezi Mungu atatuweka katika hali ya dunia.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa ya ufasaha na naamini wajumbe wameifahamu vizuri na kuweza kuichangia kikamilifu na pia leo watakuwa tayari kuichangia hata wale waliosema wanaichangia nusu, najua ni utani tu lakini wako tayari kuichangia kwa sababu ni hotuba nzuri na inaleta matumaini katika kipindi kijacho na kipindi kilichopita.

Mhe. Spika, vile vile nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na wajumbe wote wa kamati hii kwa mashirikiano mazuri waliyotupa katika wizara yetu, naipongeza pia kamati hii kwa hotuba yao nzuri na yenye maelekezo ya wizara yetu ambayo tunaahidi kuyafanyia kazi. Pia namshukuru Mhe. Asaa Othman Hamad waziri kivuli wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa hotuba yake ya kutoa maoni kwa kambi ya upinzani juu ya maeneo ya kufanyiwa kazi zaidi na wizara yetu ambae na yeye tunamshukuru kwa kuwa alikuwa ni miongoni mwa wafanyakazi wetu wa kilimo.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Mifugo na Mazingira nachukua nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote waliochangia na hata wale waliokuwa hawakupata nafasi ya kuchangia kwa mashirikiano mazuri ya Wizara yetu, baada ya shukurani hizo sasa naomba kusema machache juu ya hota zilizotolewa na waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Spika, baadhi ya wajumbe walionyeshwa kutoridhika na utendaji wa

baadhi ya mabwana na mabibi shamba kulalamika kwamba hawafiki katika maeneo yao ya wakulima na kuwasaidia. Napenda kutoa ufafanuzi juu ya suala hili kusema kwamba hadi sasa wataalam wa kilimo ni wachache kwa kuweza kuwafikia wakulima wote nchini. Kutokana na hali hii wizara inachukua jitihada za kuwapatika taaluma kupitia vikundi vya wakulima na skuli za wakulima.

Pia napenda kuwaelezwa Waheshimiwa wajumbe mara nyingi wamekuwa wakituuliza suala la kwamba ni lini tutaweza kufikia idadi ya wataalam ambao tunawataka, sasa tuna wataalam ambao wamo ndani ya hili baraza lako tukufu wanatoka Wizara ya Kilimo, mimi siwezi kuwaambia wacha Baraza la Wawakilishi na kurejea kilimo tena, lakini pia kuna yale mambo ya mungu ambayo yanapita wapo wataalam ambao tunawasomesha lakini baadae Mwenyezi Mungu anachukua roho zao kwa kufariki duinia, kwa hivyo kila pale serikali itakapopata nafasi itaendelea kuongeza idadi ya wataalam ili waweze kukidhi mahitaji yetu.

Mhe. Spika, katika tatizo la kukabiliana na upungufu wa madaktari wa mifugo wizara hivi karibuni ilifundisha watoa huduma za msingi kwa wafugaji vijijini tisini kutoka wilaya zote za Unguja na Pemba isipokuwa wilaya ya mjini kwa ajili ya kutoa huduma hizo na kuziba pengo la madaktari liliopo hivi sasa. Hata hivyo pia inaonyesha vijana hao kujiajiri wenyewe kwa vile baada ya mafunzo hayo walipatiwa zana za kufanyia kazi. Hivi sasa Wizara inakusudia vijana wote waliohitimu mafunzo ya cheti katika chuo chetu cha kilimo cha Kizimbani kuajiriwa na kupelekwa vijijini kufanya kazi ya mabibi na mwabwana shamba hii itasaidia kuondosha upungufu wa wataalam wa kilimo katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Aidha Idara inakusudia kuongeza idadi ya skuli za wakulima ili kutoa taaluma zaidi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mhe. Spika, wanyama kazi ni wanyama waliopata mafunzo maalum na hutumiwa kufanya kazi ili kumrahisishia binaadam katika kazi zake za kiuchumi na maendeleo, kazi hizo ni pamoja na usafiri na usafirishaji wa bidhaa pamoja na kulima, ni kweli kwamba wanyama kazi kama ng'ombe na punda kwa hapa kwetu wanapata mateso kutoka kwa baadhi ya watu, wizara yetu kwa kushirikiana na *World Society Protection* imeanza utaratibu wa kufuatilia watu hawa na kuwachukulia hatua za kisheria.

Wizara pia inaendelea kutoa taaluma kwa wananchi juu ya matumizi bora ya wanyama kazi hawa, pia wizara imeshajihidhi waanzishaji wa jumuiya zisizo za kiserikali kusaidia juhudi za serikali kudhibiti uhalifu huu. Jumla ya jumuiya tatu zimeanzishwa na zinaendelea na juhudi hizi, napenda kuliarifu baraza lako tukufu kwamba wizara hivi karibuni itaipitia sheria ya mifugo kuiweka makali

zaidi ya kuwabana wahalifu hao wanaotumia vibaya wanayamakazi.

Mhe. Spika, hivi karibuni nilifanya ziara kwenye maeneo ya wakulima katika wilaya zote za kisiwa cha Pemba nilichokiona ni maendeleo ya kupigiwa mfano ambayo wakulima wameyapata kwa msaada wa wataalam wa kilimo, naomba waheshimiwa wawakilishi kumega muda wao makusudi kuwatembelea wakulima katika maeneo yao na kuona hatua zilizofikiwa, napenda kueleza kwamba lengo kubwa la kuchanja mbwa na paka kuzuia uzazi ni kulinda afya za binaadamu. Mbwa na paka ni wanyama ambao wanasambaza maradhi ya kichaa cha mbwa kwa njia ya kuuma wanyama wengine na binaadam.

Hivyo kudhibiti hali hii mpango maalum wa kuwachanja dhidi ya maradhi hayo huandaliwa na kutekelezwa, ng'ombe na mbuzi hawana uwezo wa kuweza kupata maradhi hayo hivyo huwa hawaingizwi katika chanjo hii, aidha wanyama hawa hutolewa uzazi kwa vile tu hawana wamiliki na hubaki kudhurura ovyo mitaani na kuongezeka kwa kasi, hali ambayo haipendezi pia na inahatarisha maisha ya binaadam.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mama yetu Biashura Abeid Faraji kwa ushauri wake mzuri aliotupatia na tunaahidi kuuendeleza, hata hivyo naomba kumjulisha kwamba shamba la Mtakata hivi sasa haliko katika umiliki wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira shamba hilo wamepatiwa wenzetu wa ZSTC kwa ajili ya uzalishaji wa mikaratusi na michai chai kwa ajili ya matumizi ya kiwanda cha makonywe.

Mhe. Spika, suala la upatikanaji wa mbegu mpya umeulizwa na wajumbe wengi napenda kuwaeleza kwamba mbegu mpya zilizozalishwa hivi sasa zipo katika utaratibu wa kuzalishwa zaidi kwa ajili ya kuweza kusambazwa kwa wakulima wengi zaidi wa Unguja na Pemba, wakulima wapatao thamanini elfu Unguja na Pemba walipatiwa mbegu za muhogo kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu hizo na kuzisambaza kwa wakulima wengine, hivi sasa jumla ya wakulima wa mihogo elfu nane wameshapata mbegu hizo tangu mwezi Disemba, 2007.

Kuhusu mbegu mpya za mpunga hizi zimetoka katika mwezi wa March, 2010 kwa kuanzia na wakulima kumi na tano kutoka Wilaya za Unguja wamepatiwa mbegu hizo kwa wazalishaji wa mbegu, kwa Pemba wakulima kumi kwa ajili ya bonde walilopatiwa mbegu hizo. Mabonde hayo ni Mangwena, Uweni, Saninja na Tibirinzi aidha vituo vya kilimo pia vinaendelea kuzalisha mbegu hizi ili kuwa na uwezo wa kuwapatia wakulima wengi zaidi katika misimu ijayo ya kilimo cha mpunga.

Mhe. Spika, utaratibu unaotumika katika kuchukua takwimu za uzalishaji wa

mazao ni kuchukua sampuli ya mavuno katika maeneo mbali mbali ya uzalishaji, utaratibu huu hutegemea eneo dogo huchaguliwa katika kila sampuli na mavuno hufanyika katika eneo hilo, mavuno hayo hupimwa na baadae hujumuishwa na kupata wastani wa uzalishaji kutokana na eka zilizolimwa katika nchi nzima. Utaratibu hufanyika kwa mwaka mazao tofauti ndio mwanzo wa takwimu na uzalishaji ndio zinazotumika na wizara na Afisi na mtakwimu mkuu wa serikali. Mhe. Spika, naomba kuwatoa wasi wasi wajumbe wako kwamba utaratibu huo ndio unaotumika kwa nchi zote za Afrika.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache naomba kurudia tena kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mhe. Waziri kwa mashirikiano yake mazuri kwangu, namshukuru karibu mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, namshukuru Afisa Mdhamini wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maziangira, Kamishna, Wakurugenzi pamoja na watendaji wote wa wizara lakini pia nampongeza sana yule mwenzangu Mkurugenzi ambae ameamua kunifuata jimboni kuja kugombea. Namuomba asiwe na wasi wasi wowote kipindi kilichopita nataka nimhakikishie mimi niligombea na shemeji yangu ambae amemuoa mdogo wangu baba mmoja mama mmoja, kwa hivyo suala la Mkurugenzi kuja hakuna matatizo muhimu tufuate utaratibu wa uchaguzi.

Namuomba Mwenyezi Mungu akitujaalia nikishinda anisaidie na akishinda yeye nitamsaidia kama chama kinavyoendelea na utaratibu wake.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Uzini naomba kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi vifimbo mpaka nyumbani vinaingia ee. *(Kicheko).*

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, na Mazingira: Mhe. Spika, awali ya yote tumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhanah Wataala* kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kwa kuwa hai na uzima wa afya na kuweza kuhudhuria hii leo na kuendelea na shughuli zetu za Baraza la Wawakilishi kuhusu bajeti ya serikali ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, pili nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho juu ya hoja mbali mbali zilizoulizwa na waheshimiwa wajumbe, kwa kweli wajumbe wamechangia vuziri hotuba yetu na tunawapongeza sana na tunajitahidi

Mhe. Spika. tunawaomba wajumbe wale wanaotoka kwa dharura basi wasisahau kurudi kwa sababu tutahitaji kuja kuamua hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Tutajitahidi kama alivyotangulia Mhe. Naibu Waziri wangu ambae kwa kweli nampongeza sana kajibu vizuri sana baadhi ya hoja zilizoulizwa na wajumbe.

Mhe. Spika, hotuba yangu imechangiwa na Waheshimiwa wajumbe ishirini na sita na watano kwa maandishi naomba kuwataja kabla sijaendelea kujibu hoja.

1. Mhe. Assaa Othman Hamad
2. Mhe. Salmin Awadha Salmin
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Said Khelef Ali,
5. Mhe. Omar Ali Jadi
6. Mhe. Subeit Khamis Faki
7. Mhe. Said Ali Mbarouk
8. Mhe. Haji Faki Shaali,
9. Mhe. Moh'd Ali Salim
10. Mhe. Rashid Seif Suleiman,
11. Mhe. Ashura Abeid Faraji
12. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
13. Mhe. Asha Moh'd Hilal
14. Mhe. Ame Mati Wadi
15. Mhe. Salim Abdalla Hemed
16. Mhe. Najma Khalfan Juma
17. Mhe. Zakiya Omar Juma
18. Mhe. Ame Ussi Juma
19. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
20. Mhe. Abubakar Khamis Bakary
21. Mhe. Hasnuu Moh'd Haji
22. Mhe. Abass Juma Mhunzi
23. Mhe. Muhidin Moh'd Muhidin,
24. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk
25. Mhe. Zahra Ali Hamad
26. Mhe. Khatib Suleiman Bakari.

Mhe. Spika waliochangia kwa maandishi ni ;-

Mhe. Mahamoud Thabit Kombo
Mhe. Dadi Faki Dadi
Mhe. Omar Ali Shehe
Ali Suleiman Ali na
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi,

Kiukweli hao wote tunawapongeza kwa michango yao mizuri sana.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea kwa ruhusa yako naomba kuna baadhi ya wajumbe hapa kama Mhe. Haji Faki Shaali na wengineo walitaka baadhi ya mambo hapa tuwaletee kwa hivyo naomba tuwakabidhi watumishi wetu wawasilishe kwa wajumbe wetu wapitie. Kwanza ni suala la kalenda za upandeaji, lakini la pili ni kama lilivyotakiwa ni *Zanzibar good balance sheet report* ambazo hizi tatu naomba zisambazwe kwa wajumbe.

Mhe. Spika, nikiendelea kujibu hoja za wajumbe nawashukuru kwa kuchangia vizuri hotuba yangu napenda kuwahakikishia kwamba michango yao, maelekezo na ushauri tumeyapokea na tutayaranyia kazi ipasavyo kadiri ya uwezo utakavyoturuhusu, kwa utekelezaji mzuri wa majukumu ya maendeleo ya wizara yangu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira, kama nilivyosema amenisaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu wizarani na vile vile nampongeza kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi Mhe. Salmin Awadh Salmin kwa hotuba yake nzuri iliyojaa michango mizuri ambayo tunaahidi kuifanyia kazi kikamilifu, namshukuru na nampongeza sana Mhe. Waziri Kivuli wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira Mhe. Assa Othman Hamad kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba yake na michango yake iliyolenga kuimarisha sekta ya kilimo na kukuza uchumi, ambayo nayo vile vile tumeipokea na tutaifanyia kazi.

Mhe. Spika, tunatoa pongezi kwa heshima kubwa sana zilizotolewa kwa wizara yangu au kwetu kwa wafanyakazi kwa niaba ya wafanyakazi wa wizara yangu tumezipokea pongezi hizo na tunawashukuru sana na tunawaambia ahsanteni sana wajumbe wawakilishi.

Mhe. Spika, hotuba ya wizara yangu imechangiwa kama nilivyosema sina haja ya kurejea kwa ruhusa yako sasa naomba kujibu hoja za waheshimiwa wajumbe wa baraza lako tukufu kama ifuatavyo.

Kama nilivyokwisha kueleza hapo awali kwamba tumechukua michango yote yaliyokwisha kutolewa na Kamati ya Fedha na Uchumi hivyo kwa ruhusa yako naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu michango ya Wizara ya kuimarisha eneo la karantini la Kisakasaka kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba hali ya eneo la karantini la mifugo la Kisakasaka

sio ya kuridhisha na wizara baada ya kuona hilo imefanya mazungumza na Wizara ya Fedha na Uchumi na tayari tumeshapatiwa fedha kwa ajili ya kupeleka umeme katika eneo hilo, kazi ya kuweka umeme uo inatarajiwa kuanza hivi karibuni. Aidha wizara imetenga jumla ya shilingi milioni mia moja katika bajeti ya mwaka 2010/2011 kwa ajili ya kufanyia ukarabati wa majengo ya Kisakasaka likiwemo jengo la chinjio na Afisi aidha shamba litaimarishwa kwa ufyekwaji na kuwekwa uzio kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mhe. Spika, hotuba ya Mhe. Waziri Kivuli kwa mara nyengine tena namshukuru sana Mhe. Assa Othman Hamad kwa michango yake na naomba kutoa ufafanuzi kwa hoja alizozitoa kama ifuatavyo.
Kwanza kuhusu hoja ya kubinafsishwa zao la karafuu ambalo hili litakuwa kwa wajumbe wengi sana waliozungumza suala hili sasa litakuwa ni jibu la pamoja, hoja ambayo pia iliguswa na Mhe. Zakiya Omar Juma na Mhe. Suleiman Hemed Khamis napenda kwa mara nyengine tena kueleza kwamba serikali inaendelea na hatua zinaendelea kuanywa na wataalam waliofanya utafiti wa kina kwa hali ya soko la zao la karafuu hapa nchini ikiwemo utekelezaji wa mkakati wa kuimarisha zao la karafuu, yaani *Zanzibar Cloves State.*

Mhe. Spika, serikali inaendelea na hatua za kuimarisha zao la karafuu kwa kuhamasisha wakulima kupanda kwa wingi mikarafuu na kuitunza ili kuongeza uzalishaji, kuhusu ufinyu wa bajeti iliyotengwa kwa uimarishaji wa zao la karafuu napenda kueleza kuwa bajeti hiyo iliyotengwa ni kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya mikarafuu tu, kazi ambayo pia inasaidiwa kifedadha na Shirika la Biashara la Taifa *(ZSTC)* wakulima wenyewe wanalazimika kuendelea kutunza mashamba yao kwa kuyaweka katika hali ya usafi.

Hapa napenda kueleza kwamba kama nilivyokutaka Mhe. Abubakary Khamis Bakary na wengineo kusema kwamba atamko la serikali juu ya suala zima la karafuu serikali inasema kwamba mpaka sasa hivi karafuu ni zao moja kubwa sana la uchumi kwa maendeleo ya nchi, kwa hivyo suala la kubinafsisha kama nilivyosema kwamba tunangojea ripoti ya wataalam jinsi itakavyotueleza. Lakini kwa kifupi mpaka sasa hivi serikali kupitia wizara yake inalithamini sana zao la karafuu na tunaomba liendelezwe na wakulima wa karafuu na serikali hadi sasa itakuwa tayari kuwasaidia wakulima kadri itakavyowezekana. Kwa hivyo suala la tamko hasa tusubiri utafiti utakaavyoelekeza au kutushauri.

Mhe. Assaa Othman Hamad alitaka kujua kwa kiasi gani kuweko kwa pembejeo kumeweza kuongeza uzalishaji na kupunguza uagizishiaji wa chakula hapa nchini hasa mchele na wakulima wangapi wanaatumia pembejeo hizo, nashukuru sana kwa suala hili zuri ambalo limeulizwa na wajumbe wengi kuhusu suala hili la mchele. Mahitaji ya mchele hapa Zanzibar yanakisiwa

kuwa tani laki moja kwa mwaka na hadi sasa uzalishaji wa ndani ni asilimia ishirini tu ya mahitaji hayo, hata hivyo hali ya uzalishaji inaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka, Takwimu za mahitaji ya vyakula mbali mbali zipo katika taarifa maalum ya hali ya upatikanaji wa chakula nchini *(food balance sheet)* ambayo inatarajiwa kutolewa hivi karibuni ambayo ndiyo hiyo tuliyoisambaza hiyo ndio itakayokupa hasa picha ya hali ya chakula nchini.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri Kivuli pia alitaka kujua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi jinsi gani imefanikiwa katika kuongeza tija na uzalishaji. Katika kufikia malengo hayo Wizara kupitia miradi yake mbali mbali imekuwa ikitoa taaluma kwa wakulima na wafugaji kupitia Skuli za Wakulima. Mafunzo hayo yamelenga kilimo cha ufugaji bora, ikiwemo matumizi ya zana za kisasa, mbegu bora, matumizi ya mbolea, kupanda kwa wakati na masafa yaliyokubaliwa. Kuimarisha huduma za kinga na tija kwa mimea na mifugo nakadhalika. Haya yote yanalenga kuongeza tija ya uzalishaji.

Mhe. Spika, upo ushahidi wa kutosha kwamba kwa ukulima wanaotumia utaalamu wanaopata kutokana na mafunzo wanayopewa ya kuongeza uzalishaji wa eneo. Wapo wakulima ambao wamepata mpunga wa kufikia wastani wa tani nane kwa hekta ikiwa mpunga wa kutegemea mvua, mahindi uzalishaji wa wastani wa tani nne kwa hekta na muhogo kufikia wastani wa tani 25 hadi 30 kwa hekta. Viwango hivi ni vikubwa na vinaonesha uwezo wetu wa kuongeza uzalishaji wa chakula.

Mhe. Spika, Wizara inaendelea kuimarisha kilimo cha matunda kwa kuwahimiza wapandaji wa miti ya matunda kila mwaka na kufanya jitihada ya kudhibiti nzi wa matunda ya uzalishaji umeongezeka kwa matunda mbali mbali hapa Zanzibar. Wizara tayari imeshaanzisha mashamba ya majaribio ya kuchanganya mazao ya viungo katika mashamba ya mikarafuu. Vile vile juhudi ya kukusanya mbegu ya mazao mbali mbali zimeanza kuchukuliwa katika shamba la Kizimbani kwa lengo la kuzalisha mbegu na miche ya kutosha ya mazao ya viungo na mpango ni kuanza kwa wakulima kwa mfano katika Wilaya ambazo mazao hayo yanastawi.

Mhe. Spika, naomba kumtoa wasi wasi Mhe. Waziri Kivuli kwamba serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha zaidi ya kutekeleza mpango mkuu wa umwagiliaji maji. Hivi karibuni kazi ya kufanya upembuzi yakinifu kwa mpango huo itafanyika kwa eneo lote la hekta 8,521 chini ya ufadhili wa *Bank ya Exim* ya Korea ya Kusini. Benki hiyo imeahidi kuzingatia ombi la serikali ya kupatia mkopo nafuu wa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji mara baada ya kumalizika upembezi huo. Vile vile juhudi zinaendelea za kuchumba visima vipya na kujenga misingi ya umwagiliaji maji katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba na tunatarajia kuongeza eneo lililolimwa kwa

umwagiliaji maji na hivi sasa kutoka hekta 730 hadi kufikia hekta 1200 ifikapo Juni, 2011.

Mhe. Spika, kazi ya kuwaimarisha wakulima kuanzisha vyama vya hakiba na mikopo wizara yangu imeendelea na kazi hiyo na hadi sasa nina fura kusema vyama vya Hakiba na Mikopo vya Wakulima vilivyosajiliwa rasmi ni 11.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, mwakilishi wa Jimbo la Kitope, yeye ameuliza kwamba ombi la kung'olewa vigogo vya minazi katika Hoteli ya Bravo ambao hutumia vigogo vya mnazi kwa kujenga.

Wizara inatoa tamko la kuzuia ujenzi huo kwa maandishi na nakala zake kusambazwa katika taasisi zote husika ikiwa pamoja na Afisi za Sheha wa Kiwengwa na Kituo cha Polisi Kiwengwa . Wizara haina taarifa kwamba muwekezaji huyo anaendelea na ujenzi huo. Hata hivyo suala hili tutalifatilia na kulichukulia hatua haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, jengine ni hoja ya vijana wanaochukuliwa katika Chuo cha Kilimo cha Kizimbani je, wana sifa gani? Ni kwamba vijana wanaochukuliwa kwa ajili ya mafunzo hayo ni wale waliomaliza elimu ya Sekondari ya kidatu cha nne ambao wamefaulu masomo ya sayansi pamoja na somo la hesabati. Pamoja na sifa hizo vijana hao tutakiwa kufanya mitihani maalum na kujiunga na chuo.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu Kilimo cha Umwagiliaji maji kipelekwe kwenye maeneo mengine zaidi ya mabonde ya Cheju, Kiboko na Bumbwisudi. Pia mpango mkuu wa umwagiliaji maji uenezwe katika maeneo makubwa na kwa kazi zaidi.

Ushauri tunaupokea na tunaufanyia kazi kila hali itakaporuhusu. Ufupi kwamba wengi wamezungumza suala la uimarisha wa ukulima wa umwagiliaji maji. Tungependa kusama kwamba kwa kweli hilo ndio lengo la Wizara na tumo katika kushirikiana na wafadhili au wahisani wan chi mbali mbali na washirika waweze kutusaidia ili tuweze kuandaa miundo mbinu katika maeneo yote yale ambayo yataweza kuanzisha ukulima wa umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, jengine alitaka kujua wakulima wa Jimbo la Pangeni wanashtakiwa kutokana na wakulima kulima na kuvuna ndani ya eneo la serikali wakati wanadai eneo la miti iliyomo ni mali yao.

Miembe na miti yote ya kudumu iliyomo ndani ya shamba la mifugo la Pengeni ni mali ya serikali na wizara haijaruhusu mtu yeyote kupanda miti ya kudumu ndani ya shamba hilo. Hata hivyo Wizara ilitoa vibali kwa kupanda mazao ya mihogo na viazi pamoja na matunda mengine ya muda mfupi.

Mhe. Spika, miembe na minazi iliyomo shambani humo ilipangwa, ilichukuliwa na serikali na waliokuwa wakimiliki miti hiyo wote walilipwa fidia. Hawa wanaovuna embe kwa hivi sasa wanavuna mali ya serikali na hili halikubaliki. Aidha wengi watu hao huvuna kwa kujificha wakijua vika kwamba kitendo wanachokifanya si sahihi. Hata hivyo Wizara itafanya ziara kwa makusudi katika shamba hilo na kumshirikisha Mhe. Mwakilishi wa jimbo hilo ili tuweze kupata ufumbuzi wa kudumu kwa pamoja.

Mhe. Spika, Mhe. Khelef Said Khelef mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini yeye alisema kwamba naomba kumjulisha Mheshimiwa kwamba Idara ya Mazingira inajukumu la kusimamia uhifadhi wa mazingira katika maeneo ya ardhi, angani na majini. Kutoa elimu ya mazingira na kushahisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira pamoja na kuratibu kufanya tathmini za mazingira. Hizo ni moja katika kazi zake kubwa ya Idara hii.

Kuhusu hoja yake kwamba jimbo la Bumbwini kuna wakulima wengi ambao wanahhitaji kuongezwa pembejeo karibu yao na mbolea na kadhalika. Napenda kumueleza kwamba kwa kuwa wakulima wa jimbo hili wangi wao wanalima katika bonde la jangwani ambalo lipo karibu na kituo chetu cha Muwanda, bado wakulima hao wanaweza kwenda kununua vituoni hapo ambapo ni karibu. Hata hivyo Wizara itaangalia uwezekano wa kuanzisha kituo cha kuuzia pembejeo katika eneo huko Bumbwini.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya kukatwa minazi kwa ajili ya kuchimba michanga nah ii kwa kweli hoja hii imeulizwa na waheshimiwa wengi ambao jibu litakuwa kwa pamoja.

Napenda kueleza kwamba minazi inayokatwa ni makosa, alinayefanya hivyo atachukuliwa hatua za kisheria. Kawaida maeneo yenye miti miti kama minazi huwa ruhusa haitolewi. Kabla ya ruhusa kutolewa taasisi zinazoshirikishwa ni Idara ya Misitu Mazingira, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara yaani (UUB) na Idara ya Majenzi na Wilaya husuka.

Mhe. Subeti mwakilishi wa jimbo la Micheweni yeye aliuliza kwamba je kilimo cha maweni wakulima hawapiti kutoa elimu.

Tunaomba kumjulisha Mheshimiwa Mwakilishi kwamba Wizara ya Kilimo kupitia programu ya JP 5 ilitoa mafunzo katika shehia sita zilizomo katika jimbo lake la Micheweni. Wakulima wamepatiwa taaluma za ushalishaji mazao aina tofauti kama viazi vikuu, migomba, uwele, mtama pamoja na mboga mboga. Aidha baadhi ya wakulima walipewa mbegu za viwazi vikuu bure na kusaidiwa kupanda wale ambao walikubali kufata elimu hiyo wameona

mafaniko yake na bado wanahitaji mbegu hiyo ya viazi vikuu.

Mhe. Spika, sambamba na hilo kupitia programu ya ASSP jumla ya skuli nane za wakulima wa Wilaya ya Micheweni wamepatiwa mbegu za aina tatu za muhogo, Kizimbani, Machui na Mahonda, baada ya wakulima wengi kuona ubora wa mbegu hizo na wao wameanza kuzalisha kwa lengo la kuwauzia wakulima waziwao.

Mhe. Spika, Mhe. Said Ali Mbarouk Mwakilishi wa Gando yeye aliuliza kwamba hadi sasa Wizara imefikia hatua gani kuhusu kuipa hadhi karakana na matrekta.

Mhe. Spika, wizara tayari imeanza kuchukua hatua ya kuijengea uwezo karakana zetu mbili za matrekta. Hivi karibuni Wizara imenunua gari mbili aina ya *double Cabin Picup* kwa karakana ya Unguja na moja kwa karakana ya Pemba. Pia mafundi na madereva wa trekta wamepatiwa mafunzo na itaendelea kutolewa kila mara kwa lengo la kuwajengea uwezo mafundi na wafanyakazi hao. Aidha hivi karibuni vifaa vya zana vya kutendea kazi zimenunuliwa, vifaa hivyo vimegharimu jumla ya dola za Marekani laki moja.

Mhe. Spika, wizara pia inazingatia muundo mpya wa uendeshaji wa karakana ya matrekta. Hivi karibuni Wizara itatoa mapendekezo serikalini ya muundo muwafaka wa karakana hiyo. Kama nilivyosema mara mwisho ubadilishwaji wa taasisi za serikali au uundwaji wa taasisi za serikali unafanywa na serikali kuu. Kwa hivyo wizara yetu ilichukua hatua ya kuishauri serikali kuu kwamba karakana hii ibadilishwe badala yake iwe idara au shirika. Kwa hivyo mambo ya kiserikali yana utaratibu wake.

Hivi karibuni kama nilivyosema hapa kwamba tunamaliza maandiko fulani tuweze kwenda tena serikalini kuweza kuishauri karakana hii ima iwe Shirika, Idara au Serikali itakavyoona vyenginevyo. Kwa ufupi kwamba suala la kuimarishwa kwa karakana hii kiutendaji lakini vifao vimo kuchukuliwa.

Mhe. Spika, Wizara pia inazingatia muundo mpa kama alivyosema. Mhe. Moh'd Salim Mula mwakilishi wa Jimbo la Mkoani yeye alitaka kujua, alitoa hoja kwamba hatua zilizofikiwa na mradi wa umwagiliaji maji katika eneo la Makombeni.

Mradi umeshaanza na kazi zifuatazo zimeshakamilika, Ujenzi ya afisi na ghala upo katika hatua za kutiwa linta. Mamlaka ya Maji imeshalipwa na kazi ya uchimbaji kisima Kampuni ya Shatif Limitted imshalipwa kwa ajili ya ununuzi wa pamp na pia malipo yameshafanyika kwa Kampuni ya TANDEC Limitted kwa ajili ya ununuzi wa *transformer*.

Mhe. Spika, kuhusu ng'ombe waliopelekwa Wambaa ni wadogo na hawana mimba. Wizara yangu italifatilia suala hilo na sio kwa Wambaa tu bali kwa maeneo yote ya Unguja na Pemba na hatua muwafaka zitachukuliwa ili matatizo kama haya yasijitokeze mara nyengine sehemu zetu za Unguja na Pemba.

Mhe. Rashid Seif Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani alisema kwamba panapotokea ukame au majanga ya aina yoyote ambapo mkulima hukosa mazao wizara inachukua hatua tani.

Mhe. Spika, kwa msimu huu wa mwaka 2010 baadhi ya wakulima wetu walipatwa na jangwa la kuvamiwa na viwavi jeshi katika mashamba yao ya mpunga. Miongoni mwa hatua ambazo wizara ilichukua ni pamoja na kufanya tathmini ya eneo lililoathiriwa au lililoathirika na kuwaburugia tena konde zao pamoja na kuwapa mbegu nyengine wakulima hao bila ya malipo ambapo waliweza kupanda tena na kuwahi msimu. Hata hivyo ipo idara maalum inayoshuhulikia masuala ya majanga ambayo ipo chini ya Afisi ya Mhe. Waziri Kiongozi.

Kwa upande wa Wizara yatu linapotokea janga kama hilo basi mara maja ikiwezekana tunashirikiana na serikali kuu kuweza kupata msaada wa kuwasaidia wakulima ambao wamepata majanga kama hayo.

Kuhusu mitego ya nzi inayosambazwa maeneo ya Mjini Unguja na Wilaya ya Kati ya Kusini Unguja na kwa Pemba mitego imewekwa katika maeneo ishirini ya Wilaya ya Chakechake, na katika maeneo ya Ole, Kojani na Wilaya ya Wete.

Mhe. Ame Mati Wadi mwakilishi wa jimbo la Matemwe amesema kwamba ongezeko la mifugo ya kienyeji, ng'ombe, mbuzi na kuku wafugaji wapatiwe matibabu bure. Wizara itajitahidi kutoa huduma ya chanjo bure hasa kwa maradhi ya mripuko mfano Wizara ilifanya zoezi la chanjo kwa kuku wa kienyeji dhidi ya wagonjwa wa mahepe.

Mhe. Salim Abdallah Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe hoja alisema kwamba uvuvi wa kisasa kwamba je, na uvuvi unaofanywa na meli kubwa kama ile iliyokamatwa utaitwajwe.

Zipo aina tatu za kitaalamu za uvuvi, ya kwanza uvuvi mdogo mdogo ya piliuvuvi wa viwanda vya kati na aina ya tatu ya uvuvi unakuwa ni uvuvi wa viwanda kamili. Wavuvi wa Zanzibar wanavua uvuvi mdogo. Yaani hata hivyo wapo ambao wanaotumia zana za kisasa na wengine bado wanatumia zana

duni.

Mhe. Spika, muelekeo wa wizara ni kuwasaidia wavuvi wetu kuwapatia zana za kisasa zitakazowawezesha kuvua maji ya kati na maji ya bahari kuu.

Mhe. Najma Khalfan mwakilishi wa Viti maalum, alitaka kujua kwamba wizara inawaelimisha wananchi wanaoishi kando kando ya pwani juu ya umuhimu wa kupanda mikoko ili kuepukana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Wizara tayari imeshawaelimisha na inaendelea kuwaeilimisha wananchi wa ukanda huo na itaendelea kuwapatia elimu hiyo aidha kupitia maadhimisho ya siku ya mazingira duniani, wizara imeanzisha tunzo ya mazingira kwa taasisi zisizokuwa za serikali zenye kujishughulisha na uhifadhi wa mazingira kila mwaka ikiwa ni pamoja na tunzo ya mazingira kwa vikundi vinavyojishughulisha na upandaji miti ya juu pamoja na miti ya mikoko.
Kutoa taaluma kwa vijana wa Kizanzibari kuhusu usindikaji wa mazao.

Wizara kwa kushirikianana na Shirika la maendeleo ya Korea KOICA tayari tumeanza kujenga Chuo cha Mafunzo ya usarifu mazao na maabara huko Kizimbani na ujenzi huo unatarajia kumalizika mwezi wa November mwaka huu. Aidha mafunzo ya usarifu wa mazao kama maziwa, mbogamboga na mazao ya mizizi tayari yameanza kutolewa kwa vikundi mbali mbali vya wakulima kupitia promgramu ya AFFP na mradi wa PADEP.

Mhe. Spika, kuhusu hoja kwa eneo la karantini kwa upande wa kaskazini Unguja napenda kuelezea kwamba Wizara ina dhamiri hiyo na hivi sasa inatafuta eneo huko Kaskazini litakalofaa kwa shughuli za karantini ya mifugo. Mara tu litakapopatikana eneo hilo karantini hiyo itafunguliwa rasmin.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya Mhe. Zakia aliyetaka apate ufafanuzi wa aina za mafunzo yaliyotolewa na yatakayotolewa katika Chuo cha Kizimbani. Napenda kueleza kwamba tangu kuanzishwa kwa chuo mwaka 1998 Chuo kimekuwa kinatoa mafunzo ya stashahada yaani cheti katika fani ya Kilimo na Mifugo. Aidha chuo kimeazimia kuanzisha mafunzo ya ngazi ya stashahada diploma katika fani ya uzalishaji wa mazao pamoja na afya ya mifugo katika mwaka 2010/2011.

Mhe. Spika, Suleiman Hemed Mwakilishi wa Jimbo la Konde yeye aliuliza mpango wa Wizara kuondokana na mifugo yetu ya asili na kuwa na mifugo ya kisasa.

Wizara yangu ina lengo la kuondoa wafugaji wetu katika ufugaji wa kienyeji

kuelekea katika ufugaji wa kisasa. Kutimiza lengo hilo wizara inatoa mafunzo ya elimu ya ufugaji kupitia maafisa waogani na katika mashamba ya darasa. Hatua nyengine zinazochukuliwa za kubadili mifugo yetu ya asili mbali ya kugawa mifugo ya kisasa kwa wafugaji ng'ombe na mbuzi.

Wizara inashajihisha upandishaji wa ng'ombe na mbuzi kwa kutumia madume ya kisasa na upandishaji wa kutumia sindano wa ng'ombe. Kwa kuku wizara inagawa majogoo ya kisasa ili kuongeza kiwango cha ubora wa kuku wetu wa kienyeji.

Mhe. Abubakar Khamis wa jimbo la Mgogoni, Mhe. Juma Muhunzi Jimbo la Chambani, hoja kwamba takwimu zinaonyesha katika ukurasa wa 6 haziowani na takwimu za ukurasa wa 52, kiambatanisho na moja.

Mhe. Spika, hii nakiri kwamba yapo makosa ya uandishi katika paragrafu 2.2.3 takwimu sahihi ni zile zilizokuwepo katika jaduweli Nam.1 katika ukurasa wa 25, haya ni makosa ya kibinaadamu na paragrafu hiyo itafanyiwa marekebisho mara moja.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Abasi Juma Muhunzi kuhusu ufugaji wa nyuki haujapewa mkazo unaostahiki.

Wizara tayari imeshaanza kutekeleza mpango wa kuwahamasisha wananchi kuanza kazi ya ufugaji nyuki. Tayari kitengo kimeanzishwa katika Idara ya mazao ya biashara, matunda na misitu. Taaluma inatolewa na wananchi wanasaidiwa kupatiwa vifaa ikiwa na mizinga ya kisasa na nguo maalum za kazi hiyo. Hivi karibuni wizara imefanya mazungumzo na wawekezaji kutoka Iran, wawekezaji hao wametembelea maeneo ya ufugaji Unguja na Pemba na kuahidi kutoa misaada ya vifaa na kuanzisha kiwanda cha kusarifu asali.

Kilimo kimeongezeka kiasi gani kwa mujibu wa ongezeko la matrekta. Kiasi cha matrekta 45 na matrekta 21 mapya na yatakayoweza kufanya kazi katika msimu wa wakulima kwa mwaka huu 2010/2011. Kwa maana hiyo ongezeko la kilimo lililotajwa ndani ya kitabu hiki ni kwa mujibu wa matrekta yaliyotumiwa katika mwaka 2009/2010 tu. Kwa maana hiyo kwamba kuongezeka kwa matrekta kwa maka huu wa kilimo kilimo kitaongezeka.

Mhe. Muhidin alitaka kujua athari za mabadiliko ya tabia ya nchi. Ni kweli zipo athari za mazingira zinazotokana na mabadiliko ya hali ya nchi. Wizara yangu tayari imeshaanza kufanya tathmini ya athari hizo na kuzipitia kwa kuzihakiki athari hizo kwa kisiwa cha Pemba, tayari hatua hiyo inachukuliwa nakazi hiyo itaendelea kwa kisiwa cha Unguja. Athari zinazotokana ni pamoja na kuingia kwa maji ya chumvi katika maeneo ya kilimo, mmong'onyoko wa

fukwe wizara tayari imetekeleza mradi wa hifadhi ya misitu ya asili, kuhamasisha vikundi juu ya upandaji wa mikoko na kujitahidi kushajihisha matumizi ya nishati mbadala ikiwemo gesi na kutunza misitu. Vile vile ZAWE inafanya mawasiliano na mashirika ya maendeleo juu ya kuvumiliana na athari za mabadiliko ya ndani ya nchi.

Mhe. Muhidin alisema kuwa vijana kuvua bahati kuu watafaidika vipi vila ya zana, wizara ina mpango gani. Pili alisema Chole, Kengeja wanaingiliwa na meli za kigeni za uvuvi je, watasaidiwa vipi ili waweze kuvua katika maeneo yao.

Wizara yangu haitoi vibali kwa meli yoyote ile ya kiteni kuvua katika maeneo ya ndani uvuvi wa kienyeji, wanaovua huko ni wezi au wanavua haramu ambao njea pekee ya kuwasaidia ni kutumia vyombo vyetu vya dola ambapo tukiwafanyia hilo kuwakabili tunavyoweza tukishirikiana na Vikosi maalum vya KMKM.

Jengine Mhe. Abasi Juma Muhunzi alitaka kujua zao la mwani halijafanyiwa juhudi za kutosha uzalishaji wake umeshuka.

Mhe. Spika, zao la mwani lina sehemu mbili kubwa. Kwa mfumo wa aina yake mwani mwembamba ni jamii ya mwani inayoota kwa wingi sana katika kipindi cha mwaka mzima. Wizara yangu kwa makusudi kabisa imeshajihisha wakulima kupunguza aina hii ya mwani kutokana na bei yake kuwa ndogo au kutokidhi nguvu za kulima wanazopoteza kwa siku, badala yale kupitia mradi wa MACEMP tumeweza kwa kiasi kikubwa kuwapatia mradi mbadala ili kupunguza nguvu hii ya uzalishaji mwani mwembamba ambao kwa sasa huuzwa kwenye soko la dunia kama ilivyo karafuu.

Mwani mnene ni mwani ambao kwa kawaida yake hauoti vizuri na ni miongo mmoja tu, maana jamii hii huota zaidi vipindi vya baridi na hivyo hutegemea sana na hali ya hewa ndani ya kipindi cha mwaka mzima.

Mhe. Spika, kuhusu statement ya mikarafuu tumeshasema kwamba bado serikali haitachukua hatua ya kubinafsisha mpaka tupate ripoti ya utafiti unaofanywa. Suala la ripoti ile Mhe. Abubakar tulisema kwamba figa imekosewa na hatua za marekebisho zitachukuliwa.

Jengine ni suala la nzi wa mazao kama nilivyosema hatua zitachukuliwa za dawa za kienyeji na dawa za kuweka wadudu madume, mitego hii itaendelea kusambazwa zaidi Unguja na Pemba na sehemu mbali mbali.

Mhe. Hasnuu alisema matibabu ya mimea hayapatikani, dawa hazipatikani na

akashauri kwamba utafiti ufanywe.

Kwa kweli tafiti zitaendelea kufanywa za aina mbali mbali na za mazao mbali mbali. Madawa yapo ya kutosha na hapa kama hayo maeneo uliosema kwamba hayajafika basi mara moja tukimaliza hapa kikao tutawambia maofisa wetuu kuwasiliana mara Baraza letu hili likimalizika weje katika Jimbo lako au maeneo yako yaliyoathirika waweze kuona vipi watawaza kutusaidia kwa madawa na utaalamu.

Mhe. Spika, nimeulizwa habari ya tani ya vyakula ambavyo tumesambaza hizi warka, imeonesha mle namna gani ya mazao yalivyopatikana.

Wengine wametushauri kwamba vipando tupande kama vya zamani mbali mbali kama vitunguu thomu vinakuja katika maeneo ya maweni, karotina na kadhalika, hili vile vile tutalichukua. Na suala la kwamba wataalamu wetu hawapiti nafikiri Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba hawa waliopo tutajitahidi kuwambia wapiti. Lakini lengo kubwa sana kituo chetu cha Kizimbani ndio mbaana kinaendelea kusomesha ile idadi hasa tunayoitaka ya mabibi shamba na mabwana shamba haijafikia. Mara tu tukifikia idadi hiyo basi tutaona ikiwezekana kila Wilaya watakuwepo mabwana shamba na mabibi shamba wa kutosha ili waweze ikiwezekana kwa program maalum ya kuwatembelea wakulima kuweza kuwasaidia kuwalimisha katika upandeji na kuweza kuwatatulia matatizo yao.

Habari ya ng'ombe walioletwa kwamba ni wadogo hili tutahakikisha kwamba mambo haya hayatokei tena.

Mhe. Spika, suala la Mhe. Rais kwamba agizo lake halijatekelezwa suala hili tunalipokea na tunapenda kuwaahidi kwamba mara tu tutalifanyia kazi ipasavyo. Kama itawezekana basi tunaweza tukalilita na tukasambaza warka Barazani tuweze kuelezea hatua itakayofikiwa.

Mhe. Spika, Mhe. Muhunzi masuala yake tumejaribu kuyataja, kuyaeleza pale mwanzo pale mwanzo. Mhe. Spika, suala la mwani tumelieleza na suala la karafuu tumelieleza vya kutosha na tumejitayarisha vipi kuhusu tatizo la uchumi la dunia lilivyotokea.

Mhe. Spika, matayarisho ni kama tulivyosema kwamba ni moja tu kuongeza kilimo na kukifanya kilimo kiwe cha kisasa kwa kushirikiana na wakulima wenyewe na kushirikiana na wananchi kwa jumla na taasisi na serikali kuu kuweza kuongeza kilimo kwa njia mbali mbali. Suala la ufugaji wa samaki tunashukuru kwamba mnatupongeza kwa bwawa letu lile cha Chambani na tunaahidi kwamba moja katika malengo vile vile ni ….

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tumefikiwa na mgeni ambaye tayari yuko hapa ukumbini naye ni Mhe. Balozi wa Switzerland amekuja hapa ili kushirikiana na Kamati yetu ile ya watu sita kuhusu masuala ya taaluma ya mambo ya kura ya maoni. Lakini amependa aje hapa ukumbini kidogo ili aweze kuwasalimia wajumbe, kwa hiyo naomba nimtambulishe kwenu *His excellency the Ambassador of Switzerland Mr. Adrean Sheltha can I request him to stand to be seen by the members. Mr. Adrean Sheltha Ambassador yule pale we are very much delighted to see you and cooperate with our committee of six. Thanks very much for you come.*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kumkaribisha Mhe. Balozi, Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, vile vile alisema tutizame uwezekano kuwasaidia vijana wa Chambani katika masuala mazima ya ufugaji samaki na ukulima. Napenda kumuhakikishia Mhe. Muhunzi kwamba tutatuma ujumbe wa wataalamu kwenda kushirikiana na wewe na vijana wetu hao waweze kutizama vipi tutaweza kuwasaidia. Mhe. Muhunzi amesema anaipongeza *MACEMP* mimi pamoja na wafanyakazi wenzangu tunapokea pongezi hizo.

Mhe. Zahra Ali Hamad maelezo yake yote kama ni ushauri na kupongeza tumepokea na vile vile suala la wataalamu kwamba hawendi mashambani kama tulivyosema kwamba idadi ya kutosha bado haijakamilika lakini tutajitahidi kama tulivyosema tunaendelea kusomesha na hao waliopo basi tutatilia mkazo wapange programu ili wateremke mashambani kama alivyopendekeza.

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak na yeye amesema juu ya wataalamu hawa kwamba hawendi ameomba kwamba ufanye utafiti kwa madhara ambayo kidogo yaliyopanda kutokana na mbolea walioyoitia katika mashamba yao ya mihogo na kwenda kutizama uwezekano wa kutokea madhara. Kwa hivyo, tumepokea ombi hilo na tutatuma wataalamu katika mashamba yenu waje kutizama kama kuna athari zozote za mihogo hiyo mliyoipanda na kutoa ushauri mzuri.

Mhe. Spika, kwa ujumla yaliyobakia haya yote nafikiri ni suala la ushauri na maelekezo ya hapa na pale. Kwa hivyo, haya yote kwa kweli tumeyapokea na tunawaahidi kama tulivyosema kwamba haya yote waliyotuelekeza tumeyapokea na tutayafanyia kazi ipasavyo kwa mujibu wa hali itakavyoruhusu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa mara nyengine tena nawashukuru tena

wajumbe sana kwa michango yao mizuri ambayo kwa jumla michango yao kwa Mhe. Spika, ilikuwa ni michango ya kujenga na sio ya kulaumu, yote ilikuwa ni kujenga. Natumai kwamba wizara yetu ifanye vizuri zaidi ili tuweze kufanya kilimo cha kisasa na tuweze kujitosheleza badala ya kujitegemea kila kitu kutoka kwa majirani zetu. Mhe. Spika baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunamshukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake kwa ufafanuzi wa hoja mbali mbali na masuala mbali mbali yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na sasa tuamue. Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa mwaka 2010-2011 wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya wizara yangu sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mhe. Balozi ambaye nimemtambulishe hivi punde sasa hivi anatuaga anakwenda kufanya shughuli nyengine, tunashukuru sana.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 20 – WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA

Kifungu 03	-	Afisi Kuu Pemba	55,300.000
Kifungu 04	-	idara ya Mipango na Sera	925,474,.000

Mhe. Hasnuu Moh'd Haji: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia juu ya ahadi ya Mhe. Rais Mhe. Waziri katika majibu yake kidogo sikuridhika nayo na wawakilishi tulipewa ahadi ya kupewa mashamba ni sisi. Kwa hivyo, kikao hiki inaonekana kama ni kikao cha mwisho au huenda ikawa kuna kikao kimoja chengine mbele. Je, huo waraka utakaotolewa katika Baraza la Wawakilishi utakuwa unawasaidia wawakilishi wepi na sisi itakuwa hatupo tena.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri Mhe. Hasnuu sijui kama ndio ndipo hapa maana hapa tunajaribu kupitisha maeneo ambayo wanakusudia wenzetu hawa nao

wachangie mfuko mkuu wa serikali, kuna sehemu ya utawala huko mbele wakati wa matumizi labda unaweza ukauliza hilo. Lakini hapa hatuwezi tukawaambia kwamba msikusanye, nadhani tuendelee subiri huko mbele.

Kifungu 04	-	Idara ya Mipango na Sera	925,474.000
Kifungu 05	-	Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima	20,000.000
Kifungu 06	-	Idara ya Maendeleo ya Mifugo	48,000.000
Kifungu 07	-	Idara ya Mazao ya Biashara, Matunda na Misitu	175,000.000
Kifungu 08	-	Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini	60,000.000
Kifungu 09	-	Idara ya Mazingira	6,000.000
Kifungu 10	-	Idara yaVyama vya Ushirika	**4,000.000**
		Jumla ya Fungu	**1,293,774.000**

FUNGU 20 – WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA

Kifungu 03	-	Afisi Kuu Pemba	1,593,588.000
Kifungu 04	-	Idara ya Mipango na Sera	

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia katika hotuba ya Mhe. Waziri nilitoa azma ya kuzuia fungu la Idara ya Mipango na Sera ikiwa maelezo yangu juu ya hadhi ya Karakana Matrekta hayatakuwa yamenitosheleza, nina hakika maelezo ya Mhe. Waziri hayakunishawishi nisitimize azma yangu. Kwa kweli maelezo ndio yale yale ambayo nimeyapata mwaka 2007- 2008 na nikayapata tena mwaka jana 2009-2010 na mwaka huu tena nimepata maelezo yale yale. Hakuna kipya ambacho kimebadilika, bado ni kwamba serikali sijui wizara itashughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, la msingi katika masuala ya nini serikali inakusudia kufanya kuiondoa Karakana Matrekta kutokana na hali iliyo hamna. Kuna wenzetu walikuwa ni member wa bodi kina Mhe. Ame Mati Wadi sasa sijui wanafanya kazi gani. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo ya ziada ya Mhe. Waziri nini hasa wizara na serikali kwa jumla inakusudia kuiombea Karakana za Matrekta kutokana na hali iliyonayo hivi sasa ni mbaya.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika majumuisho kwamba suala la ubadilishaji wa taasisi za kiserikali kwa mfano uondoaji wa wizara, uondoaji wa idara, uondoaji wa shirika na kadhalika, hii hufanywa na Serikali Kuu. Sisi kwa upande wetu kuhusu Karakana zamani sana mara tu nafikiri tulipoingia madarakani

tulipopewa wizara ile tuliishauri serikali baada ya kutembelea kule na kuzungumza na wafanyakazi na viongozi tukaona kwamba ipo haja ibadilishe kutokana na hali yake, na badala yake iwe idara. Kwa bahati mapendekezo haya tukayapeleka serikali kuu, lakini serikali kuu ina utaratibu wake.

Kwa hivyo, wizara yangu baada ya kuona kwamba ipo haja ya kuendelezwa Karakana ile hatua tuliyoichukua kama tulivyoeleza tumeongeza vifaa vingi sana na tunaendelea kuongeza vifaa vingi katika Karakana ile. Vile vile tumesomesha na tunaendelea kusomesha mafundi wa Karakana ile na wafanyakazi wa Karakana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo tulivyosema kwamba bado suala la kuwasiliana na serikali kuu lipo na linaendelea na kwa taarifa yako labda ninong'oneze tu kwamba hivi karibuni mara tu baada ya kumaliza kikao hiki tuna azma ya kwenda kuonana na kiongozi wetu kuhusu mambo mbali mbali yanayohusu wizara yetu moja wapo ikiwa ni hilo. Kwa hivyo, huo ndio ushauri au ndio maelezo ambayo tunaweza kuyatoa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sisi wenyewe wizara tunajua fika kwamba hali ya Karakana ile sio nzuri, lakini pia tumechukua hatua kama tulivyoeleza tumeishauri serikali kuu na serikali kuu ina utaratibu wake, kwa sababu si wizara tu inayoweza kusema kwamba itafanya mabadiliko, sisi wizara tukakaa tukasema ah kuanzia leo iwe idara hapana, ni serikali kuu ndio inayowajibika na ushauri huo tumeshaupeleka.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa upande huo hatukungojea sisi kwamba tungojee agizo hilo au amri hiyo kutoka serikali kuu, lakini sisi wenyewe kama wizara tumechukua juhudi kubwa sana ya kukamilisha vifaa, nyenzo za utendaji na vile vile tumetoa mafunzo na bado tunaendelea kutoa mafunzo na vifaa. Kama nilivyosema kwamba baada ya Baraza hili kumalizika tunayo azma hiyo ya kwenda tena katika serikali kuu pamoja na mambo mengine ambayo tunataka kuyapeleka basi moja wapo itakuwa na hilo.

Mhe. Mwenyekiti, hili pia tujiulize kwamba nafikiri Mhe. Rais alitoa ushauri. Vile vile kwa upande mmoja tulikuwa na mwekezaji mmoja hivi karibuni tukawaambia hebu subirini kabla hatujachukua hatua yoyote na mwekezaji huyu alikuwa anatoka Urusi alitaka kufanya ubia na serikali kuhusu uendeshaji wa kiwanda kile.

Mhe. Mwenyekiti, tulikaa nafikiri kiasi ya miezi mitano mpaka sita tunamsubiri kuleta jibu lake. Mhe. Mwenyekiti, hatima yake tulipofuatilia serikalini tukaambiwa kwamba mwekezaji yule ameahiri hakuweka tena. Kwa ufupi Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio ambayo tunaweza kueleza kwamba sisi wenyewe

wizara na serikali tunajua kwamba hali ya Karakana ile sio nzuri kivifaa na vile vile kiutendaji.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nimeyasikia maelezo ya Mhe. Waziri kwa urefu sana na bahati nzuri serikali ambayo ameipelekea wazo imo katika Baraza kuna Waziri Kiongozi, msaidizi wake Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi wazo hili watakuwa wamelipata na hawakosi neno la kuiambia Baraza hili kuhusu nini hasa serikali inakusudia kufanya. Kwa hivyo, labda Mhe. Mwenyekiti, si vibaya serikali ikatusaidia maelezo inakusudia nini hasa baada ya kupata wazo la wizara mama kuhusiana na suala hili. Nafikiria ni suala zuri kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sisi tunaotembea pale na kamati tunaona aibu hasa, kwa hiyo serikali ipo basi tupate neno kutoka kwao linaweza likasaidia kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante nafikiri Mhe. Waziri ameeleza vizuri sana kwamba hili suala tumekuwa tunajadili muda mrefu na msingi hasa kweli tunakubali Mhe. Said kwamba vile viwanda vya Karakana pale Machomane na Mbweni kwa kweli palikufa na hata sisi tukulikuwa tunasema sasa huyu punda tumfanye vipi aendelee kuwa shirika au turudi idara. Kama alivyosema Mhe. Waziri amesema vizuri sana lakini sasa tutapawezesha vipi kwanza ikiwa mahali penyewe hapajarekebishwa.

Kwa hivyo, wizara wakaja na ombi kwamba tupajaze vitu au tupajenge upya kwa hiyo tunashukuru Mhe. Mwenyekiti, tukatumia pesa za MDRI tumenunua vitu vingi sana nafikiri viko njiani. Kwa hivyo, tukishakuviwezesha hivyo sasa tutaamua tulirudishe liwe shirika la meno yake sasa hivi linaweza kufanya kazi au tuifanye kama zamani iwe chini ya Idara ya Kilimo. Mhe. Mwenyekiti, uamuzi huo ni sentensi moja tu lakini kwanza tumeona hebu tuliwezeshe. Mhe. Mwenyekiti, alivyosema Mhe. Waziri ni sawa kabisa kwamba tunaliwezesha hatua hizo tayari tunamuahidi Mhe. Said *inshaallah* yeye ameshapita Jimbo la Gando na sisi atuombee Mungu tupite tukirudi hapa haturudi tena na kauli hii.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 04 - Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Hasnuu Moh'd Haji: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala ahadi ya Mhe. Rais sasa Mhe. Waziri sikusudii kumpa tabu lakini majibu yake alipotoa kidogo hayakuniridhisha kwa sababu sisi Rais aliyetupa ahadi ni wawakilishi tuliomo katika Baraza lako hili na kikao hiki inaonekana ndio kikao cha mwisho. Kwa hivyo, hizo shamba tutazipata kwa

utaratibu gani pindipo Baraza hili kama litakuwa limeshavunjwa. Naomba maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nafikiri Mhe. Rais akitoa agizo au ushauri au maelekezo basi taasisi husika huipokea na kuifanyia kazi, na kuna mambo mengine kama kawaida unaweza sasa hivi ukayapata na sasa hivi ukayafanyia kazi, kuna mambo unataka uchukue hatua kufanya utafiti, uulize hapa na pale, uwezekano utizame tena ndio unaweza kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hili tunasema kwamba sisi tumepata kama ni ushauri hebu tizameni huko wizara kama upo uwezekano Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama alivyofanya Mhe. Mansour tunampongeza akatupa viwanja kule Tunguu na sasa hivi ametupa tena kule Matemwe na Pemba ni kwamba walikuwa na uwezo huo. Mhe. Mwenyekiti, lakini sisi kuhusu mambo haya ya eka kwanza sisi wizara yetu haihusiki na eka, sisi wizara yetu hata yale maeneo tunayolima yako chini ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi sisi kazi yetu tumepewa tulime tu, leo yale yakitakiwa na serikali au wizara husika basi wanayachukua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi tunasema tena kwamba sio rahisi kusema kwamba nikatoa kauli hapa kwamba kesho tutawapatia hizi eka katika mashamba yetu ya kilimo. Kwa mfano, hivi sasa sisi kwa taarifa ya Baraza hili kuna wakulima waliokuwa wakilima maeneo ya Dole wamekuja kiasi miaka miwili iliyopita kama sikosei yale walikuwa wamevamia pale pahala bila ya wenyewe kujua. Mhe. Mwenyekiti, alipofanya ziara Mhe. Waziri Kiongozi alipofika pale wakamlalamikia kwamba sisi hapa tunalima miaka mitano lakini hatukupewa eka, eka wamepewa watu wengine na sisi tunaomba tumekosa nini na sisi ni wananchi. Mhe. Mwenyekiti, kikafanywa kikao sisi wizara yetu na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi pamoja na hao wananchi waliohusika. Hapo yakazungumzwa ikaonekana kwamba mabwana wale kweli wamevamia na kisheria ni kwamba walikuwa hawastahiki.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kwa upande wake ikatizama kwamba hawa ni binadamu na wanaishi hebu katizameni uwezekano wa kuwasaidia hawa angalau mkawapatia japo eka moja moja walime. Mhe. Mwenyekiti, mimi na Wizara ya Maji tukaunda kamati ya kwenda kupitia sehemu mbali mbali ya wizara yetu maeneo yetu ya ardhi na ikaonekana kwamba kwa kweli hakuna maeneo yaliyobakia ni madogo sana.

Lakini hayo hayo tukawaambia kwamba tutashirikiana na Wizara ya Maji yakapimwa na kwa taarifa yako hivi sasa wakati wowote watu wale watapewa hizo eka zilizokuwa zimepatikana. Kwa ufupi naweza kusema kwamba tatizo

kwa upande wetu kwenye wizara yetu sisi mpaka sasa hivi hatuna maeneo yaliyokuwa kwamba haya hatuyataki tuwape watu, hayo hatuna.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba suala hili sio rahisi ilivyokuwa limesemwa na Mhe.Rais lakini si rahisi kulitekeleza mara moja. Kwa hivyo, ipo haja kukaa tena ikiwezekana baada ya kumaliza kadhia inayoendelea ya watu wa Dole tukishamaliza hii tukae tena sasa kutizama je, waheshimiwa nao tutaweza kuwapatia vipi kwa kushirikiana na idara moja.

Kwa hivyo, kwa ufupi mpaka sasa hivi suala hili Mhe. Mwenyekiti, si rahisi kusema kwamba nitatoa kauli hapa kwamba kesho waheshimiwa nitawapatia eka, si kweli.

Mhe. Hasnuu Moh'd Haji: Mhe. Mwenyekiti, kwa kauli ya Mhe. Waziri inaonekana kauli ya Rais alipotoa kipindi kile kile wizara ilikuwa ina uwezo wa kusema kwamba haya masuala haiwezekani. Lakini sisi tulikuwa tunauliza kwa sababu hili suala limezungumzwa kwa muda mrefu na likawa bado halijapata ufumbuzi. Lakini kwa kauli ya Mhe. Waziri pamoja na kuwa ilikuwa inaufinyu ufinyu lakini huenda ikawa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote wanajua kwamba sasa zile shamba hazipo. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 04	-	Idara ya Mipango na Sera	936,965.00
Kifungu 05	-	Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima	2,448,319.000
Kifungu 06	-	Idara ya Maendeleo ya Mifugo	848,636,000
Kifungu 07	-	Idara ya Mazao ya Biashara, Matunda na Misitu	

Mhe. Haji Faki Shaali: Leo wala sio siku ya buti ya Mzee, lakini kuna mambo mengine nataka nimpongeze. Hii buti ni ya kumpongeza sio ya kumlaumu. Wakati Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilikuwa nina wasi wasi na takwimu za mazao. Bahati nzuri nikamuomba atupatie hiki kitabu wanachokiita *Zanzibar Food Balance Sheet Report*. Niliamini mimi kwamba kitabu hiki kitakuwa na majibu ninayoyahitaji na kweli yamo. Kwa mujibu wa kitabu hiki ambacho katupatia Mhe. Waziri ile hofu tuliyokuwanayo wajumbe kwamba hizi takwimu ni za kubabaisha ndio majibu yaliyomo katika hiki kitabu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kutupatia vitabu hivi na hivyo naomba tuendelee. Kwa sababu vile vitulivyofikiria wengi ndivyo hali ilivyo kweli kweli. Kwa hivyo, tuendelee.

Kifungu 07	-	Idara ya Mazao ya Biashara,	
	-	Matunda na Misitu	919,177,000

Kifungu 08	- I	dara ya Uvuvi na	
	-	Mazao ya Baharini	267,666,000

Kifungu 09

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa hii. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia sikusudii kumlaumu Mhe. Waziri wala kumtaabisha. Lakini nilipochangia nilimuomba kwamba serikali inachangia uharibifu wa mazingira. Sasa nikamtaka kwa sehemu zile zinazochimbwa kifusi basi wazitake zile kampuni baada ya kuchimba kifusi warudishe kidogo yale mashimo ili hali irudi kidogo. Kwa hivyo, jibu hilo hakunipa Mhe. Waziri nataka anipe jibu kidogo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Subeit Khamis Faki aliwahi kunambia kwamba kuna maeneo kule yanachimbwa na yamo katika hali mbaya sana. napenda kusema au kulifahamisha Baraza lako tukufu, kwamba mimi mwenyewe nimetembelea sehemu mbali mbali za Pemba na Unguja. Pemba hivi karibuni tu baada ya wiki mbili zilizopita kama sikosei nimerudi huko na sehemu zote nilizozitembelea hizo zinazolalamikiwa kwamba zimechimbwa mashimo hayajafukiwa ni kweli, maeneo mengi tu.

Hatua niliyochukua Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba, tumewasiliana na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi ambao kwa kweli ndio wahusika wakuu kwa sababu hao watengenezaji wa barabara ndio wachimbaji wakuu wa maeneo hayo. Nimemwambia kwamba itakuwa jambo la busara mara tu wakishachimba kifusi tena sio wachimbe, kwa sababu wengine kwa taarifa ya Baraza lako wanachimba kwa kweli ni hatari, maana yake ni eneo kubwa sana kwenda chini.

Mfano mmoja kule Bambi eneo fulani nafikiri watanisaidia watu wa Bambi mpaka yamechimbuka maji. Kwa hivyo, kama nilivyosema wajumbe kwa kweli hali si nzuri. Tumezungumza na Mhe. Waziri wa Mawasiliano kumwambia kwamba hawa mnaowapa *contractor* ya kutengeneza barabara, basi kwanza wahakikishe kwamba wawape kwa masharti, pamoja na mikataba ile, lakini kuwe kuna masharti kwamba mkichimba mchimbe mpaka *size* fulani na mkishachimba muweze kufukia.

Kwa upande wa wananchi kila utamofika katika sehemu zile uwaambie kwamba na wao hasa kule kwa rafiki yangu kunakochimbwa matofali, kwamba wakishachimba waweze kufukia na kupanda migomba na miti mingine tofauti. Kwa ufupi napenda kumhakikishia Mhe. Subeit kwamba sisi wizara yetu kwa kweli suala hilo halitupendezi hata kidogo. Tunaona ni baya na hatari.

Kwa mfano, hivi juzi nimekwenda ah, *geographically* ya kule Pemba inanishinda. Lakini tumekwenda katika sehemu moja ambayo nafikiri Vitongoji kama sikosei kuna ushirika wa kikundi kimoja kinajishughulisha na masuala ya uhifadhi wa mazingira. Wakatuchukua wakatupeleka sehemu fulani wakatuonesha shamba lao wanapanda mivinje mingi sana. lakini katika shamba hilo hilo kuna sehemu fulani tukaona hiyo hali ya uchimbaji wa hayo majabali namna mlivyochimbwa wale watengenezaji barabara hatari kubwa. Kwa sababu hatari yenyewe kwamba bahari iko kama hapo, nafikiri kipande kifupi sana ilipo barabara na hapa wanachimba mahandaki hatari kubwa sana.

Kwa hivyo, tumeona hali hiyo na kwa kweli kama nilivyosema tuliporudi tu mara tumeshirikiana na wenzetu kuwaambia kwamba ikiwezekana pahala pale tunawapigia marufuku pasiendelee kuchimbwa kuna hatari.

Mhe. Subeit napenda kukuhakikishia kwamba tunalijua na tutashirikiana na wizara husika kuweza kulisimamia suala hili lisiendelee kufanyika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema sikusudii kumsumbua Mzee wangu nilitaka nipate hilo jibu na jibu lake alilonipa limeniridhisha naomba tuendelee.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi hiyo. Nilipokuwa nachangia nilichangia Karakana nimerizika na majibu yake, lakini pia nilichangia suala la matumbawe. Matumbawe nilisema yanaharibiwa na baadhi ya wavuvi waharibifu, wanaripua mabaruti kwenye mazalio ya samaki na nyavu zinabakia mle sasa samaki hawazai vizuri na wengine wanakufa. Mhe. Waziri hakunambia kama hawa wataalamu watafanya vipi na adhabu gani itatolewa kwa hao wataokamatwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kweli Mhe. Asha Moh'd Hilal aliuliza suala hilo juu ya uharibifu wa matumbawe unaofanywa na baadhi ya wavuvi. Mhe. Mwenyekiti, suala hili Idara yetu ya Uvuvi chini ya uongozi wa Mkurugenzi wake Ndugu Mussa Aboud Jumbe linajulikana. Na hii sana inasababishwa na uvuvi haramu anaotumia baruti, mikuki na kadhalika.

Napenda kumhakikishia kwamba kwa kweli idara hii inajitahidi sana kuweza kupambana na waharibifu wa matumbawe. Kwa sababu inajulikana fika kwamba samaki wanategemea matumbawe ili kupatikana uzazi. Sasa ukiharibu matumbawe basi samaki unawafukuza. Kwa hivyo, hili tunalijua na bahati nzuri Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi yupo na amelisikia na ninaamini kwa ninavyomjua atalifuatilia kama ilivyo desturi yake.

Kwa kweli nipitie Baraza hili kutoa pongezi za dhati kwa Kikosi chetu maalum cha KMKM wanavyoshirikiana na idara hii bega kwa bega katika suala la kufuatilia uvuvi haramu. Kwa hivyo, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi Bi Asha, kwamba suala hili tumelipokea na bahati nzuri Mkurugenzi yupo amelisikia vizuri. Hizo hatua za kupiga vita hawa wavuvi haramu kama hawa wanaoharibu matumbawe ni kazi ya kila siku inayofanywa na wizara hii. Kwa hivyo, anavyotwambia Mheshimiwa kwamba tuzidishe juhudi katika kulinda matumbawe tunajitahidi. Ahsante.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 09	-	Idara ya Mazingira	199,803,000
Kifungu 10	-	Idara ya Vyama vya Ushirika	171,840,000
Kifungu 11	-	Idara ya Umwagiliaji Maji	369,006,000
Jumla ya Fungu:			**7,283,977,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 04	-	Idara ya Mipango na Sera	4,211,717,000
Kifungu 05	-	Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu kwa Wakulima	166,000,000
Kifungu 06	-	dara ya Maendeleo ya Mifugo	1,087,300,000
Kifungu 07	-	Idara ya Mazao ya Biashara, Matunda na Misitu	3,643,415,000
Kifungu 08	-	Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini	

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nilipokuwa nikichangia nilimtaka Mhe. Waziri kwa sababu uvuvi haramu unapigwa vita, aishawishi serikali aiwezeshe hii Idara ya Uvuvi ili wale wavuvi wapatiwe vifaa vywa kwenda kuvua nje. Lakini naona suala hilo sikulisikia hivyo, naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, lengo la idara hii ni ile ile aliyosema Mhe. Omar Ali Jadi, ni kuwawezesha wavuvi wetu waweze kuvua bahari kuu au maji makubwa, ili waweze kupata samaki wakubwa na kuongeza vipato vyao. Hilo ndio lengo letu la wizara na idara yetu. Lakini kila mambo kwa hatua. Hatua ya mwanzo tuliyoianza sasa hivi kupitia Mradi wa *MACEMP* ni kuweza kuwasaidia baadhi ya wavuvi. Jitihada hizo bado zinaendelea na zitaendelae kuwapatia boti za *engine* kubwa ili badala ya kuvua pale maji madogo madogo angalau watoke nje kidogo.

Lakini suala la kuwezesha wavuvi wetu hawa lipo nalo litajiri kuwapatia meli

tena sasa, kwenda katika Bahari Kuu. Sasa hilo kama nilivyosema kwamba mambo kwa hatua, haya tuliyonayo madogo hatuyawezi, tumo katika kuyachukulia hatua. Lakini lengo letu ikiwezekana kufumba na kufumbua wavuvi wetu waweze kwenda bahari kuu kuvua kwa meli hasa, hilo ndilo lengo letu.

Mhe. Mwenyekiti, tutakwenda kidogo kidogo mpaka tutafika, *provide* ni kwamba na sisi serikali yetu uchumi wetu utaongezeka na wafadhili watakuwa wanazidi kuendelea. Hili ndio lengo letu na tutaweza kuwasaidia kwa kuwapatai vyombo angalau vidogo vidogo vya moto ili watoke nje wakavue.
Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Omar Ali akawa na stahamala wakati wizara hii na serikali inajitahidi kufikisha lengo hilo.

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kwa sababu muda unapotea na majibu aliyotoa Mhe. Waziri ni mazuri basi sina maneno. Mimi nia yangu ni kumuondolea usumbufu Mkurugenzi ili kazi zake nzuri alizozifanya zisije zikaharibika njiani. Kwa hivyo, naomba awezeshwe na tuendelee. Ahsante sana.

Kifungu 08	-	Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini	9,85,000,000
Kifungu 09	-	Idara ya Mazingira	64,385,000
Kifungu 10	-	Idara ya Vyama vya Ushirika	40,000,000
Kifungu 11	-	Idara ya Umwagiliaji Maji	557,000,000
Jumla ya Fungu:			**19,619,817,000**

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makisio haya. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi wale wanaoafiki Makadirio hayo ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa kazi nzuri ambayo mmeshaifanya, sasa tusitishe shughuli zetu kwa sasa hivi hadi jioni.

(Saa 6:45 Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:
Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili lipokee, lijadili na hatimaye lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa kazi za kawaida na za maendeleo ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kwa kutuwezesha kukutana tena tukiwa wenye afya na uzima na kutujaalia nchi yetu kubakia katika hali ya amani na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara ninayoiongoza, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume kwa uongozi wake wa busara na juhudi zake kubwa anazoendelea kuchukua katika kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu na kuiletea maendeleo na mafanikio yanayouwezesha uchumi na ustawi wa jamii yetu kukua mwaka hadi mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mhe. Waziri Kiongozi kwa juhudi zake kubwa anazozichukua katika kumsaidia Rais wetu katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ninaendelea kukupongeza wewe pamoja na Mhe. Spika, Naibu Spika na Mwenyekiti mwengine wa Baraza, Katibu wa Baraza, Maofisa na wafanyakazi wote wa Baraza lako tukufu, kwa kufanya kazi kwa hekima na busara kubwa sana na kuliwezesha Baraza lako likaendelea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza hili la Wawakilishi. Mwenyezi Mungu akupe

maisha mema, afya na baraka uweze kuliongoza Baraza hili kwa utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo napenda kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza lako tukufu na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kwa mashirikiano makubwa waliyoipa Wizara yangu. Ushauri, mawazo na maelekezo yao tumeyapokea, tumeyathamini na yametusaidia sana katika kutekeleza vyema mujukumu ya wizara yetu. Nampongeza Waziri Kivuli kwa mashirikiano yake mazuri anayoipa Wizara yangu kila haja inapotokea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo na kama ulivyoniagiza, sasa niruhusu kutoa muhtasari wa maelezo ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kipindi cha mwaka 2010/2011. Katika muhtasari huu, nitaelezea mambo makuu ambayo Wizara yangu imeweza kuyatekeleza katika kipindi cha miaka mitano, yaani 2005/2006 hadi 2009/2010. Kisha nitayaeleza malengo ya mwaka wa fedha wa 2010/2011 ambayo Wizara inakusudia kuyatekeleza baada ya kupatiwa fedha tunazoziomba.

Utekelezaji kwa ukamilifu nitakabidhi kwa Wajumbe katika mfumo wa vitabu ambavyo baada ya kuzinduliwa rasmi na Mhe. Rais taarifa hiyo tutaikabidhi kabla ya kumaliza Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imeundwa na Taasisi zifuatazo:-

i. Idara ya Mipango na Sera,

ii. Idara ya Utamaduni,
iii. Idara ya Michezo,

iv. Idara ya Televisheni,

v. Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar,

vi. Idara ya Habari Maelezo,

vii. Idara ya Upigaji Chapa,

viii. Chuo cha Uandishi wa Habari,

ix. Shirika la Magazeti ya Serikali,

x. Tume ya Utangazaji; na

xi. Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara ilipangiwa kutumia sh. 3,953,243,000, /= kwa kazi za kawaida na sh. 1,067,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010 Wizara ilikwishapatiwa sh. 2,407,700,312/= kwa kazi za kawaida, sawa na asilimia 60.9 na sh. 853,040,000/= kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 79.9. (Tafadhali angalia Viambatanisho Nam. 1a na 1b).

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara ilipanga kukusanya mapato ya sh. 330,800,000/=. Hadi kufikia Machi 2010, Wizara imeweza kukusanya sh. 155,771,504/= sawa na asilimia 47 (Tafadhali angalia Kiambatanisho Nam. 1c)

MALENGO YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara yangu, kupitia taasisi zilizo chini yake, ilipanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

I. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli na mipango yote ya wizara;

II. Kusimamia ujenzi wa ofisi mpya za Idara ya Michezo na Baraza la Michezo baada ya idara hizo kuhamishwa katika maeneo ya uwanja wa Amaan na Kariakoo;

III. Kuendelea kuwasiliana na kushirikiana na washirika wa maendeleo kwa lengo la kutekeleza malengo ya Wizara;

IV. Kuendelea kutoa taaluma kwa wafanyakazi wa Wizara wa kike na wa kiume kuhusu kujikinga dhidi ya maradhi ya ukimwi;

V. Kuendelea kuratibu shughuli zote za Habari za Serikali;

VI. Kushirikiana na Taasisi za Serikali na Mashirika yasiyokuwa ya Serikali kuendelea kutayarisha vipindi kwa ajili ya kuoneshwa vijijini na mijini kwa kutumia gari letu la Sinema;

VII. Kusimamia ufungaji wa antena mpya na ununuzi wa kifaa

cha kudhibiti umeme *UPS* kwa ajili ya transmita ya Pemba, ili kuepuka ukatikaji wa vipindi mara kwa mara;

VIII. Ununuzi wa vifaa vya dijitali kwa ajili ya matengenezo makubwa ya studio za Karume House Unguja na Machomane Pemba;

IX. Kuendeleza mawasiliano na Serikali ya China juu ya kupatiwa misaada mbali mbali ambayo itaweza kusaidia katika uendelezaji wa mitambo iliyoko katika vituo vyetu;

X. Kuendelea kuwasomesha wafanyakazi wa kike na wa kiume mafunzo ya nadharia na vitendo katika viwango mbali mbali vya elimu na kufanya vipindi ambavyo vitasaidia kuelimisha jamii kuondokana na umaskini;

XI. Kuendeleza kufanya vipindi juu ya mapambano dhidi ya unyanyasaji wa jinsia, maradhi, yakiwemo ukimwi na ajira kwa watoto;

XII. Kufunga mtambo mpya wa MW–KW 50 na vifaa vyake ikiwa ni msaada mmoja wapo kutoka Jamhuri ya Watu wa China;

XIII. Kukamilisha kazi ya ufungaji mitambo miwili mipya ya FM 2KW mmoja Unguja na mmoja Pemba ili kusaidia urushaji wa matangazo ya mtambo wa masafa ya kati (MW/AM) na masafa mafupi (SW);

XIV. Kununua mitambo ili kutoa huduma bora za machapisho kwa Taasisi za Serikali na wananchi;

XV. Kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara baadhi ya mashine kongwe ili ziendelee kutoa huduma hasa za uchapishaji wa magazeti;

XVI. Kuwaelimisha na kuwapatia wananchi taarifa mbali mbali zinazohusu maendeleo yao kupitia makala mbali mbali za magazeti ya Serekali;

XVII. Kuliendesha kibiashara na kwa misingi ya kujitegemea Gazeti la Zanzibar Leo na mengine yatakayoanzishwa,

chini ya shirika hilo;

XVIII. Kuongeza ufanisi wa menejimenti, sifa na ubora wa magazeti yote yatakayochapishwa chini ya Shirika hili;

XIX. Kuongeza uwezo wa uchapishaji na usambazaji wa magazeti ya Shirika;

XX. Kukamilisha mchakato wa marekebisho ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 1997 kwa kuingiza mfumo wa utumiaji wa utangazaji wa dijitali;

XXI. Kuendeleza, kuelimisha na kuratibu urushaji wa matangazo kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya dijitali hadi kufikia kiwango kinachotegemewa;

XXII. Kuandaa muongozo wa matumizi wa vyombo vya utangazaji kulingana na Sheria namba 7 ya mwaka 1997 ya Tume ya Utangazaji kifungu namba 7 (1) (h);

XXIII. Kuimarisha Chuo kwa kununua vitendea kazi, samani za Chuo na kuajiri walimu wa kudumu na maafisa watendaji wa chuo pamoja na kukamilisha usajili wa Chuo kwenye *NACTE*;

XXIV. Kuanza kutoa mafunzo ya kiwango cha Diploma na kushajiisha taasisi na watu binafsi ili kuanzisha programu maalumu ya mafunzo ya muda mfupi ya utayarishaji vipindi na uandishi wa makala;

XXV. Kujenga uhusiano na vyombo mbali mbali ili kukifanya chuo kitambulike na kupata hadhi na umaarufu;

XXVI. Kuendelea na utafiti wa urithi wa utamaduni katika Wilaya zetu zote Unguja na Pemba;

XXVII. Kuandaa matamasha ya utamaduni kwa mashirikiano na vikundi vya utamaduni vya ndani na nje;

XXVIII. Kuendelea kurithisha mila, silka na utamaduni wetu kwa vizazi vyetu kupitia mafunzo ya Redio, Televisheni, Magazeti, Vipeperushi nk.;

XXIX. Kufufua utendaji kazi wa nyumba ya sanaa Mwanakwerekwe;

XXX. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii kwa kutumia semina na vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa kutunza na kulinda maadili ya jamii;

XXXI. Kuendelea kukagua na kuhakiki kanda za sanaa zinazouzwa madukani, na zinazoonyeshwa hadharani na kwenye matamasha mbali mbali;

XXXII. Kuelimisha jamii juu ya matumizi ya Kiswahili sahihi na fasaha kupitia vipindi vya redio, televisheni na makala za magazetini;

XXXIII. Kuchapisha miswada ya makamusi ya lahaja za Kitumbatu na Kimakunduchi, kukamilisha mswada wa kamusi la lahaja ya Kipemba na kusimamia uchapishaji wa kamusi la Kiswahili fasaha;

XXXIV. Kuandika kitabu cha Kiswahili kwa wageni na kufanya maadhimisho ya siku ya Kiswahili Zanzibar;

XXXV. Kuendelea kulitangaza Baraza la Sanaa na kazi zake kwa wasanii na vikundi vya sanaa;

XXXVI. Kusimamia utoaji wa leseni za shughuli za kisanii kwa watu binafsi na vikundi vya sanaa;

XXXVII. Kutoa elimu ya muamko juu ya usajili wa kazi za sanaa mbali mbali kwa wasanii Zanzibar;

XXXVIII. Kukuza mashirikiano na mabaraza ya sanaa ya ndani na nje ya Tanzania kwa lengo la kubadilishana ujuzi, uzoefu na utaalamu;

XXXIX. Kusimamia uwekaji nyasi bandia Uwanja wa Gombani kwa mashirikiano na Shirika la Kimataifa la Mchezo wa Mpira wa Miguu (*FIFA GOAL PROJECT No. 3*);

XL. Kusimamia upelekaji wa umeme na ufungaji wa taa

kwenye minara ya Uwanja wa Gombani;

XLI. Kuendelea kusimamia matengenezo ya Uwanja wa Amaan;

XLII. Kukamilisha ujenzi wa Akademia ya Michezo Dole;

XLIII. Kuendelea kukuza vipaji vya wanamichezo chipukizi wa umri wa chini ya miaka 15, 17 na 20 kwa kushirikiana na mradi wa *USPORT*, kupitia Akademia ya michezo na programu za vyama mbali mbali vya michezo;

XLIV. Kuwawezesha wanamichezo wetu kushiriki mashindano ya ndani na nje, kuandaa mashindano ya kitaifa na kimataifa, matamasha na bonanza za michezo;

XLV. Kuwapatia wanamichezo mafunzo ya ndani na nje ya nchi yanayohusu utawala, ualimu na uamuzi wa michezo; na mialiko ya mechi za kujipima nguvu (mechi za kirafiki);

XLVI. Kukamilisha uchaguzi wa viongozi wa Vyama vya Taifa vya Michezo ambavyo muda wao wa kuongoza umemalizika;

XLVII. Kusimamia marekebisho ya Katiba na kanuni za vyama vyote vya michezo ambazo hazikidhi haja;

XLVIII. Kuendeleza na kusimamia shughuli zote za utawala, na za maendeleo zilizopo Pemba;

XLIX. Kulifanyia matengenezo jengo la Afisi Kuu Pemba;

L. Kuweka Jenereta litakalokidhi haja ya umeme Ofisini na Kituo cha Redio Pemba; na

LI. Kukamilisha ujenzi na uwekaji mitambo kituo kipya cha Redio Jamii cha Micheweni.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2005/2010

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nieleze kwa ufupi mafanikio ya

utekelezaji wa malengo makuu ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2005/2010. Wizara yangu kupitia taasisi zilizo chini yake ilitekeleza mambo yafuatayo:-

i. Imejenga jengo jipya la Ofisi kuu ya wizara iliyoko Migombani Zanzibar, ofisi ya Idara na Baraza la Michezo, Baraza la Kiswahili Zanzibar na Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho huko Mwanakwerekwe;

ii. Imetayarisha Sera ya Habari ya 2006, Sera ya Michezo 2007, Sera ya Utangazaji 2008. Aidha, Sheria mbali mbali zimerekebishwa na nyengine kuandikwa upya. Sheria hizo ni Sheria Nam. 11 ya mwaka 2006 ya kuanzishwa Chuo cha Uandishi wa Habari, Sheria Nam. 11 ya mwaka 2008 ya kuanzisha Shirika la Magazeti ya Serekali, Sheria ya kuanzisha Baraza la Michezo Zanzibar ya 2010 na Marekebisho ya sheria ya kuanzishwa Tume ya Utangazaji Zanzibar;

iii. Imeweka mtambo mpya wa dijitali wa *medium wave* wa KW 50 kwa ajili ya kituo cha Sauti ya Tanzania Zanzibar huko Chumbuni. Aidha, STZ imepatiwa mitambo miwili ya FM ya KW2 ya dijitali na tepu rikoda za kisasa. Kutokana na kuimarika uwezo wake STZ sasa itaanza kutangaza kwa muda wa saa 18 mfululizo kuanzia tarehe 1 Julai, 2010 kama Baraza hili lilivyokuwa linashauri;

iv. Imeanzisha mafunzo ya kiwango cha Cheti na Diploma ya Uandishi wa Habari katika Chuo Cha Uandishi wa Habari cha Zanzibar;

v. Imefanya matengenezo makubwa ya Uwanja wa Amaan kwa msaada wa Jamhuri ya Watu wa China ili kiwanja hicho kiwe na hadhi ya Kimataifa. Vile vile kwa msaada wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Ulimwenguni *(FIFA)* Wizara imeanza kazi za kuweka nyasi bandia katika kiwanja cha Gombani Pemba;

vi. Imeanzisha ujenzi wa akademia ya michezo Dole ili kuibua vipaji vya wanamichezo chipukizi;

vii. Imekamilisha utafiti ambao umewezesha kuandika kitabu cha ramani ya urithi wa utamaduni wa Zanzibar; na

viii. Imejenga kituo cha kurushia matangazo cha Redio Jamii Micheweni - Pemba ili kuelimisha na kupasha habari jamii katika masuala mbali mbali ya maendeleo yakiwemo kupunguza umasikini.

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2009/2010

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara yangu kupitia taasisi mbali mbali zilizo chini yake iliweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli na mipango yote ya Wizara kwa Unguja na Pemba ;

ii. Imesimamia kujengwa kwa ofisi mpya ya Idara ya Michezo na Baraza la Michezo huko Mwanakwerekwe na hivi sasa

wafanyakazi wa Idara hizo tayari wameshahamia katika jengo hilo;

iii. Imeendelea kuwasiliana na kushirikiana na washirika wa maendeleo katika kutekeleza malengo ya Wizara kama vile *UNESCO*, Jamhuri ya Watu wa China, Misri, Japan, Ufaransa, Ujerumani, Marekani na *FIFA*;

iv. Imewapatia wafanyakazi wa kike na wa kiume mafunzo mbali mbali katika viwango vya cheti, stashahada, shahada ya kwanza na za pili. (Angalia kiambatanisho Nam. 2-14);

v. Imeendelea kutoa taaluma kwa wafanyakazi wa Wizara wa kike na wa kiume kuhusu kujikinga na maambukizo mapya na ukimwi pamoja na kufanya zoezi la upimaji wa hiari wa virusi vinavyosababisha ukimwi kwa wafanyakazi wa wizara, wanamichezo na wasanii;

vi. Imeendelea kushirikiana na Taasisi mbali mbali za serikali na watu binafsi kuonesha vipindi vya elimu na maendeleo kwa kutumia gari za sinema za Wizara zilizoko Unguja na Pemba. (Angalia kiambatanisho Nam. 15);

vii. Imeendelea kuratibu shughuli zote za Habari za Serikali pamoja na kuimarisha kitengo cha picha, vielelezo na maktaba ya picha kwa kutumia njia za kisasa;

viii. Imeendelea kuwaelimisha na kuwapatia wananchi taarifa mbali mbali zinazohusu maendeleo yao;

ix. Imeendelea kutoa huduma ya machapisho mbali mbali yakiwemo sheria, katiba, vyeti vya kuzaliwa na mambo mengineyo;

x. Imeweza kutengeneza mtambo mkubwa ambao unachapa gazeti la Zanzibar Leo na kuchapisha kazi maalum za kitaifa. Aidha, wizara imepata mshauri kutoka *Gazelle Limited* Nairobi, Kenya ambaye alishauri kufanyiwa matengenezo mitambo iliyopo na suala la kununua mtambo wa *Colour Seperation Unit* litafuata baadae;

xi. Imeanza kuliendesha Shirika la Magazeti ya Serekali kwa misingi ya kibiashara baada ya kukamilisha safu ya uongozi wa shirika na kuteuliwa kwa Bodi ya Shirika;

xii. Imekamilisha mchakato wa marekebisho ya sheria Nam. 7 ya mwaka 1997 ya Tume ya Utangazaji kwa kuingiza vipengele vya mfumo wa utumiaji wa utangazaji wa dijitali;

xiii. Imeendelea kutayarisha vipindi na kufanya mikutano na wafanyabiashara na wamiliki wa vituo vya utangazaji juu ya umuhimu wa kuzingatia ubora wakati wa uingizaji wa vifaa vya dijitali na hasara za kuendelea kuingiza vifaa vya analogi;

xiv. Imeendesha programu ya mafunzo juu ya njia bora za kutayarisha vipindi vyenye maudhui ya ndani na kutoa taaluma ya utangazaji;

xv. Imekamilisha kuandaa muongozo wa kuendeleza, kuelimisha na kuratibu urushaji wa matangazo kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya dijitali na kufikia kiwango kinachotarajiwa;

xvi. Imenunua vitendea kazi na samani za Chuo Cha Uandishi wa Habari kwa ajili ya watendaji wake mbali mbali na wanafunzi;

xvii. Imeweza kuwaajiri walimu watano wa kudumu na maafisa watendaji wakuu wa Chuo cha Uandishi wa Habari;

xviii. Imeweza kuanzisha mafunzo ya Diploma ya fani ya uandishi wa habari yanayotolewa katika Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar na hivi sasa kuna wanafunzi 40 wanaoendelea na masomo;

xix. Chuo cha Habari kimeendelea kujenga uhusiano na vyombo mbali mbali kama vile STZ, TVZ, Habari Maelezo na Baraza la Taifa la Kuthibitisha Vyuo vya Elimu ya Ufundi Tanzania *(NACTE)* ili kukifanya chuo kitambulike. Katika kujenga uhusiano huo Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi, na Utamaduni *(UNESCO)* limeahidi kusaidia miradi miwili ili kukijengea uwezo Chuo. Miradi hiyo ni kuifanyia mapitio mitaala yake ili kuiweka katika viwango vya kimataifa na mradi wa ujenzi wa studiona vifaa vyake kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi;

xx. Imeendelea kukamilisha taratibu za usajili wa Chuo kwenye Baraza la Taifa la Kuthibitisha Vyuo Vya Elimu ya Ufundi Tanzania.*(NACTE);*

xxi. Imesimamia utoaji wa leseni za shughuli za kisanii kwa watu binafsi na vikundi vya sanaa;

xxii. Imetoa elimu kwa wasanii wa Zanzibar ili wapate muamko juu ya usajili wa kazi za sanaa mbali mbali kwa wasanii;

xxiii. Imeendelea kukuza ushirikiano na mabaraza ya sanaa ya ndani na nje ya nchi ikiwemo BASATA Kikundi cha parapanda kwa lengo la kubadilisha ujuzi, uzoefu na utaalamu;

xxiv. Imekamilisha utafiti wa kuweka ramani ya urithi wa Utamaduni wa Zanzibar wilaya zote za Unguja na Pemba;

xxv. Imeviwezesha vikundi vya utamaduni kushiriki matamasha katika nchi mbalimbali pamoja na sherehe za kitaifa ndani ya nchi. (Angalia kiambatanisho Nam. 16);

xxvi. Imeendelea kutoa taaluma ya utamaduni na sanaa ili kurithisha mila, silka na desturi zetu kwa vizazi vyetu;

xxvii. Imeendelea kukagua na kuhakiki kazi za sanaa mbalimbali zikiwemo kanda za mchanganyiko zinazoonyeshwa kwa jamii. (Angalia kiambatanisho Nam.17);

xxviii. Imeweza kutoa elimu kwa jamii kwa kupitia semina zilizoandaliwa kwa viongozi mbalimbali wa vyombo vya habari na wadau wengine ili kulinda na kutunza maadili yetu;

xxix. Imefanya maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Zanzibar;

xxx. Inakamilisha mswada wa kitabu cha Kiswahili kwa wageni ambao uko katika hatua ya uhariri;

xxxi. Machapisho ya Makamusi ya lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu yanaendelea na yanatarajiwa kutoka mwishoni mwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kamusi la Kipemba liko katika hatua ya mswada;

xxxii. Imesimamia marekebisho ya Katiba za vyama vya michezo ya Watu wenye Ulemavu wa akili, Chama cha Karata Zanzibar (CHAKAZA) na Chama cha Mpira wa Vikapu (BAZA);

xxxiii. Imewapatia wanamichezo mafunzo ya uamuzi wa mchezo wa netiboli yaliyoongozwa na mkufunzi kutoka Afrika Kusini, na ya ualimu wa mpira wa mikono kwa kushirikiana na shirikisho la mchezo huo la Afrika Mashariki na Kati *(ECAHF);*

xxxiv. Imevisaidia kifedha vyama vya michezo ili kumudu kufanikisha kuandaa mashindano, mabonanza na kushiriki mashindano mbali mbali ndani na nje ya nchi. (Angalia kiambatisho Nam. 18);

xxxv. Imekamilisha taratibu zote za uwekaji wa majani bandia katika Uwanja wa Gombani Pemba na kazi za shughuli ya uwekaji inatarajiwa kuanza muda wowote kuanzia sasa wakati kazi ya uchimbuaji imeshaanza;

xxxvi. Imeshakamilisha kazi ya upelekaji umeme wa fezi kubwa kwenye kiwanja cha Gombani na hivi sasa wanasubiriwa wataalamu kutoka nje kuja kuzifunga taa kwenye minara;

xxxvii. Imekamilisha kusimamia matengenezo makubwa ya kiwanja cha Amaan yaliyofanywa kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na serikali imeshakabidhiwa rasmi Uwanja wa Amaan tarehe 19 Mei 2010 na tarehe 19 Juni, 2010 tumezindua rasmi kwa matumizi;

xxxviii. Imeendelea na shughuli za ujenzi wa kituo cha akademia ya Michezo Dole kwa matengenezo ya Uwanja wa kuchezea Michezo ya riadha, mpira wa miguu na michezo midogo midogo;

xxxix. Imechukua hatua za utekelezaji za mpango wa kukuza

vipaji vya wanamichezo chipukizi kwa kutumia wataalamu kutoka nje ya nchi, kutumia vituo vya akademia za ndani vya michezo (akademia) na programu za vyama vya taifa vya michezo;

xl. Imekamilisha ujenzi wa Kituo cha Redio Jamii Micheweni pamoja na uwekaji wa mitambo ya kurushia matangazo na hivi sasa kimeanza shughuli za utangazaji;

xli. Imeyafanyia matengenezo majengo ya kituo cha *EACROTANAL* na kukiweka kituo hicho katika mazingira mazuri;

xlii. Imepatiwa vifaa vya kisasa kama vile *microwave* moja inayotumika kupeleka sauti kutoka Jengo la TVZ, Karume House hadi Masingini na vifaa vya upigaji picha vya digitali;

xliii. Imeweka mtambo mpya wa kisasa wa *MEDIUM WAVE* wa KW50 kwa ajili ya kituo cha STZ; na

xliv. Aidha, kituo hicho kimepatiwa mitambo miwili (2) ya FM ya KW 2 ya dijitali na *tape recorders* za kisasa.

IDARA YA MIPANGO NA SERA

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Idara ya Mipango na Sera ni kuandaa sera na mipango ya maendeleo ya Wizara, kusimamia utekelezaji wake na kusimamia udhibiti wa bajeti ya Wizara. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli zote za sera na mipango ya wizara;

ii Kuendelea kuwapatia nafasi za masomo wafanyakazi wa kike na wa kiume wa wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo na wizara inayohusika na elimu ya juu;

iii Kuendelea kuwasiliana na Washirika wa Maendeleo na taasisi za kimataifa katika kushirikiana ili kufanikisha utekelezaji wa malengo na mipango ya wizara; na

iv Kuendelea kuratibu na kutoa mafunzo ya kupambana na maambukizi mapya ya

Virusi vya Ukimwi kwa wafanyakazi wa wizara wa kike na wa kiume.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango na Sera iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2010/2011, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe sh. 662,305,000/= kwa kazi za kawaida na sh. 500,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA HABARI MAELEZO

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Idara ya Habari Maelezo ni kutoa ufafanuzi wa taarifa za Serikali pamoja na kujenga uhusiano mzuri kati ya Serikali na wananchi; kutayarisha na kutoa vielelezo vya picha, video na majarida yanayohusu shughuli mbali mbali za Serikali; na kusimamia udhibiti na utekelezaji wa Sera ya Habari pamoja na Sheria zinazohusu vyombo vya habari. Katika mwaka wa Fedha wa 2010/2011 Idara hii pamoja na majukumu ya misingi yaliyoelezwa hapo juu, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo;

i. Kuendelea kutoa habari mjini na vijijini kwa kupitia njia ya sinema kwa kuelimisha juu ya maambukizi ya HIV na Ukimwi, jinsia, mazingira, ajira kwa watoto na kupambana na umaskini.
ii. Kuelimisha jamii juu ya uhuru wa vyombo vya habari kwa kutumia sheria iliyopo;
iii. Kuifanyia marekebisho Sheria Nam. 5 ya mwaka 1988 ya Usajili wa Magazeti, Vitabu, na Wakala wa Habari na kuanzisha Sheria mpya ya Uhuru wa vyombo vya habari Zanzibar; na
iv. Kusimamia utendaji wa vyombo vya habari katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 kwa kutengeneza vipindi na makala maalum, kuandaa mikutano ya wanasiasa na vyama vya siasa pamoja na kutoa taarifa maalum kwa wananchi na vyombo vyengine vya habari vya ndani na nje ya nchi .

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Habari Maelezo iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe sh. 249,848,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA TELEVISHENI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Idara ya Televisheni ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha wananchi. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i) Kuwapatia wafanyakazi wa sehemu ya ufundi

elimu ya teknolojia ya dijitali ili kwenda sambamba na vifaa vya teknolojia hiyo vinavyoagizwa hivi sasa;

ii) Kuendelea kutengeneza vipindi vyenye maudhui ya kuelimisha, kupasha habari na kuburudisha jamii pamoja na vipindi vinavyohusu mambo ya uchaguzi;

iii) Kuendeleza na kukuza uwezo wa TVZ katika kutumia teknolojia ya kisasa ya dijitali kwa kununua vifaa vinavyotumia teknolojia hiyo. Ili kukamilisha mpango wake wa matangazo TVZ itajiunga na huduma za *Multi-plus Operator* zinazotolewa na *TBC*. Kwa kujiunga na huduma hizo vipindi vya TVZ vitaweza kuonekana Tanzania nzima muda wa saa 24 kila siku;

iv) Kuwasomesha wafanyakazi kwa ajili ya kuwasiliana na kutoa habari kwa watu wenye ulemavu; na

v) Kuandaa na kurusha hewani vipindi maalum vya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 vitakavyoshirikisha na kuvipa nafasi sawa vyama vyote vya siasa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuiwezesha Idara ya Televisheni kutekeleza malengo iliyojipangia naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya sh. 667,954,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida katika mwaka wa fedha 2010/2011.

IDARA YA SAUTI YA TANZANIA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar ni kuarifu, kuelimisha na kuburudisha wananchi. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

Kuimarisha Ofisi ya Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) kwa kufungua Ofisi Dar es Salaam.

i. Kuendelea kununua vifaa vya kisasa vinavyotumia teknolojia ya dijitali katika kuimarisha matangazo ya STZ;

ii. Kuendeleza kufanya vipindi mbali mbali vya kuelimisha, kupasha habari na kuburudisha jamii; na

iii. Kutoa habari zinazohusu mambo ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar ili iweze kutekeleza majukumu yake iliyojiwekea, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya sh. 545,204,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

IDARA YA UPIGAJI CHAPA

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Idara ya Upigaji Chapa ni kuchapisha nyaraka zote za Serikali, kuchapisha Gazeti Rasmi la Serikali, kuzipatia shajala taasisi zote za Serikali na kuwapatia wananchi huduma za uchapishaji kwa jumla. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara kwa kuwapatia mafunzo ya vitendo;

ii. Kuimarisha utoaji wa huduma za machapisho mbali mbali kwa taasisi za Serikali na wananchi;

iii. Kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa kuzifanyia matengenezo mashine zote za kiwandani ili ziwe katika kiwango kinachoridhisha cha utoaji wa huduma za machapisho; na

iv. Kununua mitambo ambayo itasaidia kuimarisha utoaji wa machapisho yaliyo bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia naliomba baraza lako tukufu kuidhinisha Sh. 627,895,000/= kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Shirika la Magazeti ya Serikali ni kuratibu uchapishwaji wa magazeti ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kuelimisha wananchi katika kukuza uelewa wa mambo mbali mbali ya kilimwengu na kutoa habari zenye kuhamasisha kushiriki katika harakati za maendeleo nchini. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 shirika hili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuongeza ubora na idadi ya magazeti yanayotolewa na Shirika la Magazeti ya Serikali na kupanua maeneo ya usambazaji Unguja, Pemba na Tanzania Bara ili kukuza ushindani wa soko na kuongeza mapato;
ii. Kuimarisha mazingira ya ofisi za Shirika la Magazeti pamoja na wafanyakazi wake;
iii. Kuwaelimisha na kuwapatia wananchi taarifa mbali mbali zinazohusu maendeleo; na
iv. Kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 kwa kutoa elimu, taarifa kupitia uchapishaji wa makala, habari, taarifa maalum, maoni na vikatuni.

Mhe. Mwenyekiti, ili Shirika la Magazeti ya Serikali liweze kutekeleza malengo hayo, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha sh. 245,000,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka 2010/2011.

TUME YA UTANGAZAJI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Tume ya Utangazaji ni kusimamia vyombo vya utangazaji vya Serikali na vya binafsi vinavyoanzishwa humu nchini. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Tume ya Utangazaji imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa kanuni za utangazaji wa dijitali ili kuongoza kasi ya mageuzi ya mfumo wa utangazaji;
ii. Kusimamia majaribio ya urushaji wa matangazo kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya dijitali;
iii. Kuratibu shughuli za utangazaji kwa kuzingatia miongozo ya kufanyika uchaguzi kwa njia ya amani na utulivu; na
iv. Kuendeleza, kuelimisha na kuratibu urushaji wa matangazo kwa kutumia mfumo wa teknolojia ya dijitali hadi kufikia kiwango kinachotegemewa;

Mhe. Mwenyekiti, ili kukamilisha vyema majukumu yake iliyojipangia katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Tume inaliomba Baraza lako Tukufu kuidhinishiwa jumla ya sh. 105,000,000/= kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

CHUO CHA UANDISHI WA HABARI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Chuo cha Uandishi wa Habari ni kufundisha taaluma ya uandishi wa habari kwa ngazi ya Cheti na Diploma. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Chuo kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuanza matayarisho ya ujenzi wa Chuo katika kiwanja chake kilichopo Tunguu;
ii. Kuendelea na usajili wa wanafunzi wapya wa ngazi ya Diploma na Cheti pamoja na kuanzisha programu maalumu za mafunzo ya muda mfupi;
iii. Kuendelea kukuza uhusiano na kukitangaza Chuo kwa taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi;
iv. Kuendelea kukamilisha taratibu za usajili wa Chuo katika Baraza la Taifa la Kuthibitisha Vyuo ya Elimu ya Ufundi Tanzania *(NACTE); na*
v. Kukiimarisha Chuo kwa kuwapatia mafunzo watendaji wake mbali mbali na kuajiri walimu zaidi wa Chuo.

Mhe. Mwenyekiti, ili kukamilisha vyema majukumu yake iliyojipangia katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya sh.120,000,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA UTAMADUNI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Idara ya Utamaduni ni kusimamia, kuratibu, kufufua, kuendeleza na kudumisha utamaduni wa Zanzibar. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kufanya utafiti wa urithi wa utamaduni wa majina ya miji na mitaa ya Zanzibar kwa kutumia taarifa za mchoro wa ramani ya urithi wa Utamaduni zilizokusanywa katika wilaya zote za Zanzibar;

ii. Kuendelea kutekeleza Sera ya Utamaduni Zanzibar kwa kuelimisha jamii kuhusu nini utamaduni wetu kupitia matamasha ya utamaduni, vikundi vya utamaduni, redio, televisheni na vipeperushi na kusimamia utekelezaji wake; na
iii. Kuimarisha utendaji kazi wa nyumba ya sanaa

Mwanakwerekwe.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Utamaduni iweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe sh. 392,115,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

BODI YA SENSA YA FILAMU NA SANAA ZA MAONESHO

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la msingi la Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho ni kukagua sanaa zote za maonesho katika hali zake zote, ili kuhakikisha kuwa haziharibu maadili ya jamii yetu zinapooneshwa hadharani. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Bodi hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuendelea kutoa elimu na miongozo kwa jamii juu ya uandaaji wa sanaa za maonesho na filamu kwa kutumia semina na vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa kutunza na kulinda maadili ya jamii; na
ii. Kuendelea kukagua na kuhakiki kanda za sanaa zinazooneshwa hadharani na kwenye matamasha mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, ili Bodi iweze kukamilisha shughuli zake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe sh. 22,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

BARAZA LA KISWAHILI

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili linaendelea kutekeleza majukumu ya msingi ambayo ni kukuza, kushajiisha na kufuatilia matumizi na maendeleo ya Kiswahili hapa Zanzibar, ndani na nje ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza hili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kukiendeleza Kiswahili kwa kuwashajiisha wasanii wa sanaa za uandishi kushiriki mashindano mbali mbali ya uandishi wa mashairi, tenzi, hadithi na insha;

ii. Kuchapisha Kamusi la Lahaja ya Kipemba;

iii. Kuchapisha kitabu cha Kiswahili kwa wageni; na

iv Kushajiisha na kukuza matumizi ya lugha ya kiswahili fasaha kitaifa na kimataifa kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza la Kiswahili Zanzibar liweze kutekeleza malengo yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe sh. 35,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

BARAZA LA SANAA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Baraza la Sanaa Zanzibar (BASAZA) ni kusimamia na kuratibu maendeleo ya shughuli za sanaa zote Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Baraza la Sanaa limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuifanyia marekebisho Sheria Nam. 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa Zanzibar na kuandaa kanuni zake;
ii. Kushajiisha wasanii na vikundi vya sanaa katika kuendeleza mila, silka na desturi; na
iii. Kutoa mafunzo ya sanaa kwa vijana wenye vipaji maalum vya sanaa.

Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza liweze kutekeleza malengo na majukumu yake ipasavyo, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe sh. 38,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

IDARA YA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Idara ya Michezo ni kusimamia maendeleo ya michezo yote iliyosajiliwa Zanzibar kwa kushirikiana na Baraza la Michezo, vyama vya kitaifa vya michezo, vilabu na wachezaji. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Michezo kwa kuinua viwango vya wanamichezo;

ii. Kuandaa na kushiriki michezo ya kimataifa kwa lengo la kuwapa nafasi wachezaji chipukizi kushiriki vizuri kwenye mashindano ya kitaifa na kimataifa;

iii. Kuibua na kuviendeleza vipaji vya wanamichezo mbali mbali;

iv. Kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Michezo kwa kuinua viwango vya wanamichezo;

v. Kuandaa na kushiriki michezo ya kimataifa kwa lengo la kuwapa nafasi wachezaji chipukizi kushiriki vizuri kwenye mashindano ya kitaifa na kimataifa;

vi. Kuibua na kuviendeleza vipaji vya wanamichezo mbali mbali ili kupata wachezaji walioandaliwa vizuri pamoja na kuwatengenezea mazingira mazuri ya kupata ajira katika michezo;

iv. Kusimamia na kushajiisha kufanyika mashindano ya wizara na mashirika ya Serikali kwa michezo mbali mbali;

v. Kusimamia ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha Akademia ya Michezo Dole;

vi. Kuendeleza maombi ya ujenzi wa viwanja vya michezo ya ndani katika uwanja wa Amani kwa msaada wa Serikali na Jamhuri ya Watu wa China; na

vii. Kuandaa na kushiriki katika mkutano na uongozi wa FIFA kwa ajili ya kudai haki ya Zanzibar kuwa mwanachama wa FIFA.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara iweze kutekeleza shughuli zake za msingi za utawala, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shs. 366,523,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar ni kuvijengea uwezo vyama vya michezo ili viweze kutoa wanamichezo bora wa ridhaa na wa kulipwa. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Baraza hili limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia utekelezaji wa sheria mpya ya Baraza la Michezo ili kukuza michezo Zanzibar na kuandaa kanuni za sheria hiyo;

ii. Kutoa msukumo kwa wanamichezo ili waweze kuandaa mashindano ya kitaifa na kimataifa, matamasha, bonanza za michezo na kushiriki mashindano ya ndani na nje ya nchi;

iii. Kuwapatia wanamichezo mafunzo ya ndani na nje ya nchi yanayohusu utawala, ualimu na uamuzi wa michezo na kutilia mkazo mialiko ya mechi za kujipima nguvu na mechi za kirafiki;

vii. Kusimamia rekebisho ya Katiba na kanuni za vyama vya michezo pamoja na kukamilisha uchaguzi wa viongozi kwa vyama ambavyo muda wa kuongoza umemalizika; n

viii. Kuvisaidia vyama vya michezo kushiriki katika mashindano ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza la Michezo liweze kutekeleza malengo yake, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ruzuku ya Shs. 100,000,000/= kwa kazi za kawaida kwa mwaka 2010/2011.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya msingi ya Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Pemba ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za Wizara Pemba. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Ofisi hii imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwajengea uwezo wafanyakazi ili kila mmoja afanye kazi kwa mujibu wa kada yake;

ii. Kuendelea kuwazindua wafanyakazi juu ya kujikinga na maambukizi mapya ya Ukimwi;

iii. Kukamilisha ujenzi wa uzio wa Kituo cha TVZ Pemba;

iv. Kuvijengea uwezo vyombo vya habari ili vitekeleze majukumu yake kwa ufanisi kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi;

v. Kulifanyia matengenezo jengo la Ofisi Kuu ya Wizara Pemba; na

vi. Kuendelea kukilea kituo cha Redio Jamii Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi Kuu ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Pemba iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, naomba Baraza lako tukufu liidhinishe Shs. 415,156,000/= kwa kazi za kawaida.

KITUO CHA AFRIKA MASHARIKI NA KATI CHA UTAFITI WA SIMULIZI ASILI NA LUGHA ZA AFRIKA (EACROTANAL)

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika na Kituo, yaani Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo Tanzania na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Zanzibar zinaandaa utaratibu wa kituo hicho kutumika kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu inakusudia kubadilisha matumizi ya jengo la EACROTANAL ili liwe ni sehemu muhimu ya Kamisheni ya Kiswahili baada ya kupata ridhaa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, ili Kituo kiweze kutekeleza shughul zake za msingi za utawala. Kwa sasa, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Sh. 15,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

SHUKRANI

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumaliza hutuba yangu naomba kuwashukuru wote waliochangia katika kuitayarisha. Shukrani za pekee na za utiifu mkubwa zimwendee Rais wetu Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume na Mama Shadya Karume binafsi na ZAYADESA kwa kuendelea kutuunga mkono katika shughuli zetu mbali mbali za Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani maalumu zimwendee Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yangu na wasaidizi wao wote kwa kufanya kazi kwa ushirikiano, juhudi, maarifa na uadilifu mkubwa katika kukamilisha mambo yote niliyoyataja hapo awali. Pia nawashukuru Wenyeviti wa Mabaraza na Bodi mbali mbali kwa kusimamia vyema taasisi zao na kunishauri kwa busara na hekima.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuishukuru Kamati yako ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa michango yao mizuri iliyoniwezesha

kuiwasilisha bajeti hii. Michango ya Kamati yako hii wakati wa kupitia baadhi ya taasisi zetu kuona utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu na wakati wa kupitia bajeti hii ndiyo iliyosaidia kuiweka vizuri bajeti ya Wizara yetu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha naomba kuwashukuru wafanyakazi, wanamichezo, wasanii na wamiliki wa vyombo vya habari vya binafsi wote kwa jitihada zao katika kufanikisha maendeleo ya sekta ya habari, utamaduni na michezo nchini. Shukrani za pekee ziwaendee wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa mchango wao katika kufanikisha shughuli za Wizara yetu. Pia kwa namna maalumu natoa shukrani za dhati kwa vyombo vyote vya habari vya umma na vya binafsi kwa michango yao mikubwa wanayoitoa katika kuwashajiisha wananchi katika kutekeleza shughuli za maendeleo. Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikuishukuru Wizara ya Fedha na Uchumi kwa ushirikiano mkubwa iliyotupa kila tulipoikabili kwa mahitaji ya fedha, hasa katika hali ya dharura.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi maalumu, kuwashukuru Mheshimiwa Waziri George Mkuchika, Naibu Waziri Joel Bendera na viongozi mbali mbali wa Idara, Taasisi na Baraza yanayohusika ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Serikali ya Muungano wa Tanzania kwa mashirikiano makubwa yaliyotukuka baina ya wizara zetu mbili zilizobeba majukumu yanayofanana. Mashirikiano yaliyopo yanayohusu sekta za wizara zetu yamechangia kuwepo na ufanisi mkubwa katika kulitumikia Taifa letu. Aidha, kupitia utaratibu wa vikao vyetu vya mashirikiano, wizara zetu mbili za habari, utamaduni na michezo (SMT na SMZ) zimeweza kutatua matatizo mbali mbali yanayozikabili sekta zetu kwa utaratibu ule ule wa maelewano.

Mhe. Mwenyekiti, naomba vilevile nitumie fursa hii kuishukuru kwa namna maalumu Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa misaada yao katika sekta ya habari na michezo. Aidha nazishukuru pia Serikali za Misri, Msumbiji, Iran, Cuba, Uholanzi, India, Ujerumani, Uingereza, Korea ya Kusini na Umarekani kwa mashirikiano yetu na kwa misaada yao ya kitaaluma katika fani ya habari na michezo pia. Vilevile napenda kuyashukuru mashirika ya kimataifa ya UNDP, Ofisi zetu za Ubalozi zilizoko Misri na Oman na Ofisi yetu ya Ubalozi Mdogo ulioko Dubai kwa mashirikiano na misaada waliyotupa katika kufanikisha shughuli za Wizara yetu. Pia, naomba kuzishukuru kampuni za Zantel, Vodacom,

Tigo, Barclays na Jumuiya ya Sheikh Al-Yusouf kwa misaada yao na kutuunga mkono katika kufanikisha mashindano yetu mbali mbali kwenye sekta ya michezo na utamaduni.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani za pekee ziwaendee viongozi wa UNESCO kwa mashirikiano yao na kutuwezesha kujenga Kituo cha Redio Jamii, Micheweni Pemba, kwa kutupatia mitambo ya kituo hicho pamoja na vifaa katika Chuo cha Uandishi wa Habari kilichoko Shangani Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuliarifu Baraza lako kuwa Kituo cha Redio Jamii Micheweni kimeshafunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na hivi sasa kimeshaanza shughuli za utangazaji. Kituo hiki pamoja na majukumu mengine kitasaidia kutoa elimu ya mbinu za kuondoa umaskini nchini. Huu ni mradi maalumu chini ya UNESCO walioahidi kushirikiana nasi kufanikisha malengo ya kujengwa kituo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, penye mafanikio hapakosi matatizo, wakati wizara yangu inafurahia mafanikio ya timu yetu ya soka ya Zanzibar Heroes ya kupata mshindi wa tatu katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati ya *Challenge Cup* yaliyofanyika Kenya mwaka jana, kwa ujumla, chama cha mchezo wa netiboli CHANETA na CHANEZA, malumbano na mabishano ya muda mrefu kati ya viongozi wa vyama hivi yameathiri uundaji na maandalizi ya timu ya Taifa ya Netiboli ya Tanzania iliyoshiriki katika michezo ya kimataifa yenye sura ya Tanzania na hivyo kupelekea matokeo mabaya kwa timu hiyo. Sisi mawaziri wa pande zote mbili tumedhamiria kwa dhati kabisa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa matatizo yanayovikabili vyama hivi na kwa taarifa ya Baraza hili ni kuwa tuliyataka Mabaraza ya Michezo Tanzania (BTMZ na BMT) yakae pamoja na vyama hivyo ili kujadili matatizo yaliyopo na hatimae kupata suluhisho la kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa vyama hivyo vilikaa pamoja na kufikia makubaliano ya kuendeleza mchezo wa netiboli kwa maelewano katika masuala yote ambayo hapo awali yalileta utatanishi ili kuondosha tafauti zao na kuweka mbele utaifa wa Tanzania katika michezo ya kimataifa. Wizara hizi mbili zinazohusika na michezo zitaendele kuhakikisha kuwa makubaliano yaliyofikiwa yanatekelezwa kwa vitendo na mtendaji yeyote atakayebainika kuvunja makubaliano hayo atachukuliwa hatua muafaka dhidi yake.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na uvumilivu. Aidha natanguliza shukurani zangu kwao kwa michango yao watakayoitoa katika kujadili hutuba hii. Naamini kabisa michango hiyo itaisaidia sana Wizara yangu katika kutekeleza malengo yake ya mwaka wa fedha wa 2010/2011.

JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, sasa naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya Shs. 3,934,000,000/= kwa kazi za kawaida na sh. 500,000,000/= kwa kazi za maendeleo kwa ajili ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2010/2011 (Viambatanisho Namba 19 na 20)

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja**.**

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, shukurani zote tunazitoa kwa Mola muweza, ambaye kwa rehema zake ametuweka hai na uzima hadi siku ya leo. Nimesimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii juu ya mwelekeo wa bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa pongezi zetu za dhati kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kushirikiana bega kwa bega na Kamati kila wanapohitajika kufanya hivyo.

Kamati yetu imeridhishwa mno na utendaji wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kipindi chote cha msimu huu wa miaka miwili na nusu unaomalizika.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi nyengine za dhati kabisa kamati yangu inatoa kwa Mhe. Naibu Waziri Kiongozi ambaye pia ni Waziri wa Habari, Utamaudni na Michezo, kwa kujitokeza kuwa mwanachama wa chama cha Mapinduzi aliyechukua fursa hii ya kugombea nafasi ya Urais wa Zanzíbar. Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wajumbe wenzangu wa kamati yetu hii tunamuombea kheri Mwenyezi Mungu amjaalie aliloliomba alipate kwa ajili ya kuiendeleza nchi yetu hii ya Zanzíbar.

Mhe. Mwenyekiti, ukiliomba lolote jema na mwenzio unamuombea Mwenyezi Mungu ampe, na mimi *Inshaallah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu ampe Urais ili aweze kutuendesha katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, wapokee taji kubwa la shukurani ambalo tunawatunukia leo hii kutokana na kazi kubwa waliyoifanya katika kuihoji, kuishauri na kuipa muongozo unaofaa Wizara ya Habari, Utamaduni na

Michezo na hatimaye kupata mafanikio makubwa ambayo tunayashuhudia leo hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwatambulishe wajumbe wa Baraza lako tukufu wanakamati hao kwa majina kama ifuatavyo:-

Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Mwenyekiti
Mhe. Ame Mati Wadi	-	M/Mwenyekiti
Mhe. Abubakar Khamis Bakary	-	Mjumbe
Mhe. Ali Haji Ali	-	Mjumbe
Mhe. Ali Mzee Ali	-	Mjumbe
Mhe. Haji Faki Shaalí	-	Mjumbe
Mhe. Hasnuu Moh'd Hají	-	Mjumbe
Mhe. Moh'd Ali Salim	-	Mjumbe
Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak	-	Mjumbe
Mhe. Raya Suleiman Hamad	-	Mjumbe
Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
Ndg. Salmin Amour Abdalla	-	Katibu
Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo imekadiriwa kupatiwa jumla ya shilingi 4,434,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Waheshimiwa Wajumbe, kiwango hichi ni punguzo la 25% kutoka katika bajeti ya mwaka uliopita.

Ni mafanikio makubwa ya kujivunia kwa Wizara kuweza kupunguza matumizi yake kama ilivyofanya Wizara hii. Kutokana na kukamilisha ujenzi wa miundombinu mikubwa ya habari na michezo katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea na majukumu yake ya kawaida kwa mwaka huu na hii ndiyo hasa sababu ya kupungua kwa makadirio ya matumizi yake kwa mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani za pekee tunazitoa kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kukamilisha ujenzi wa kituo cha kurushia matangazo cha redio jamii huko Micheweni-Pemba, chini ya udhamini washirika la Kimataifa la UNESCO. Kituo hicho kitawapa fursa zaidi wananchi wa Zanzibar kupata taarifa muhimu za ndani na nje ya nchi.

Aidha, Wizara inastahili pongezi kwa ujenzi wa Afisi kuu huko Migombani mjini Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wizara itaendelea na juhudi zake za kuimarisha vyombo vya habari nchini, hasa vile vilivyopo chini ya usimamizi wake. Kasma maalumu imetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya *digital* vya televisheni

na redio. Mafunzo kwa watendaji wa kada hizo yanaandaliwa ili kuwaweka tayari kukabiliana na mfumo huo mpya na wa kisasa unaotarajiwa kuanza rasmi hapa Zanzibar mnamo mwaka 2013.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa hilo, Idara ya Televisheni imepatiwa jumla ya yuro 427,834 kwa ajili ya ununuzi wa mtambo mpya wa wa kurushia matangazo wa dijitali wa KW 5 pamoja na ununuzi wa vipuri vya mtambo wa Pemba. Kutokana na tatizo la upungufu mkubwa wa vifaa vya *Digital* vya kupigia picha, Televisen Zanzíbar imenunua vifaa hivyo vyenye thamani ya $114,155.7 mwishoni mwa mwaka 2009 na tayari vimeanza kutumika. Idara hii pia imeshirikiana na taasisi kadhaa za Serikali na za vatu binafsi katika kutayarisha vipindi mbalimbali vya Elimu.

Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzíbar imenunua mitambo miwili ya FM ya KW 2 kwa kila mmoja inayotumia teknolojia ya *digital*. Idara pia imenunua mtambo wa KW 50 wa Medium Wave na tape recorder ya kisasa ya digitali. Idara hii itaimarishwa zaidi katika mwaka wa fedha 2010/2011 kwa kufungua afisi yake huko Dar-es-Salaam.

Mhe. Mwenyekiti, hatua nyengine muhimu ambayo imechukuliwa na Wizara kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011 ni kukiimarisha chuo cha uandishi wa habarí cha Zanzíbar kwa kufanya matayarisho ya ujenzi wa jengo lake huko Tunguu. Ili kutoa mafunzo yanayohitajika kwa wakati huu, chuo kimenunua samani na vifaa mbale mbali vya kufundishia. Chuo hicho kinatarajia kuajiri walimu wa kudumu wenye kiwango kinachokubalika kusomesha diploma na kukamisha hatua zinazofuata za usajili wake kwenye *NACTE*.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Uandishi wa Habari cha Zanzíbar kina mahusiano mazuri na kinatambuliwa na mashirika Mbale mbali ya ndani na nje ya nchi kama *UNESCO*, na hivyo kukipa hadhi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, tunamshukuru Mhe.Rais wa Zanzibar Dk. Amani Abeid Krume kwa kumteuwa Dk. Ali Mwinyikai kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Magazeti ya Serikali. Uteuzi huo, ambao umefanywa kwa mujibu wa Sheria Nam. 11(1) ya mwaka 2008, utasaidia sana kutatua matatizo yanayoyakumba magazeti ya serikali kwa kuondoa urasimu katika uendeshaji wake na hivyo kuharakisha maendeleo ya sekta ya habari.

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la magazeti ya Serikali linaendelea na juhudi zake za kuliboresha gazeti lake la Zanzíbar leo na kwa kuanzia gazeti hili limeanza kuchapwa la rangi kila ifikapo Ijumaa. Lengo la Shirika kwa mwaka huu wa fedha (2010/2011) ni kuchapisha gazeti la rangi kwa wiki nzima.

Mhe. Mwenyekiti, katika harakati za uchaguzi mkuu wa mwaka huu, Wizara imejipanga vilivyo kutoa habarí za uchaguzi za ukweli na uhakika ili kuinusuru nchi yetu na machafuko yanayoweza kutokea kutokana na habari zisizokuwa na uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, harakati za kuanzisha magazeti mapya nazo zinaendelea na hivi karibuni Wizara imetoa ruhusa ya muda ya kuanzishwa kwa magazeti ya "Zanzíbar Daima" na "*The Cost News*" ili kuwapa uhuru zaidi wananchi wa kuitumia haki yao ya msingi ya kupata habari. Hata hivyo, magazeti hayo bado hayajaanza kutolewa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia kazi za sanaa nchini, wizara imetoa mafunzo ya umuhimu wa kusajili kazi za sanaa kwa wasanii wa Zanzíbar sambamba na kuwapatia leseni wasanii wa hapa nchini. Vile vile, ushirikiano mwema na mabaraza mbalimbali ya sanaa umeendelezwa na wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, Matengenezo makubwa ya Kituo cha Afrika Mashariki na Kati cha Utafiti wa simulizi asili na lugha za Afrika huko Ecrotanal yamefanywa na wizara, kwa kushirikiana na Wizara nyengine zinazohusika kama Wizara ya Mambo ya nje. Kituo hicho kinatarajiwa kuwa Makao makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inato pongezi kwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa kukamilisha matengenezo makubwa ya uwanja wa Amaan katika mwaka 2009/2010. Kazi kubwa iliyobakia ni utunzaji wa uwanja huo pamoja na uendeshaji mzuri utakaopelekea kupatikana faida kwa ajili ya matengenezo madogo madogo kila yanapohitajika.

Waheshimiwa tupokee taarifa ya kwamba muda wowote kuanzia mwezi huu wa Juni ambao unamalizika leo, mwaka huu, nyasi za bandia zitawasili nchini kwa ajili ya kuwekwa kwenye uwanja wa Gombani-Pemba, kwani hatua zote za matayarisho zimekamilika. Uwanja huu utakuwa ni kivutio kikubwa kwa wachezaji na wapenzi wa michezo nchini kwani utakua ni uwanja wa mwanzo wenye nyasi bandia kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, vipaji vya wanamichezo wetu vitaendelezwa zaidi katika mwaka huu wa fedha kupitia uanzishwaji wa Academia ya michezo ambayo ujenzi wake unaendelea huko Dole. Wanamichezo chipukizi watalelewa na kuendelezwa vipaji vyao ili hatimaye Zanzibar ipate wawakilishi wazuri wa michezo ya ndani na nje ya nchi.

Pamoja na mwanzo mzuri waliouonesha, vijana wa *Zanzibar Heroes* wataendelea kupelekwa nchini Misri ili kujifunza na kupata uzoefu zaidi. Kwa

vile mwaka wa fedha 2009/2010 vijana hawa walipata ushindi wa tatu katika mashindano ya *challenge*, Wizara imeweka lengo kwa msimu ujao kuibuka na ushindi wa mwanzo katika mashindano yajayo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza wizara kwa kukamilisha marekebisho ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 1997 ya Tume ya Utangazaji Ambayo ililetwa mbele ya Baraza lako kwa kujadiliwa na hatimaye kupitishwa na Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, wizara, kupitia kitengo cha Idara ya Upigaji Chapa inaendelea kutoa huduma za machapisho kwa Taasisi za Serikali ikiwemo vitabu vya Bajeti, vyeti vya kuzaliwa, fomu za uhaulishaji ardhi, *estimate books* za Wizara ya Fedha na Uchumi, mafaili ya mahakama kuu na risiti mbali mbali. Kazi hii muhimu inatekelezwa na wizara hii ili kuhakikisha shughuli za serikali zinaendelea vyema.
Mhe. Spika, mashine mbali mbali za kiwanda cha upigaji chapa zimefanyiwa matengenezo ili kuweza kuchapa mitihani ya Taifa ya kidato cha pili na ya darasa la saba. Hatua hii imesaidia kupunguza gharama za uchapishaji kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, utafiti wa urithi wa utamaduni katika Wilaya zote za Unguja na Pemba unaendelea. Kwa awamu ya kwanza, mchoro wa ramani ya utamaduni wa Mkoa wa Kaskazini na Kusini Unguja na Pemba umekamilika.

Idara ya utamaduni inaendelea na uratibu wa tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari na hadi sasa tamasha la mwaka huu (2010) tayari limesha fanyika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Maoni hayo ya Kamati, nawaomba wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu, wakubali na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya shilingi za Kitanzania bilioni 4,434,000,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3,934,000,000/= ni kwa kazi za kawaida na shilingi 500,000,000 /= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya mwaka 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijawasilisha kwa ruhusa yako naomba nichangie kidogo kwa kuwa wananchi wangu wananisikiliza katika Jimbo langu la Kwahani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusoma hotuba hii ya kamati, nachukua fursa hii kama Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia kwenye Jimbo langu la Kwahani kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri Kiongozi. Pia kumpongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini Bemba na wengine wote, kwa kazi nzuri ambayo wameionesha naamini katika Baraza lako hili kwa mara hii, Mhe. Waziri hasa tukizingatia kwamba ana mchakato mkubwa huko mbele hatopata shida kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nachukua fursa hii kuwapongeza vijana wetu wa Kopa Coka Cola ambao wanaendelea na mashindano Tanzania Bara kwa timu zetu za Zanzíbar. Timu ya Mkoa wa Mjini Magharibi na timu ya Mkoa wa Kusini Unguja kuingia robo fainali. Nazipongeza kwa dhati timu hizo na ninamuomba Mwenyezi Mungu azijaalie timu hizo ziingie fainali. Kwa sababu *Astaghfiruh* Mhe. Mwenyekiti, nitasema neno moja nachukulia kama masihara, lakini nasema *Astaghfiruh*.

Mhe. Mwenyekiti, kuna safari moja ziliingia timu hizo katika mashindano ya Afrika ya Mashariki timu za Kenya. Zilipoingia mtangazaji Lenard Mambo Mbotela nakumbuka wakati huo, nilikuwa namfuatilia sana, alisema "leo Mungu akitaka asitake kombe linabakia Kenya" na ilikuwa hivyo. Kwa hivyo, mimi nachukulia kama Mwenyezi Mungu atatujaalia timu hizi zikiingia zote za Zanzíbar basi kombe hilo linakuja Zanzíbar ni fahari yetu. Kwa hvyo, tuwaombee dua vijana wetu hawa Mwenyezi Mungu awape nguvu ili hekima ziwe kubwa zaidi na ushindi uje hapa kwa manufaa ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuliko hilo tunatoa pongezi kwa Zantel. Zantel kwa mara hii wameionesha nchi yetu kuiweka katika nuru ya maendeleo. Wameweka *screen* kama nne au tano kubwa katika maeneo tofauti. Eneo moja ni viwanja vya Malindi, usiku ukipita pale unawaona watu wanatazama kombe la dunia. Lakini Chumbuni, Makunduchi na Gombani Pemba. Kwa hivyo, huu ni mwanga mzuri wa kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata kuangalia mambo ya maendeleo. Kwa sababu tukiangalia sasa hivi ajira ya soka na michezo mingine ni ajira binafsi lakini na taifa linafaidika. Kwa hivyo, naiomba sana wizara ikawapa nguvu vijana wetu hawa kuhakikisha kwamba wanaendelea katika shughuli zao za kila siku ili kuona mambo yanaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ni zuri napenda nimpongeze Mhe. Waziri, safari hii nampongeza kwa mara ya kwanza. Mhe. Waziri katika kelele zetu za kamati yetu hii tuliyokuwa nayo na wajumbe wengi katika Baraza hili, tulikuwa tunapiga kelele sana kuhusu vijana wetu wanaosimama mbele ya televisheni na hata waandishi wa habari wa vyombo vya habari kwamba safari hii wanang'ara tena sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri isiwe mwisho, najua yameanza zamani, lakini tunaomba waendelee siku hadi siku. Wanapoingia hapa Barazani na kwenye shughuli yoyote kwengine basi wajulikane kweli Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Zanzíbar iko imara na wale wakiingia popote Mhe. Mwenyekiti wanapata soko. Kwa hivyo, tunasema ajira yoyote imo mikononi mwetu kumng'arisha mtu.

Mhe. Mwenyekiti, kama timu za mpira zinaingia ndani ya uwanja. Mimi timu yangu ya *Mrembo Sport Club* zamani, lakini kama nilikuwa nacheza na Simba

au na Yanga. Kama watavaa jezi nzuri ile timu yangu basi wale wapinzani wanakuwa na wasi wasi. Kwa hivyo, watangazaji au waandishi wetu wa habari wakiwa katika mwelekeo mzuri wanafurahi na wanafanyakazi vizuri zaidi, nawapongeza na ninawaombeni vijana wetu muongeze bidii na mafao mengine yatakuja kwa sababu wizara hii najua Mhe. Waziri yuko makini katika kuharakisha hayo.

Mhe. Mwenyekiti, najua muda unakwenda lakini kuna moja tu ambalo nitasema ni la mwisho, kwa ruhusa yako naomba unikubalie. Mhe. Mwenyekiti, katika vyombo vyetu vya habari, habari ni sehemu moja ya changamoto kwa chombo cha habari chochote. Redio Zanzíbar zamani ilikuwa ina vipengele vingi, kuna baada ya taarifa ya habari, kuna mawio, kuna matangazo ya vifo, matangazo ya biashara na matangazo maalum mengine yote yanayotokea. Kwa hivyo, naipongeza sana wizara kwa hayo.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi wanapenda kuisikiliza Sauti ya Tanzania Zanzibar sasa hivi kwenye kipindi cha kutoka magazetini na kibonzo. Mhe. Mwenyekiti, ndugu yetu Al Haji Juma Mmanga na ndugu yetu Farida Abdalla hawa wamekuwa ni chachu ya maendeleo na changamoto katika kuwasikiliza ukitaka usitake. Kwa sababu baada ya matangazo yote wanakuletea habari za kitaifa za nje, wanakuletea michezo, lakini mwisho wanakufurahisha kuna kibonzo. Sasa hiki kibonzo kinakuletea sura maalum ya kama vichekezo, lakini zina maana nyengine. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza sana ndugu zetu hawa Al Haji Juma Mmanga na ndugu Farida Abdalla kwa kutuletea hamasa katika redio yetu na kuipa pambo zuri na asubuhi ukitaka kibonzo kinakuletea sura maalum kama vichekesho, lakini kinakuwa na maana.

Kwa hivyo, nawapongeza sana ndugu zetu hawa *Alhajj* Juma Mmanga na Farida Abdalla kwa kutuletea kipindi maalum cha Dondoo za Magazeti, wakati wa asubuhi katika redio yetu ya Sauti ya Tanzania Zanzibar, kwa kweli wakati wa kipindi hicho utasikiliza na utakapoondoka umefurahi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa baada ya hayo machache, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii pamoja na wananchi wa Jimbo la Kwahani, naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Nakushukuru ahsante sana.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Najma Khalfan Juma (Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuanza

kwa kumshukuru *Allah* muumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa rehma na huruma zake. Vile vile sisi waja wake kwa kutujaalia mpaka wakati huu tukawa hai na uzima na afya, kutuwezesha leo tukawa katika Baraza hili Tukufu la wananchi wa Zanzibar, ili kuwatumikia kama walivyotutuma kwa maslahi muhimu ya nchi yao. Pia namtakia rehema na amani Mtume wetu Muhammad (*SAW*).

Mhe. Mwenyekiti, sitofanya jambo la maana ikiwa sikumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajaalia uono wa mbali viongozi wetu Mhe. Amani Abeid Karume Rais wa Zanzibar na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kuweka maslahi ya Zanzibar, Wanzanzibari na vizazi vyao.

Kutokana na maamuzi ya kijasiri, kishujaa na upendo wao mkubwa kwa kutokujali maslahi binafsi, kuwaleta Waazanzibari wakawa wamoja tena na kusahau yaliyo pita kwa ujenzi wa Zanzibar mpya. Pamoja na hayo, kuleta maridhiano yatakayoleta mwanga mpya wa maendeleo endelevu kwa Zanzibar yenye matumaini mapya, salama, amani, utulivu kufanyakazi kwa ujenzi wa nchi kwanza na uvivu mwiko.

SAUTI YA TANZANIA ZANZIBAR.

Mhe. Mwenyekiti, chombo hiki ndio mdomo, sikio na sauti ya wananchi na serikali. Jambo la kusikitisha ni kwamba chombo hiki kimegeuzwa "mchumi mndu" (panga), kwani mkulima akitaka kulima hukitafuta kwa kazi ya kukata visiki akimaliza huweka kipembeni pa mlango hauna haja tena, ila lawama pale utakapopita ukimparaza mkulima, huambia mndu wee unataka kunikata mguu. Kwa kweli kazi yake yote husahauliwa mpaka ukiwa na haja tena ndio huchukuliwa ukisifiwa na kutiwa makali kwa kazi ya kulisafisha shamba.

Mhe. Mwenyekiti, suala la maslahi ya vitendea kazi na ya maisha nimeyasema kwa muda wote wa miaka mitano ya kuwepo kwangu nikiwa Waziri kivuli wa Wizara hii, nayasema sio kibubusa, isipokuwa nasema kwa kuyajuwa na kuyaelewa. Lakini yamekuwa donda ndugu halitibiki hufanya gaga siku mbili tatu kwa kuzibwa macho kwa kupewa posho kama *overtime*, fedha za likizo wafanyakazi wawili watatu, yaani wachache ikisha hufa kabisa mambo haya hadi lini?

Mhe. Mwenyekiti, huko Pemba hakusemwi ikiwa kilemba kimerowa itakuwa mkuti (shuka inayovaliawa na wanaume kuanzia sehemu ya kiunoni). Kwa kweli wafanyakazi wa vyombo vya habari huko Pemba zaidi ya mshahara hawana chengine, hawana posho hata wanapofanyakazi siku za Sikukuu, wala Jumamosi na Jumapili tofauti na wizara nyengine, ambazo sina haja ya kuzitaja ambao wanapata posho ndani ya mishahara yao. Wenzangu mie wafanyakazi wa vyombo vya habari kazi zao ni rahisi na nyepesi kiasi gani, hata ikawa

hawastahiki kupata posho lolote zaidi ya mshahara wao tu?

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wa vyombo vya habari wao wanawasemea na kuwasifu watu wengine, lakini wao hawaonekani kwamba wanafanyakazi ngumu na zenye mazingira ya hatari "hawaonekani wala hawakumbukwi" wanageuzwa mshumaa wawaka wateketea kufurahisha umati.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wa vyombo hivi waonewe huruma, kazi zao ngumu kama askari wa mstari wa mbele kwenye vita, wanaonekane kimaslahi wasiwe mchumi mndu.

Mhe. Mwenyekiti, maslahi ya vitendea kazi nayo pia ni shida kwa watenda kazi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar. Kwa mfano, Chumba cha Habari (*News Room*) kimekaa kipindi cha zaidi ya mwaka hakuna *Internet*, nasikia imerudi hivi karibuni, huu sio utaratibu mzuri wa dunia ya leo ya utandawazi, dunia ni kijiji hali irekebishwe ili isitokee tena.

Mhe. Mwenyekiti, Chumba cha Habari ni lazima kuwa na redio, hiyo iliopo hivi sasa ukiiona utaonea huruma, spana mkononi na kaseti za kurekodia zinatolewa kama dawa kali za hospiotali moja kwa kipindi kirefu mpaka imalizike kabisa ndio itolewe nyengine. Kwa kweli kazi za *News Room* ni za kila siku jamani tusiwatie tabu wafanyakazi pasi na sababu za msingi, ukitaka uzuri sharti uzurike hii ni Radio ya Taifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, dunia ya leo kila kitu kinafanywa kibiashara, *computer* ni kitendea kazi muhimu katika ulimwengu wa leo, lakini ikiwepo sio tena ndio ibakie kama jiwe kwamba haihitaji huduma hilo jiwe nalo likipakwa chokaa hupendeza.

Sasa Sauti ya Tanzania Zanzibar, ambapo kuna *computer* kwa matumizi yao inashindwa kununua *Program* ya *Anti Virus*, ili kuziweka *computer* katika utaratibu mzuri wa kufanya kazi za Studio na vipindi. Hata hivyo, ikielewa kuwa kampuni zenye utaalamu wa *Anti Virus* zipo, mbona mawizara mengine yanayojali huajiri kampuni hizo Sauti ya Tanzania Zanzibar kulikoni huko?

Mhe. Mwenyekiti, wazee wetu wametulea katika mazingira mazuri ya kusema kweli japo chungu, kwani mambo ukiyawacha bila ya kusema yatazidi kuharibika. Pemba Sauti ya Tanzania Zanzibar, vitendea kazi navyo ni kilio, watenda kazi mbali ya maslahi madogo wanayopata, lakini vifaa vya kazi ni vichache vimeshachakaa, mfano *mixer* ni moja na iko hali mbaya, kwani wakati mwengine mpaka ipigwe makofi ndio ifanye kazi, *microphone wire*, *microphone* zenyewe na *table stand* hakuna.

Studio ni moja tuu. *Transmission studio* na *production studio* ni hiyo hiyo. Je, kutokana na maendeleo ya Pemba muda wa matangazo ukiongezwa mambo yatakuwaje haja itakuwa haikidhi.

Mhe. Mwenyekiti, usafiri kwa ajili ya kazi za kutafuta habari na vipindi vijijini hazisikiki kwa ukosefu wa usafiri wa uhakika wa ufuatiliaji wa habari hizo. Wakati mwengine kituo cha kurushia matangazo ya FM kilichopo Mkanjuni hushindwa kurusha matangazo yake, kutokana na kushindwa kutiliwa pesa za kununulia *unit* za umeme, tunangoja mpaka *Radio BBC* walipe pesa ndio na sisi tupate matangazo ya FM yasikike huku tukielewa kuwa STZ Pemba haisikiki vizuri kupitia MW, hivyo wananchi wa Pemba wanaomba FM isikae kama kipindi kilichopita.

Mhe. Mwenyekiti, watangazaji katika kituo cha kurushia matangazo cha Pemba ni watatu, ambao hulazimika kuzalisha vipindi 13 kwa wiki, jambo ambalo hupelekea kufanya kazi bila mapunziko hadi siku za sikukuu za kitaifa na hakuna posho wanalopata. Mara nyingi kituo hubaki na mtangazaji mmoja iwapo kwa bahati mmoja akenda masomoni, mwengine likizo ya kawaida, anaebakia huzongwa na utendaji wa kazi kwa kutokuepo na wazalishaji wa vipindi. Idara ifikirie kuongeza wafanyakazi wenye sifa na uwezo.
Mhe. Mwenyekiti, Sauti ya Tanzania Zanzibar ilikuwa na utaratibu mzuri wa kusoma taarifa ya habari kwa Lugha ya Kiingereza kuanzia saa tatu usiku sasa ni zaidi ya mwaka habari kwa lugha hiyo haisikiki nafasi yake wakati mwengine unapigwa muziki, haya basi *internet* hivi karibuni ishalipiwa madeni yake ile kazi nzuri na ianze tena isiwe mgema akisifiwa tembo hulitia maji.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina mila na desturi zake katika kila jambo. Kivazi kina haiba ya kumueleza yule ni nani, leo inasikitisha na kushangaza mtangazaji wa kike anarejeshwa kwa sababu hakuvaa fulana za STZ wakati wa *O.B* (matangazo ya moja kwa moja ya nje), ikumbukwe kuwa mtangazaji akiwa nje ya studio kwa kazi huona fakhari kuvaa vizuri, ili kuonesha taswira yake na kazi yake, wasilazimishwe kuvaa fulana waachiwe wapendeze kulingana na mila zetu. Ingawa hawapatiwi maposho ya kivazi lakini hawajisikii kulazimishwa kuvaa vifulana katika hafla za kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Sauti ya Tanzania Zanzibar inatarajia kufunga mtambo wake wa kurushia matangazo wa Masafa ya Kati (MW) huko kwenye Kituo chake cha Chumbuni wa *kilowatts* 50. Ni jambo la faraji kwa wafanyakazi na wananchi hasa wa Pemba sasa radio yao wataisikia tena vizuri baada ya kilio cha muda mrefu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mtambo mpya utakuwa na nguvu mpya, je Sauti ya Tanzania Zanzibar inayo matayarisho ya ziada juu ya kuutumia mtambo kama

itakiwavyo, kwani huwenda vipindi vikaongezeka, mtambo mpya mambo yawe mapya usije ukatumika kwa vipindi vya ngoma pekee. Kwa kweli wananchi wanayo mengi ya mambo ya maendeleo vijijini na mijini, ujenzi mpya wa nchi, mambo yanayofanywa na serikali kwa maslahi ya wananchi wake yanataka yasikike. Hivyo uongozi wa radio ujirekebishe uendane na wakati wa sasa wa maendeleo ya haraka ya nchi.

IDARA YA TELEVISHENI

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ni muhimu mno, kwani ndipo panapoonekana kwa macho na kusikia kwa sauti yale yote yatokeayo ndani na nje ya nchi. Lakini inasikitisha na inaudhi kubaki na jina kwamba Zanzibar ni ya mwanzo kuwa na Televisheni na kuwa wa kwanza kuwa na televisheni ya rangi Kusini mwa Jangwa la Sahara. Wakati chombo hiki kinaachwa kuporomoka kwa kutokuwa na uwezo wa kuonesha vipindi bora, huku zikishindwa na televisheni zilizoanzishwa miaka ya karibuni. Wafanyakazi mahiri wapo lakini wanabinywa kivifaa na kimaslahi.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Pemba kwa muda mrefu wameyakosa matangazo ya televisheni yao, ambapo wanaoona televisheni mbali mbali wale tu ni wenye uwezo wa kuwa na madishi au waliojiunga na *Cable*.

Lakini waliowengi wamebaki na masanduku ya TV huku yakiliwa na mende kisa *amplifier* imekataa kwa upande wa sauti, picha inafika mpaka kwenye kituo Mkanjuni lakini haiwezekani kurusha picha isiyokuwa na sauti itakuwa Senema Bubu. Kwa upande wa kifaa kilichoharibika inasema kama hakitengenezeki mpaka kirejeshwe Ujarumani na kujitayarisha na mtambo mpya wa *UHF* badala ya mtambo wa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, idara imeshakamilisha mpango wa kununua antenna mpya, lakini haijawa suluhisho kwani *transmitter* iliyopo itashindwa kurusha matangazo, iwapo vifaa vilivyoharibika havitopelekwa nje kwa matengenezo, ili kukidhi haja ya kuingia katika matangazo ya *digital* moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, kilio cha usafiri bado kipo pale pale kwa vituo vyote Unguja na Pemba. Unguja idara ina gari moja tuu kwa huduma zote, Pemba gari ni mkweche au tuseme haina gari hii ni hatari kubwa sana. Kwa kweli ni vyema kueleweka pale pana *transmitter* inawezekana kwa bahati mbaya mtu akapigwa na umeme hapa gari ya kumkimbiza hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, limeshatokea hapo nyuma ambapo mfanyakazi mmoja, alipigwa na '*High Tension*" na kupoteza fahamu, ilibidi wenziwe wamkongoje hadi barabarani na kuomba msaada wa gari kwa wasamaria wema hiyo ni

hatari. Tatizo jengine kwa wafanyakazi wa kituo baada ya *transmission* kwa mujibu ya *shift* ya mtu hulazimika mfanyakazi ajipange namna atavyoondoka hata inyeshe mvua ya kilimiya (mvua kubwa sana), basi utajijuwa mwenyewe namna utafika kwako.

Mhe. Mwenyekiti, maslahi ya mishahara bado inapigiwa kelele na wafanyakazi wa televisheni kwamba bado ni midogo na hadithi ya *Scheme of Service* ni Wimbo wa Taifa. Posho ya nyumba na usafiri ni dogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, jambo lisiloonekana na idara ni kuwaachiya majukumu makubwa wazoefu, lakini kimaslahi wana pata mashahara mdogo, ukilinganisha na vijana wetu wasomi wana mishahara mikubwa, hatugombi wasomi tunawahitaji sana, lakini na hawa wazoefu ambao wana dhamana kubwa kama vile Mhariri Mkuu, Mkuu wa Mtambo wa masingini na wengineo hawathaminiwi uzoefu wao na majukumu yao.

Hivyo ni vyema wenye elimu wanapopewa mishahara mikubwa wapewe na majukumu makubwa badala ya kuachiwa wazoefu majukumu makubwa na mshahara mdogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, madai ya fedha ni mengi mno mwaka huu, kwani wafanyakazi wanaona hawasikilizwi wanaposema katika Idara zao hasa Televisheni na Sauti ya Tanzania Zanzibar. Marupupu ya safari za likizo, pamoja na za masomo zinafikia 15,000,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, mcheza kwao hutunzwa, Idara ya Televisheni haina utamaduni ya kuwaaga wafanyakazi wake pale wanapostaafu baada ya kuitumikia idara kwa muda wao wote. Lakini idara iko mbele kuwatangazia maidara mengine namna wanavyowaenzi wastaafu.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya hayo kila ifikapo Tarehe Mosi Mei huwa ni Siku ya Wafanyakazi Duniani na wafanyakazi wa Zanzibar nao hushiriki kupitia idara zao huteuwa wafanyakazi bora. Lakini inashangaza kwa Idara ya Televisheni inashindwa kumzawadia mfanyakazi bora hata penseli kwa mwaka, wakati wao ndio watangazaji wakubwa kwa wafanyakazi wanaopata zawadi za *May Day* wao wanageuka Ngariba wa Kilwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, afya ya wafanyakazi ni jambo muhimu, walielezwa kwamba kuna utaratibu wa kila mwezi wa kufanyiwa *Medical Checking*, wafanyakazi wa televisheni hawajui mfanyakazi yupi aliyefanyiwa hiyo *checking*, posho ya maziwa kwa ajili ya wafanyakazi wanaoathirika na mionzi idara ilitoa ahadi lakini haijatimizwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ya Televisheni kuna utaratibu wa baadhi ya miezi wafanyakazi wanaoshughulika na minara hupanda, kwa ajili ya kazi zao na hulipwa posho ya kazi hiyo. Idara imesahau kabisa posho ya kazi iyo ngumu na ya hatari.

Mhe. Mwenyekiti, hapo kale palikuwa na utaratibu kwa wafanyakazi wanaofuatana na viongozi kwa ziara za mashamba wakigaiwa posho, ili ziweze kuwasaidia kwa chakula cha mchana au japo wanunue chungwa. Sasa mpango huo haupo tena mfanyakazi kageuzwa boga ataponea umande, wakati huo huo pesa za posho la uongozi wa *section* zimeondolewa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi hawana kitu basi na hivyo vijisenti vichache walivyonavyo wanakopwa na hawalipwi. Kwa mfano, wafanyakazi wakitoka Pemba hadi Zanzibar na vifaa vya kazi inabidi kuvilipia kwenye boti, wanalipa lakini baadaye hawarejeshewi pesa zao, madai yako kwa mhasibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mcheza kwao hutunzwa wafanyakazi watunzwe na kusaidiwa kimaslahi, ili wapate moyo wa kujituma zaidi na kwa ufanisi tusiwape ahadi nyingi ambazo hazitekelezeki zinawavunja moyo.

IDARA YA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, michezo ni afya, ajira na kujuana, lakini pia michezo katika dunia ya leo ya utandawazi hasa mpira wa miguu ni ajira kubwa. Hivyo basi ili wanamichezo wanyanyuke wanahitaji matayarisho, ndipo wapate uwezo wa kuingia ndani ya anga za kitaifa na Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, ni furaha iliyoje kuona leo Uwanja wa Amani umekarabatiwa upya unapendeza umerudi tena kwa enzi zake. Naipongeza wizara kwa juhudi zake za kuishughulikia tunu hii tulioachiwa na Mzee wetu Almarhoum Abeid Amani Karume *Allah* aieweke roho yake pema peponi Amin. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini uwanja ulifuatana na hoteli yake, wakati huo ilitumiwa na wanamichezo, wageni na wananchi wa kawaida, hoteli nzuri inapendeza lakini hivi sasa haitamaniki na katika matengenezo ya uwanja hoteli haikuguswa. Ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, kwa wizara, hoteli ile itengenezwe vizuri iendane na uwanja au serikali ikiona ni mzigo basi itowe tenda ya kuikodisha kwa wenye uwezo watakaomudu kuikatarabati na kuindesha kihoteli za kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, uwanja ambao nao inafaa uenziwe kwa uasili wake ni Uwanja wa Mao. Kwa hivyo, kuna haja kubwa kwa wizara kuuweka katika

ratiba yake ya kazi, kwa ajili ya kukarabatiwa upya katika hali ya kisasa, ili uweze kutumiwa hasa ikizingatiwa pale ulipo ni mjini, itakuwa pana kiwanja chengine kizuri kitachokisaidia Kiwanja cha Amani.

Mhe. Mwenyekiti, Pemba nako kuna Kiwanja kizuri kikubwa cha Gombani kiwanja hiki inasemekana hakikumalizika kwa mujibu wa *plan* yake, ilikuwa nayo iwe na viwanja vya ndani vya michezo pia iwe na hoteli, je kuna mpango wowote na juhudi za kuona mambo haya yanapatikana?

Lakini la karibu na jepesi tulisikia wakati fulani kwamba Uwanja wa Gombani utawekewa majani bandia kwa bahati nzuri nimemsikia Mwenyekiti kwamba yako njiani, nadhani Uwanja wa gombani nao utapata hii nafasi ya kuekewa hayo majani ya bandia. Vile vile Idara ya Michezo iko mbioni kuona wanakamilisha utaratibu wa kuuwekea Uwanja wa Gombani taa hasa kwa vile sasa kuna umeme wa uhakika Pemba utakaowezesha michezo ya usiku kufana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wanamichezo wa Zanzibar wanavyo vipaji vikubwa ambavyo vinahitaji kuibuliwa, lakini vilabu vingi uwezo wao ni mdogo hasa vile vya Pemba na vijijini pia na vilabu vidogo vidogo. Kwa kweli hawana fedha za kuweza kuibuwa vipaji vilivyojificha vya kupata na sisi timu ya kuingia katika mpira wa kimataifa miaka 10 au 15 ijayo matayarisho yaanze leo.

Hivyo basi wizara kwa kushirikiana na Idara ya Michezo ilete makocha wa kigeni, ili kuinuwa mchezo wa mpira wa miguu unaopendwa zaidi, tunaelewa kocha wa Misri yupo, lakini hatumiki vizuri apangiwe utaratibu mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, michezo ni kitu kinachokuwa hakibakii hapo hapo na ndio maana Idara ya Michezo hutafuta kila njia kuingia katika njanja za Kimataifa. Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wanapenda kujuwa zile juhudi za kujiunga na Shirika la Kimataifa la Mpira Duniani (*FIFA)* zimeishia wapi au ndio tupo tunatowa macho huku tukiona wengine wanafaidika.

IDARA YA UTAMADUNI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utamaduni ina majukumu ya msingi ya kuhuisha utamaduni wetu, kuukuza, kuuendeleza na hatimaye kuuimarisha ni chombo kikuu katika nchi yetu ambacho kikitumiwa vyema kinaweza kuwa ni chachu ya kuwaletea maendeleo wananchi wetu. Sisi daima tunaamini kwamba utamaduni ndio roho na mhimili wa taifa letu.

Kwa hivyo, hatuna budi kuelekeza nguvu zetu katika kuhakikisha kwamba

sekta hii inapiga hatua, katika kulinda na kudumisha maslahi ya nchi yetu, hatimaye kuwaletea maendeleo wananchi.

Kuna mifano mingi kutoka kwa mataifa mbali mbali ulimwenguni, namna sekta hii ilivyoweza kuchangia pato la taifa, hatimaye kuwa ni moja ya vianzio vikuu vya mapato katika kuendeleza uchumi wa nchi husika. Kutokana na hali hiyo, bila shaka na sisi Wazanzibari tukiwa tumejaaliwa kuwa na urithi bora wa nyanja mbali mbali zinazotokana na utamaduni wetu.

Hivyo, lazima tukubali wimbi la mabadiliko na kuachana kabisa na dhana iliojengeka miongoni mwetu, kuuona utamaduni kuwa ni kioo cha burudani na kusahau dhana nzima ya kutambua kwamba utamduni ni chombo cha maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo, kwa kazi kubwa na nzuri yenye mwelekeo wa kujenga taswira ya maendeleo ya sasa na baadaye katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Tunaamini kwamba kukamilika kwa mchoro wa ramani ya utamaduni unaochambua na kuonesha mtawanyiko wa aina mbali mbali za hazina na tunu za utamaduni wetu, zinazopatikana katika visiwa vyetu viwili ni maendeleo mapya katika kujenga mwelekeo wa maendeleo katika uwanja wa utamaduni wetu.

Imani yangu kwamba hii ni moja ya kazi nzuri ya maendeleo, ambayo kumalizika kwake kunatoa nafasi kwa wasomi, *NGO's*, mashirika na taasisi mbali mbali za ndani na nje pamoja na watafiti kuuendeleza utamaduni wetu. Bila shaka hii ni moja kati ya vianzio vya elimu ambavyo vikitumiwa vyema vitaendelea kuitangaza Zanzibar hususan katika uwanja wa kuendeleza utamaduni wetu.

Lakini tunashauri kwamba kazi iliyoyapembua maeneo mbali mbali ya utamaduni wetu, hii iende sambamba kwa mashirikiano ya karibu zaidi kati ya Wizara ya Biashara na Utalii katika kuhakikisha kwamba wageni na watalii wanaoitembelea Zanzabar wanapata vivutio vipya. Vivutio ambavyo vinavyotokana na utamaduni wetu katika kuzidisha mvuto na kuongeza ushawishi kwa wageni wazidi kuvutika kuitembelea Zanzibar. Kwa upande wa pili vianzio hivi vichukuwe nafasi ya kuwaendeleza wananchi wetu, kujiajiri wenyewe kupitia maeneo yanayotokana na urithi wa utamaduni wao.

Mhe. Mwenyekiti, utamaduni ni kitu kinachokua na kubadilika na kama haukutuzwa na kulelewa ipasavyo, basi tutajikuta utamaduni wetu unapotea. Vifaa vya kutunzia utamaduni wetu, ili uasili wake utakapotoweka kumbukumbu zake ziwepo, vifaa hivyo vipo. Idara ya Utamaduni imenunuwa

vifaa kama vile *still camera* pamoja na *moving camera*, jambo la kusikitisha wafanyakazi wa idara hii hawapewi vifaa hivyo, kuvifanyia kazi na badala yake vimewekwa kama pambo havileti faida inayotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri afanye ziara za makusudi katika maidara zake zote za wizara yake na kuzungumza na wafanyakazi wenyewe, ili kujuwa matatizo yanayowakabili kuliko kuwasikiliza Wakuu wa Maidara peke yao. Mhe. Waziri maidarani kuna mambo na matatizo mengi huko.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie machache kuhusiana na Tamasha letu la Utamaduni, ambalo huadhimishwa kila mwaka hapa Zanzibar. Kweli lazima tukiri kwamba tokea kuanzishwa kwa tamasha letu pale mwaka 1994 sasa yapata miaka kumi na sita (16). Kambi ya Upinzani inashaka kwamba Tamasha hili linaonekana kuandaliwa kwa hofu ya kuiogopa kauli ya viongozi wetu, pale walipotangaza kwamba kila ifikapo tarehe 19 Julai ya kila mwaka iwe ni Siku ya Kuadhimisha Utamaduni wa Mzanzibar.

Mimi mwenyewe ni mmoja kati ya waanzilishi wa tamasha hili chini ya wizara hii, lakini inasikitisha kuona kwamba tamasha hili limepoteza haiba, muelekeo, mvuto na umakini wa maandalizi yake. Tamasha ni shangwe yenye lengo maalum linalowakutanisha wasanii na mabingwa mbali mbali wale wa ndani na wa nje katika uwanja wa utamaduni, kuweza kuchambua na kubadilishana ujuzi, uzoefu, umahiri na fikra mpya katika kuuendeleza utamaduni huo.

Kwa bahati mbaya tamasha letu limepoteza mwelekeo huo na linabakia tamasha la siku ifike tamasha lipite. Kama maandalizi yangekua tayari bila shaka vyombo vyetu angalau vya ndani tunavyovimiliki sisi wenyewe vingekuwa tayari vinarindima na kulieleza tamasha hilo. Kutokana na hali hiyo, napata wasi wasi kwamba kama kweli angalau tunayo chembe ya uchungu wa kuuimarisha na kuutangaza utamaduni wetu.

Kwa hivyo, ni vyema tukajiuliza tunamsubiri nani aje atusaidiye mawazo ya namna ya kudumisha na kuendeleza utamaduni wetu. Kila kitu kina ujuzi na taaluma yake, kwa nini hatuwapeleki watendaji wetu kuchukua fani za juu katika maeneo ya utamaduni, wakati tulionao sio wa kubahatisha. Kwa maana hiyo, lazima watendaji wawe wabunifu, wavumbuzi, kasi ya utendaji na mipango mkakati inayotekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, nashawishika kuwapongeza *ZIFF* na Sauti ya Busara katika kuitangaza Zanzibar, hatimaye kuwafanya wageni wengi kuitembelea Zanzibar, jambo ambalo linazidisha wigo katika uwanja wa kuendeleza utalii Visiwani Zanzibar.
Lakini mafanikio haya hayakuja kirahisi lakini baada ya kazi nzito ya

kujitangaza ndani na nje ya nchi. Kwa mfano, katika tamasha lililofanyika mwaka jana *ZIFF* taasisi isio ya kiserikali walitumia zaidi ya shilingi 200 milioni kwa ajili ya kuendeshea tamasha hilo.

Hivyo ni kweli tunakaa vikaoni kujigamba na kusimama kifua mbele kwamba tunafanya tamasha kwa kutumia shilingi 16 milioni, wapi na wapi jamani! Au ni kukamilisha tamasha la siku ipite tu. Kwa vile tamasha linahitaji gharama za maandalizi ambazo zinatabia ya kupanda kila mwaka, tunaona kwamba itakua ni wazo zuri na la busara, kama tukigeuza mwelekeo wetu na kuliandaa tamasha hili kila baada ya miaka miwili, kwani hata baadhi ya nchi zenye uchumi mzuri ulimwenguni wana utaratibu kama huo.

Mwelekeo huu utatoa nafasi ya matayarisho bora ikiwa ni pamoja na kutafuta wafadhili wa kibiashara wa ndani na nje, pamoja kutoa mialiko kwa vikundi vya nje ya nchi jambo ambalo halifanyiki kutokana na ukosefu na fedha.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na matatizo yote haya Mhe. Waziri yeye ni mkereketwa wa utamaduni na jinsi anavyoumwa na utamaduni wake. Kwa hivyo, namuomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti achukuwe hatua na juhudi za makusudi zitakazohakikisha maandalizi bora ya tamasha letu yanafanyika na sio ya kuripua ripua.

Tamasha tunaomba litangazwe ipasavyo kupitia vyombo na vianzio mbali mbali vya mashirika ya kibiashara, na utalii ili liweze kuleta faida na tijara iliokusudiwa na Taifa. Tamasha lazima liwe ni mhimili wa kuliingizia taifa letu mapato na sio kuliadhimisha kama sehemu ya kuenzi kumbukumbu tu. Kutokana na hali hiyo, lazima marekebisho yafanywe, ili liweze kutoa changamoto ya kusaidia kuliingizia taifa letu fedha za kigeni, ikiwa ni pamoja na kuwavutia wageni wanaoitembelea nchi yetu.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalize kwa kumshukuru *Allah (SW)*, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu na kutowa maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe Wazanzibari wote wenye nia safi ya kuleta maendeleo na umoja wa kweli, basi tuungane kwa nia moja kuiletea Zanzibar mwanga mpya wa mshikamano wa maridhiano, hivyo tarehe 31 Julai 2010 kwenye Kura ya Maoni waweke Kura ya Ndio, ili kuweka mustakbali mwema kwa vizazi vya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumaliza ninayo masikitiko madogo kwa wizara

yangu ninayoipenda. Mimi ni Waziri Kivuli wa wizara hii na ninaelewa kila Waziri Kivuli hupata kitabu cha hotuba siku mbili kabla nasikitika kwamba mimi kitabu nimekipata jana saa 11:30 na hii sijui niseme ni dhararu kwa sababu mimi ni mwanamke au idara ilisahau ama vipi. Lakini hilo naiachia wizara yenyewe.

Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii ya mwanzo baada ya viongozi wahusika waliopita kuwasilisha hotuba zao.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima kufika hapa na kuweza kushiriki katika shughuli muhimu za taifa letu, lakini pia nikupongeze kwa kupata nafasi hii sambamba na kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake fupi ambayo imeandikika na bila ya shaka wajumbe wameifahamu.

Mhe. Mwenyekiti mimi nianze kumpongeza Mhe. Waziri kwa uamuzi wake wa kidemokrasia kwa kuamua kuchukua fomu kwenye chama chake katika mbio za Urais wa Zanzibar. Demokrasia ni maamuzi na njia pana ya kufikia uamuzi bora. Kwa hivyo hatua ya Mhe. Waziri kuungana na wenzangu kumi na moja kwa kuchukua fomu kwenye chama chake bila ya shaka ni maamuzi ya busara na sasa bila ya shaka Wazanzibar wanasubiri kiongozi wa CCM atakayepambana na yule wa CUF Seif Sharif Hamad.

Mhe. Mwenyekiti nianze kwenye Idara ya Habari Maelezo ambayo kitabu cha Mhe. Waziri kimeeleza kwa upana malengo ya idara hii na lengo la msingi kabisa au majukumu ya msingi kwa idara hii ni kutoa ufafanuzi wa taarifa za serikali, pamoja na kujenga uhusiano wa serikali na wananchi. Mhe. Mwenyekiti ni majukumu ya msingi ambayo kila mtu anahitaji kuyapongeza na kuweza kuunga mkono kwamba ni lazima Idara ijenge uwezo wa hali ya juu wa kutoa ufafanuzi juu ya taarifa ya serikali, lakini pia ijenge mahusiano kati ya serikali na wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti idara mbali ya majukumu yake ya msingi lakini kuna majukumu mengine manne ambayo imejipangia kwenye mwaka huu na kwenye bajeti hii, jukumu namba nne linasema kwamba kusimamia utendaji wa vyombo vya habari katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 kwa kutengeneza vipindi na makala maalum, uchaguzi wa 2010 hauna maana kwamba utaanzia siku ya kura tu au siku ya kampeni lakini mchakato wake unaanza kwenye vyama vya siasa kwa kutafuta wagombea katika ngazi mbali

mbali. Niwapongeze sana vyombo vya habari TV na Redio Zanzibar kwa kutoa taarifa za wagombea wa CCM kwa ngazi ya urais hatua kwa hatua kwa hapa wamefanya wajibu wao.

Lakini kwa upande mwengine wamesahau kwamba TV na Redio ni chombo cha umma walisahau kutoa taarifa kama hizi kwenye mchakato wa kutafuta wagombea kwa upende wa CUF kwa ngazi za uwakilishi, ubunge hadi Urais, sasa demokrasia na wajibu huu uwe kwa taifa usiwe kwa chama fulani, mimi nilipongeze gazeti la Zanzibar leo wao walikuwa wakitoa taarifa hatua kwa hatua kwenye mchakato wa Chama cha CUF majimbo yote ya Unguja na Pemba. Lakini TV na Redio wametoa kwa nafasi ya urais tena kwa upande wa CCM naomba hili Mhe. Waziri alione na hasa kwa sababu hivi vyombo ni vya umma sio vya chama chochote.

Mhe. Mwenyekiti nikitoka hapo niende kwanye Idara ya Televisheni ambao pia wana jukumu la kutoa na kuelimisha na kuhuwisha wananchi, leo saa kumi baada ya taarifa ya habari nilikuwa nikiangalia Televisheni Zanzibar kuna kipindi cha vikatuni nilipoangalia kipindi kile nimejiuliza hapa Televisheni wanaelimisha jamii au wanafundisha jamii mambo ya kijitu kizima, kwa sababu vikatuni vile walikuwa wakicheza mchezo lakini alikuwa anatikisika sehemu ya kiuno tu kama hali ile ndio tunafundisha watoto wetu na ndio wanajifunza basi nadhani TV inafundisha watoto mambo makubwa mapema.

Mhe. Mwenyekiti ningeshauri basi habari zetu hizi za Zanzibar zikachuja sana ipi iwe taaluma ya watu wazima na kwa wakati gani na ipi taaluma ya watoto na kwa wakati gani, lakini vitu vyengine kuonyesha kila mtu ni mafunzo wanayopewa mapema watoto wetu ambayo hatimae madhara yake ni makubwa. Kwa hivyo mimi ushauri wangu ni kwamba waendelee kuelimisha jamii lakini watizame sana ni taaluma gani kwa watu gani na rika gani na wakati gani.
Nikiendelea na mchango wangu niende moja kwa moja kwenye Baraza la Kiswahili kwenye lengo la pili ya mwaka huu ni kuchapisha kamusi la lahaja ya Kipemba, nakumbuka mwaka jana Mhe. Waziri alitwambia wanaandaa makamusi matatu, kamusi la lahaja ya Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi sasa humu kwenye kitabu hiki kuna malengo ya kuchapisha kamusi la Kipemba. Napenda kujua je kamusi la Kimakunduchi na Kitumbatu limemalizika kwa sababu mimi ni Mtumbatu sasa nikiona wenzangu Wapemba wanaandaliwa mimi sijatajwa sijisiki raha kwa hivyo nataka nijue makamusi hayo yamekamilika au limeachwa njiani tumeona lianzie hili la Kipemba.

Mhe. Mwenyekiti jengine kwenye Baraza la Kiswahili ni hili lengo la nne ambalo ni kushajihisha na kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili fasaha kitaifa na kimataifa kupitia vyombo vya habari, bado vyombo vya habari

vinafanya jukumu hili na naomba niwapongeze, lakini kuna lugha nyengine au maneno mengine kidogo yanakuwa magumu kwa mfano kuna baadhi ya watangazaji wa vyombo vya habari hasa binafsi wanapenda sana kutumia neno baradhuli neno hili sio Kiswahili fasaha. Sasa Mzanzibari akisikia awe baradhuli nadhani tumechuja sana ndio tukaona sio Kiswahili fasaha na kwa baadhi ya Wazanzibari hili neno wanalitafsiri vibaya. Kwa hivyo mungewaelimisha kwamba baadhi ya matamshi yao wanayotamka yakienda na tamaduni zetu na utamaduni wetu wa Unguja na Pemba kwa sababu maneno mengine ni matusi kutaja kwenye watu.

Jengine ambalo ningelichangia kwa ufupi ni Idara ya Michezo niwapongeze kwa juhudi zao hasa kwa kuanzisha *Academiy* kule Dole, lakini kwa hapa ningetaka kujua kwa sasa tupo katika hatua gani, kituo hiki kimefikia hatua gani ili tupate kuelewa zaidi. Lakini sambamba na hilo napenda niwapongeze Idara hii au Serikali kwa jumla kwa kutengeneza Uwanja wa Amani katika kiwango cha kisasa, nikiungana na Waziri Kivuli kwamba Uwanja wa Amani pamoja na Hoteli yake bila ya Hoteli uwanja ule utakuwa hauna sura madhubuti.

Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba utueleze nini malengo ya serikali katika kutengeneza hoteli ya Uwanja wa Amani, lakini pia Uwanja wa Amani mipaka yake kwa upande wa Mashariki kulikuwa na majengo ambayo yalipigwa marufuku kujengwa, kwa sababu ni magorofa na yanaweza kusababisha madhara kwenye uwanja wa Aman. Lakini hivi karibuni majengo yale chini yamejengwa maduka ya kisasa mazuri tu ningeomba kujua maduka yale ni Uwanja wa Amani au yameuziwa nani au nani kapewa pale kwa ajili ya kuwekeza maduka yale, kama ya Uwanja wa Amani ni jambo la kupongeza lakini kama sio Uwanja wa Amani basi ni nani aliyepewa eneo lile kuendesha biashara ile.

Mhe. Mwenyekiti nimalizie mchango wangu kabisa ukurasa wa mwisho wa arubaini na nne ambapo Mhe. Waziri ametaka kumuidhinishia kwenye *heading* pale anasema jumla ya gharama za Wizara ya Habari , Utamaduni na Michezo. Ningetaka kujua kwa sababu hii ni Wizara ya Kiswahili hapa ni gharama au matumizi, kwa sababu gharama maana yake kuna biashara ya faida na matumizi maana yake hakuna faida. Sasa hapa umekusudia kusema gharama au matumizi kama gharama ni mwanalugha naomba atusaidie mimi sitoidhinisha gharama kwa sababu hatujafanya biashara, kama matumizi basi niko tayari kuidhinisha.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa niungane na wenzangu kumuombea dua Mhe. Waziri Mungu amjaalie ashinde ili tuwe nae kama Rais wa Zanzibar naunga mkono hoja. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Haji Faki Shaali: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kunipatia nafasi hii mimi sina mchango mkubwa sana, lakini kwanza naomba kutanguliza kwa kusema tu naunga mkono hoja hii kabla sijasahau, pia hatua ya pili niende katika pongezi Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Naibu wake, katibu Mkuu na watendaji wote kwa jukumu kubwa na zito la kusimamia habari Utamaduni na Michezo katika nchi yetu ya Zanzibar.

Lakini pia nitoe pongezi za pekee kwa Naibu Waziri Kiongozi kwa kutumia demokrasia ya Katiba ya Chama chake katika nchi yake kujitokeza katika kinyang'anyiro hiki cha Urais wa Zanzibar, akiwa yeye ni miongoni mwa watu kumi na moja wana timu kamili ya mpira wenzetu ishaalla Mwenyezi Mungu yeye ameshamjua nani atakuwa Rais wa Zanzibar ni imani yangu kwamba atakayepata atashirikiana na watakaokosa, na watakaokosa watampa mashirikiano mazuri yule atakayepata. Aliloandika Mwenyezi Mungu halifutiki.

Mhe. Mwenyekiti pia nataka nianze na pongezi kama nilivyofanya mwaka jama kwa juhudi wanayofanya Wizara hii kuwaendeleza wafanyakazi wao kimasomo, ukiangalia ukurasa wa 48 mpaka ukurasa wa 58 kama utawahisabu wanafikia watu mia kamili ambao wamepata fursa ya kimasomo katika Idara na taasisi mbali mbali zilioko chini ya Wizara hii. Hizo ni pongezi za pekee ambazo lazima mimi niwape kwa sababu ukimwendeleza mfanyakazi ndio unaendeleza Wizara ndio unaendeleza taifa, kwa hivyo pokeeni pongezi zangu za dhati kwa hilo.

Nikiacha hapo sasa nije kwenye kuchangia hasa kuna kitu kidogo kwenye staili za uandishi kidogo kinanibabaisha hasa katika ile *paragraph* ya usomaji wa fedha, maana baada ya maelezo yote waziri mwisho atakuja naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi fulani kwa kazi za kawaida. Sasa ukiangalia wizara hii kuna taasisi nyingi ambazo zinapata ruzuku hawana mafungu hapa, lakini utakuta wanaombewa fedha hapa wana fungu sasa bora ingefichika fichika zile pesa wakati hii ni ruzuku na ingeingia tu moja kwa moja katika maombi ya fungu kubwa halafu wenyewe wakawa wanajuana huko huko. Wao hata wakiwa wanapata *break down* lakini kwa inavyoomba hapa inaonyesha wazi kwamba ni watu ambao wana fungu.

Kwa mfano ukiangalia Shirika la Magazeti ya Serikali hili linapata ruzuku, lakini ukiangalia ibara ya ishirini na sita anasema Mhe. Spika, ili Shirika la Magazeti ya Serikali liweze kutekeleza malengo hayo naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha Shs. 245,000,000 sasa hapa hili utaona ni fungu, kwa ghafla utafikiria hawa wana fungu katika bajeti lakini ukiangalia katika kile kitabu

hiki cha Makadirio ya Mapato hawana fungu lolote hawa wanapata ruzuku kwa Idara ya Mpigaji Chapa. Sasa taasisi zake nyingi ndio zimekuwa zinapata ruzuku lakini vile anavyoziombea pesa kwa ile staili ya uandishi utaona kwamba wana fungu hasa, sasa pengine hili ninavyozungumza mimi sivyo pangine mlivyofanye nyie ndivyo lakini mawazo yangu kwa sababu ndivyo nilivyofikiria ni demokrasia kuyaeleza wala sitoona tabu kuelekezwa vilivyokuwa sahihi.

Lakini hapa hapo Mhe. Mwenyekiti mwanzoni mwanzoni lilipoanzisha hili shirika nilikuwa ni mmoja niliyetetea hata ukiangalia Hansard nilitetea sana kwamba Shirika la Magazeti itabidi tulilee, nakumbuka ilikuwa tunapitisha sijui sheria au hotuba ya bajeti lakini nakumbuka mwenyewe nilizungumza hivyo. Lakini sasa mtoto unapomlea unamuwekea malengo kwamba mtoto huyu nimlee mpaka kipindi fulani kidogo kidogo aweze kujitegemea, wenzetu Waingereza malengo yao ni miaka kumi na sita wanakulea ukishafika miaka kumi na sita unakuwa kivyako vyako katika famili tena, kama unatoka kwenye famili basi kwaheli.

Sasa nadhani na Shirika letu hili nalo tukaliwekea malengo iwe kila mwaka ile ruzuku iwe inapungua tungeweka malengo hivyo, sio kwamba ikatwe kabisa kabisa lakini iwe kila mwaka tunaipunguza kidogo kidogo kwa hivyo ule utegemezi usiwe mkubwa, sasa nadhani hilo iwe ndio lengo la Wizara na mpaka itakapofika pahala sasa wakasema sasa tunasimama kwa miguu yetu nafikiri itakuwa ni faraja kwa serikali, japokuwa itachukua muda mrefu lakini nasema lazima kuwe na lengo la kupunguza ruzuku kidogo kidogo kwa sababu watabweteka.

Hofu yangu kuja kubweteka hilo ndilo ninaloogopa mimi kwa sababu wakiona kila mwaka kuna ruzuku kubwa nadhani ingekuwa sasa hivi hawapati ruzuku pengine kila siku wangekuwa wakitoa magazeti ya rangi baada ya kutoa la Ijumaa. Lakini pengine yote ile kutoa gazeti la rangi ijumaa ni kwa sababu ya ile ruzuku tu pengine siku hizi ingekuwa magazeti ya siku zote wanatoa ya rangi.

Halafu nikitoka hapo nije katika Idara ya Michezo nataka nizungumze suala moja tu pale Mhe. Waziri kaeleza malengo kwa mwaka 2010/2011 kaeleza mengi lakini mimi nitaeleza moja, kusimamia na kushajihisha kufanyika kwa mashindano ya Mawizara na Mashirika ya Serikali kwa michezo mbali mbali, hili mimi siliungi mkono sana kwa sababu ama naliunga mkono kwa majeshi katika vikosi ni jambo zuri sana, lakini silipendelei sana kwa Wizara za serikali na mashirika ya umma hili kufanyika. Hofu yangu nini Mhe. Mwenyekiti kwamba pesa nyingi za serikali zitakuja kutumika kwa ajili ya mashindano haya, tukaja tukapisha mambo mengine ikabidi pesa nyingi ziende kwa mambo

haya hiyo ndio hofu yangu ya kwanza.

Lakini hofu yangu ya pili kwamba wafanyakazi wa serikali ni watu wengi ambao wameshaanza kuchoka choka sasa kile tunachokikusudia hasa kuibua vipaji vya wanamichezo haitapatikana, sasa mimi nafikiria nguvu zetu zingeelekea kwenye Wizara ya Elimu tukashirikiana tukaanzisha mashindano katika maskuli ya Sekondari, mpaka Vyuo Vikuu hapa nadhani tunaweza kuibua vipaji vizuri sana vya wanamichezo.

Halafu kuna kitu kimeanza kienyeji enyeji lakini vile vile nafikiri tukakishajihisha na kukisimamia vizuri kinaweza kuibua vipaji vile vile, yale mashindano ya Majimbo mimi bahaati nzuri katika huu msimu uliopita vijana niliwasaidia sana katika jimbo langu, lakini bahati mbaya hawakufika mbali wakatolewa njiani. Lakini nadhani kama kutakuwa na utaratibu mzuri wa kuanzisha yale mashindano ya majimbo nayo yanaweza kusaidia kuibua vipaji vizuri vya wanamichezo, lakini nina hofu kujakuwa kila mwaka tuna mashindano ya mawizara haya kwanza kwa tabia yetu itakuwa ni *advantage* kazi watu watakuwa hawazifanyi tena, pesa za serikali tutaanza kuzitumia, magari ya serikali mara nyingi yatakuwa yanashughulikia mambo haya pengine miezi sita watu watakuwa katika matayarisho unajua tena sisi Wazanzibari tabia yetu jambo dogo tena tumepata mwanya sasa hiyo ndio hofu yangu.

Mhe. Mwenyekiti jengine ambalo limenivutia na nataka nikizungumze ni ile redio jamii iliyojengwa Micheweni, mimi nimebahatika mara mbili kwenda katika kile kituoa tullikwenda mara ya kwanza kabla ya kufungwa mitambo ile, tukenda baada ya uzinduzi na kazi tayari zimeanza kwa kweli ile redio ni nzuri. Nataka nirudie mawazo yangu ambayo kila wakati nayatoa ninapokutana ama katika kamati au katika ziara juu ya kile kituo, juu ya matumizi mazuri ya kile kituo nadhani lengo la serikali kujenga kile kituo ni kuwasaidia wenzetu wa Micheweni kimaendeleo kuondoka na umasikini wa kipato na umasikini mwengine usiokuwa wa kipato nadhani hilo ndio lengo kubwa.

Kwa sababu utafiti kwa kaya ulionyesha kwamba Micheweni wako nyuma kimaendeleo na tafiti nyingi zilizofanywa zinaonyesha hivyo hivyo, kwa hivyo mimi bado nasisitiza kwamba wataalam wetu wajitahidi sana na hata ikiwezekana kutafuta wataalam wanaotoka nje ya Zanzibar kuwa na program zitakazosaidia kweli kweli hasa kwa maendeleo ya lile eneo, kuliko kutumia muda mwingi pengine kwa salam tu nadhani itakuwa haikidhi haja. Salam bila ya shaka kila wakati haziwezi kukidhi haja lakini kweli zitakuwapo wakati mwengine kuwe na burdani hiyo haikataliki, lakini nasema kama kile chombo tutakitumia vizuri basi baada ya miaka kumi Micheweni inaweza kubadilika badala ha kuwa nyuma ikawa mbele na sisi tuliokuwa mbele tukawa nyuma hiyo ndio imani yangu.

Kwa sababu wenzetu wanasema *information is power* sasa pale watu wakaelimishwa mpaka wakafika pahala watoto waliokuwa hawataki kusoma wakaweza kusoma kwa kupitia redio ile huo utakuwa ni ukombozi, kuna tatizo la kilimo cha maweni ambacho Mhe. Subeti Khamis Faki kila wakati anakizungumza watu wakashajihishika kupitia redio ile mpaka wakakithamini kilimo cha maweni na wakakitekeleza sasa haya yatakuwa ndio matumizi sahihi ya kile kituo na mambo mengine ya maendeleo sina haja ya kutaja sekta moja moja. Lakini nasema lazima tujipange vizuri ili ile redio ilete matunada hasa tuliyoyakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze kidogo juu yah ii *Eacrotanal* hiki kituo mimi nasema kimekosa bahati kwa sababu ndio mwanzo tulikusudia kiwe kituo cha utafiti, wasimulizi wa asili wa lugha za Afrika lakini ikawa kuna ugumu wa michango ilikuwa haiji mpaka hatimae kikafa hichi kituo, lakini serikali kwa kupitia wizara yako ikaona mupewe mupalee na muwe napo alhamdullilahi watu wanafanyia angalau mikutano. Sasa mmekuja na wazo jengine jipya la kugeuzi kile kituo kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, sijui mme fanya utafiti kiasi gani lakini nina wasi wasi vile vile kufanikiwa hili.

Mhe. Mwenyekiti wasi wasi wangu unakuja vipi tuna taasisi nyingi tayari za Kiswahili ambazo zinatambulikana kimataifa kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam sasa hivi haidhuru sipo kwenye chimbuko la Kiswahili, lakini sasa hivi ni ngumu tena kujenga hoja kwamba Zanzibar ndio nyumbani kwa Kiswahili hata ukijenga hiyo hoja inakuwa ni hoja ya kihistoria tu, lakini itakuwa haina nguvu kubwa sana. Kwa sababu tayari wenzetu wanazo taasisi za Kiswahili zenye maprofesa zinazotambulikana kimataifa, ukija hapa hapa tayari tuna taasisi ya Kiswahili na lugha za kigeni *TAKILUKI.*

Mhe. Mwenyekiti , sasa mimi nadhani jukumu hili ilikuwa tusiwaachie hawa wenzetu Chuo kikuu cha Zanzibar *TAKILUKI* kama kweli wenzetu wa Afrika ya Mashariki wametupa hii sekta ya Kiswahili nyie Wazanzibar ndio mnaoiweza haya mengine tuachieni sie nyie chukueni hilo, kwa nini tusilipeleke *TAKILUKI* ili ikazidi kutanuka zaidi na ikazidi kuimarika. Mimi nina mashaka kwamba kamisheni hii haitofanya kazi na itakuwa kama ile *Eacrotanal* ilivyotutoka hiyo ndio hofu yangu ambayo ninayo, lakini labda Mhe. Waziri atakapokuja kufunga mjadala anaweza kutusaidia walivyofikiria wao na walivyofikiria Jumuiya ya Afrika ya Mashariki nadhani anaweza kutushawishi na kukubaliana na hoja yake.

Halafu nije katika Chuo cha Uandishi wa Habari napo kwa bahati nzuri nimepata fursa ya kutembelea na nashukuru kwamba sasa hivi mnajenga Chuo

chengine, lakini nasikitika sana kuona mpaka leo hamjasajiliwa *NACTE* hili linanisikitisha sana mimi nilikuwa nafikiria siku zote tayari mmeshasajiliwa na *NACTE* kumbe bado. Sasa mimi namshauri Mhe. Waziri aharakishe kusajiliwa kwenye *NACTE* kwa sababu sasa hivi tusiende kienyeji enyeji lazima tupate usajili wa vyombo hivi vya kitaifa.

Lakini la pili nataka niulize je Chuo chetu cha Uandishi wa Habari cha Zanzibar tayari kimeshaanza kupokea wananchi kutoka nje ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, hilo suala la kwanza.

Suala la pili vijana wetu wanaotoka pale vipi suala la ajira wanapata ajira au bado kutambulikana kwako katika ajira watu wana wasi wasi nako sasa hilo lilikuwa ni suala jengine.

Mhe. Mwenyekiti, nitoke hapo sasa nije katika Sauti ya Tanzania Zanzibar kanuni inakataza kurejea rejea lakini haikatazi kuweka mkazo wa jambo, Mhe. Hija Hassan Hija kazungumza jambo ambalo na mimi nataka nilizungumze la Sauti ya Tanzania Zanzibar na huu mchakato wa uchukuaji wa fomu, tokae siku waliyoanza kutangaza nia ya kugombea Urais wa Zanzibar sauti ya Tanzania Zanziabr kwa kweli imekuwa ikitangaza wagombea hawa na siku za kuchukua fomu wanatangaza *live*, jambo la kuhudhunisha na kusikitisha leo wamekata matangazo ya Baraza la Masuala na Majibu ilikuwa Raza anarudisha fomu yaani baraza hadhi yake ndogo kuliko Raza leo. Sasa mimi suala langu ni hili kwa sababu najua mtu suala la kuchukua fomu halikuwa bado la chama ni la mtu mwenyewe. Je, hawa watu wanaochukua fomu kuanzia pale kutangaza nia kuchukua fomu, kurejesha fomu huwa wanalipa kiasi gani sauti ya Tanzania Zanzibar.

Maana hili nasema bado halijakuwa la kiserikali wala la Chama ni la matu binafsi baso kusema kurejesha fomu ni ishu ya chama huwa ni ishu ya mtu binafsi, sasa je, Sauti ya Tanzania Zanzibar inamchaji kiasi gani mtu anayerejesha fomu kutangaziwa ile sherehe yake, hilo ninaliomba na ikiwezekana risiti mutuonyeshe.

Halafu nije katika Idara ya Upigaji chapa karibuni hivi tulikuwa tuna shida kubwa hasa Wawakilishi wa Pemba. Tulikuwa tuna tatizo wakati ule wa uandikisha wa daftari wananchi wengi walikuwa wana vile vyeti vidogo vya kuzaliwa lakini hawana vikubwa kama vya Mambomsige. Ilikuwa tunakwenda kule Afisi ya Mrajisi Mkuu wa Serikali tunawasaidia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mtu kumtoa Pemba kuja Mambo Msige mwananchi wa kawaida kwa kweli ni ngumu. Siku nyengine unaweza ukakaa miezi minne mpaka mitano cheti hujakipata, unaambiwa sijui Ile idara ya uchapaji sijui kuna

hivi, mara wanachapa mitihani, sijui wanachapa kitu gani aah! Kwa kweli ilikuwa ni usumbufu mkubwa. Na mpaka juzi tunachangia hii utawala bora bado wananchi Waheshimiwa wengi wamelalamikia juu ya vyeti vya kuzaliwa. Vyeti vya kuzaliwa tunajua wanachapisha Idara ya Uchapaji. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti tunamuomba sana Mhe. Waziri aiboreshe Idara hii kwa sababu inakuwa aibu. Aibu mtu katika nchi mtu kwenda Mambo Msige siku zote unataka cheti unaambiwa aaa sasa hivi kunachapishwa mitihani.

Lakini ukiangalia vitabu hivi vya hotuba ya bajeti naona *alhamdulilah* vyote vimechapwa hapa, tena vizuri vimependeza, vina rangi nzuri, lakini bado inaonekana uwezo wake labda mdogo. Mhe. Waziri namuomba hii taasisi aishuhulikie kwa nguvu zake zote ili ifanye kazi kwa uwezo mkubwa na ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu umenitaka nimalizie naomba nimalizie kwa suala la mwisho kuhusu Uwanja wa Amani. Kwanza nazipongeza juhudi za Mhe. Waziri alizozifanya kwenda China mpaka akafanikiwa pale *Ahamdulillah* lazima tumpongeze mwenzetu. Ile *legacy* aliyoulizwa siku moja na Mhe. Ali Haji moja ni hii. Mhe. Shamhuna hata akiondoka madarakani mimi nahesabu moja katika *legacy* ni hii. Jambo moja zuri ambalo linampa uhalali wa kumkumbuka ni hili.

Je, sasa kuna mpango gani ya kuutumie ule uwanja. Kwa sababu wenzetu Bara kukaa baada ya miezi mitatu minne baada ya kuona ule uwanja umejaa mabuibui wanatafuta angalau timu moja wanaialika inakuja pale. Sasa je na nyie mnao mpango kama huo au itakuwa ni hizi hizi timu zetu za Malindi na Miembeni tu.

Suala la pili wakati tunatembelea pale tuliambiwa kwamba ule uwanja kuutumia kwa sherehe za kitaifa kama magwaride itakuwa ngumu kidogo kwa sababu inaharibu ile mipira ambayo tumezoea kuita tatan lakini TATAN ni jina la Kampuni ambayo kuwa hata haipo tena. Je, sasa hivi sherehe zetu za kitaifa tutazifanyia wapi, maana yake hapa inakuwa kidogo tunaharibu.

Nakushukuru Mwenyekiti.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi magharibi hii kunipa nafasi ya kuchangia machache sana katika hotuba ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari.

Kwanza na mimi nitakuwa ni vibaya sana kama sitompongeza Mhe. Waziri kwa uamuzi wake wa kuwania nafasi kubwa katika utawala wa nchi yetu. Namuombea kama hakupata uraisi basi japo makamo wa Rais wa kwanza

aupate.

Baada ya hapo mimi ningeshauri tufanye utafiti mdogo. Wenzetu waliotutawala Uingereza wana shirika lao la Habari wanaliita BBC ni maarufu sana na linaonekana limepata maanikio makubwa katika uwanja wa habari. Jirani zetu Kenya na wao wameiga wanalo KBC na inaonekana kufanya vizuri sina takwimu hasa lakini halifanyi vibaya. Swahibu zetu na wao Tanganyika na wao karibuni miaka mitatu au minne wameanzisha TBC. Sasa nikitaka kumuomba Mhe. Waziri hivi na sisi tukianzisha ZBC vipi hali ya ufanisi utakaopatikana utakuwaje. Hili ningemuomba kwa sababu kuna wataalamu wengi na wazuri aje anijibu pengine na sisi katika nyanja ya habari tukapata ufanisi mzuri.

Jengine ni suala la Televisheni, mimi nakubaliana kwamba *impartiality* inaonekana kutaka kukwaa kisiki mapema. Ningeomba Mhe. Waziri alisimamie hili. Kama ni suala la mapato basi sina wasi wasi atafute mapato kwa kila hali kwani ni wajibu lakini kwa hakika mapato yenyewe lazima uhakikiwe. Mimi ni Mjumbe wa PAC wa Baraza lako, suala la mapato ya serikali huwa najaribu kulihimiza sana. Haja ya Mhe. Haji Faki katika hili ni kupatikana risiti ya wagombea kumi 11 isipokuwa Mhe. Waziri mimi naweza kumsemehe kwa sababu yeye yuko jikoni kwa hivyo anaweza kutumia mara moja moja, lakini wengine iko haja.

Mara moja Pemba tulikuwa tuna tatizo kubwa la TVZ tukaambiwa kuna *transmitter* haijapatikana lakini mambo yako jikoni msiwe na wasi wasi, baada ya muda mrefu sana tukaambiwa sasa mambo mazuri, tushapakuwa *transmitter* imekuja kutoka Afrika ya Kusini, baada ya siku mbili tatu naona mambo puu yamezima tena. Sasa sijui kile kifaa kilichopatikana kiliungua au vipi, naona Mhandisi Mhe. Mahmoud ananitizama anacheka cheka labda itakuwa ananijibu. Naomba nije nijibiwe hilo. Kwa kweli kukosekana kwa TVZ Pemba kuna athari nyingi. Moja ni la kimila kwa sababu wananchi wa Pemba wanalazimika kuangalia TV za nchi nyengine.

Mhe. Spika, TV zina mambo mengi sio tu kama burdani lakini pia mila za nchi, wanalazimika kuangalia Kenya na mila zao watoto wetu sasa wanaiga, wanaangalia Bara na mila zao watoto wetu wanaiga. Tunapenda kuangalia TVZ angalau mila kwa kiasi japo sio asilimia mia lakini angalau asilimia 70 au 80 wanajitahidi kidogo. Angalau tuna hakika wanaangalia TV ambayo silka mila na utamaduni wetu unakua *observe.* Sasa tukenda Kenya au Bara kwa kweli tunaona watoto wana vimini, mtihani kidogo, ilimradi mashaka, kukosekana kwake TV kuna athari nyingi.

Mhe. Spika, Sauti ya Tanzania Zanzibar nayo kupatikana kwake Pemba sio nzuri. Watu wengi siku hizi wanasikiliza Zenji FM, hii ni kwa sababu

upatikanaji wake ni tatizo kidogo. Jambo hili nalo pia lingetafutiwa dawa. Isijekuwa dawa kama ile ya TVZ tuliyoambiwa dawa tayari lakini baada ya muda ikazima, tusijetukaambiwa na hii vile vile tayari halafu baada ya siku mbili ikawa matatizo.

Halafu ningewaomba TVZ wafanye utafiti waangalie *volume* ya wasikilizaji wake ikoje, naona watu wengi siku hizi wameanza kuichoka choka, watu wengine wanafungua pale wakati wa matangazo ya vifo lakini baadaye wanasikiliza radio nyengine. Hili si jambo linalopendeza sana katika nchi, radio ya umma hupenda wananchi wake waipende, ikionekana kwamba wananchi wana i-*deviate* inaonekana kuna tatizo na hilo linehitaji kurekebishwa. Ningewashauri Mhe. Waziri wafanye utafiti wa kuangalia volume ya wasikilizaji wa Zanzibari.

Jambo jengine nizungumze kidogo suala la Uwanja wa Gombani. Mwaka jana nilifurahi kwamba kuna nyasi za bandia zilikuwa zinatayarishwa, lakini mwaka tunasikia zipo njiani, hofu yangu ni kwamba zisije zikakanywangwa hapo njia zilipowekwa. Maana kuna wakati nilisikia kuna jamaa mmoja sijui Makalebela sijui nani nyasi keshazikanyaka. Sasa nataka kujua kauli ile au habari ile niliyoipata ni ya uhakika au vipi hili naomba nipate ufafanuzi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Shirika la Magazeti na mimi ninayo kidogo. Inaonekana kwamba huu ulezi unaweza ukawa mgumu kidogo. Mwaka jana tuliidhinisha shilingi milioi 246 kwa Shirika hili, nilitegemea kwamba pesa zile ambazo umezipata ungewezesha angalau kuanza kujishuja vizuri. Mwaka huu wameomba milioni 245 milioni moja tu pungufu. Inaonekana kwamba kidogo Shirika linahitaji kutafuta mbinu za biashara zaidi.

Bahati mbaya katika kitabu cha Mhe. Waziri labda sikuangalia vizuri lakini hakuna maelezo ya kilichouzwa ni kiasi gani yaani kilichopatikana baada ya kupata mtaji ule wa Shilingi 246 mwaka jana. Tungeelezwa basi kwa pesa zile ambazo Baraza ilidhiidhinisha mwaka jana kazi iliyofanywa gazeti angalau limeweza kuzalisha milioni 100 au milioni 120 tukasema sawa, sasa tulipunguzie kama sasa lina uwezo wa kuzalisha milioni 120 nisingehitaji tena 245. labda nifahamu kwamba wameuza mtaji wa milioni moja. Kwa sababu mwaka jana walihitaji 246, mwaka huu wameomba milioni 245. kwa hivyo labda walifanya kazi wakauza magazeti ya shilingi milioni moja, ikiwa ni hivyo itakuwa mtihani kidogo itakuwa hili gazeti kidogo shirika lenyewe linakuwa gumu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba Baraza la Sanaa lipewe uwezo wa kuisaidia nchi. Sanaa katika jamii ni muhimu mno na ni eneo ambalo kama wasanii wetu wanaweza kupewa msukumu kidogo basi wanaweza kusaidia

sana katika kuzuia mmong'onyoka wa mila na utamaduni wa nchi yetu. Kwa hiyo sio tu watu wetu wazoelee kuangalia wasanii wa nchi nyengine kama Bara na Naigeria wale hawakufika pale hivi hivi tu, walifika vile kwa sababu nchi zao wamewezesha, wakawasaidia wakafika pale.

Leo vijana wetu na sisi wenyewe kila mmoja anaangalia wasanii wa Bara na Nigeria. Sisi kama hatujafanya kazi kubwa ya kulisaidia Baraza hili nalo likawawezesha wasanii wa Zanzibar kwa kweli hali yetu itakuwa mbaya sana. Hapa ni eneo ambalo mmong'onyoko wa maadili unaweza kuathiriwa vibaya sana. Namshauri Mhe. Waziri aone kwamba hili ni jambo ambalo ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi ningemuomba Mhe. Waziri maslahi ya wafanyakazi wa sekta ya habari kwa kweli si mazuri wanasononesha. Unajua mtu akiwa na uwezo kidogo unamuona kwa kweli ukiwatizama usoni tu unajua hawa watu hali zao si nzuri, ukiwaangalia na wafanyakazi wa Wizara nyengine wana *incentive* nyingi wana mambo mazuri mazuri ambayo wameandaliwa, lakini kwa kweli sekta ya habari hali zao si nzuri hata kidogo. Kama kuna *scheme of cervices* inahitaji kuandaliwa mapema na kuharakishwa utendaji wake basi ni katika sekta hii. Hawa watu wanafanya kazi moja muhimu sana ambayo ingehitaji kimaslahi waongezwe sana.

Mhe. Mwenyekiti, nina tatizo la viwanja vya michezo katika Wilaya ya Wete. Wilaya ya Wete ina tatizo kidogo na hapa sijui nani tunaweza kushirikiana naye kuona kwamba Wilaya ya Wete kidogo imepata unafuu. Wilaya ya Wete hatuna uwanja wenye maana labda ya hivi vichochoroni. Lakini pia hatuna uwanja wa *netball* wala wa *volleyball, tennis, badminton* kwa kweli kwa hali hii hatuwezi vijana wetu kupiga hatua ya kimichezo kwa sababu hawana eneo ambalo wanaweza kufanya mazoezi na kuibua vipaji vyao.

Ningemuomba Mhe. Waziri labda kama sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tungesaidiana na nani kuona kwamba hivi viwanja ambavyo vijana wanavihitaji viweze kupatikana pale wilayani Wete ili vijana wetu waweze kufanya mazoezi na tuibue vipaji ambavyo vinagesaidia nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa katika kitabu chake amesikitikia uhusiana mbaya wa CHANEZA na CHANEZA. Kwa upande mmoja labda nikubaliane naye lakini mimi kwa upande mwengine nawapongeza sana CHANEZA. Katika hili wameonekana hawakukubali kuburuzwa kwa hivyo maslahi ya Zanzibar. yamekuwa o*bserved*. Katika hili sipaswi kusikitika sana napaswa kuwapongeza sana CHANEZA kwa msimamo wao sabiti waliokuwa wameuona kwamba tusipofanya hivi basi Zanzibar katika sekta hii ya michezo inayosimamiwa kwa kweli itaburuzwa kama wanavyoburuzwa katika michezo

mengine. Kwa hili mimi nawaomba wapokee pongezi zangu na waendelee na msimamo huo huo.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuweka baraka zangu katika hotuba hii ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, kama wenzangu napenda kuchukua nafasi hii kumpa moyo na kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa kutumia nafasi yake kidemokrasia na kwa hili basi namtakia heri katika mbili hizi za kuwania kuwa Rais wa Zanzibar, Mwenyezi Mungu ataleta lenye kheri.
Mhe. Mwenyekiti, aidha niwapongeze watendaji wa Wizara na bila ya kusahau Naibu Waziri wa Wizara hii kwa juhudi zake kwa kuiendeleza Wizara hii na hadi leo tunazungumzia kwamba na sisi ni miongoni mwa wale ambao tumo katika teknolojia ya *digital* teknolojia mpya na tumo katika kupeana mafunzo ya kuweza kuendelea vyema katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikianzia na ukurasa wa 12 unapozungumzia mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010 niipongeze Wizara kwa hatua hii na kwa kweli yaliyoelezwa hapa sote ni mashahidi ni vitu vyenye kuonekana, tunapongeza kwa juhudi zao hususan katika kupata Ofisi mpya na kurejesha hadhi ya uwanja wa Aman Stadium.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nianzie kuzungumza kidogo kuhusu Idara ya Television. Hapa nilitaka kujua suala zima la uhifadhi wa vipindi mbali mbali wakati nilipokuwa mjumbe wa kamati kipindi cha mwanzo tulivyoanza katika Baraza hili tulikwenda tukaona hali mbaya ya uwekaji au uhifadhi wa kumbukumbu. Kidogo inanipa masikitiko kwa sababu katika jambo ambalo ningetegemea mpaka leo linapatikana nilipenda kuona ule ufunguzi pale kilipofunguliwa kituo cha *Television* Zanzibar. Nasikitika sana kwamba hili sijui kama wameweza kufanya utaratibu tukaweza kuipata.

Bila shaka itakuwa inatokana na tatizo hili la uhifadhi, sasa sijui tunamkakati gani au tumefikia wapi kwa sababu tulishauri muda mrefu kiasi, najua mipango na matumizi hayaendani sawa. Lakini nilitaka kujua hatua ambayo imefikiwa katika kuona jinsi gani tunaweza kuwa na uhifadhi wa vitu muhimu sana kama hivi, vikiwemo hotuba za viongozi mbali mbali au matukio mbali mbali ya serikali pamoja na mambo mengine ambayo yanatokea katika nchi yetu.

Jambo jengine la kupongeza katika upande huu wa Idara ya televiseni Zanzibar katika ukurasa wa 25 kuna kipengele hichi cha tano kinazozungumzia suala

zima katika haya malengo la kuandaa na kurusha hewani vipindi maalum vya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 vitakavyoshirikisha na kuvipa nafasi sawa vyama vyote vya siasa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, sipendi kurudia yale ambayo wanzangu wamesema lakini hapa ningependa kutoa ushauri tu kamba kutokana na hali ambayo sasa tupo ya kuanza kuaminiana hali ya amani na utulivu ambavyo mpaka sasa hivi tunakwenda nayo na *inshallah* itaendelea basi katika zoezi hili tukaona kwamba suala zima kama lilivyoandikwa hapa la uwazi.

Napenda sana kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pale aliposema matangazo haya yatakuwa ya ukweli na uwazi. Ningeomba basi tufanye kama vile wenzetu wanafanya ili kuondosha zile dhana na wasi wasi, tuweze kuonesha mchakato mzima wa chaguzi zinavyokwenda labda matokeo yanavyotoka na kadhalika. Haya yatazidi kutuletea imani na kutufikisha kwenye lengo lile tulilolikusudia kwamba tuwe na uchaguzi wa amani na salama lakini pia tusiwe na mashaka yule anayeshindwa aweze kumpongeza mwenzake anayeshinda bila ya matatizo, tusiwe na mivutano. Hiki chombo kitatusaidia sana kutufikisha katika lengo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nataka nizungumzie kidogo kuhusu tume ya utangazaji. Hapa nilitaka kuzungumzia, kipengele cha nne kama kilivyoeleza kwamba Kuendeleza na Kuelimisha na kuratibu urushaji wa matangazo na kutumia mfumo wa teknolojia *digital* hadi kufikia kiwango. Nilichokusudia hapa zaidi ni suala zima la utangazaji tuko katika mfumo mpya sawa na hata kama ungekuwa wa zamani bado nahisi kuna matatizo katika suala zima la vijana wetu ambao wanatangaza. Binafsi huwa napenda sana kusikiliza lakini nakosa raha ya kusikiliza kutokana na lafdhi za maneno au matamshi yao. Sijui hawakwenda chuoni au vipi kuna ladha unaposikiliza mtu anapozungumza kuna watu wengine wakizungumza unapenda uwasikilize kwa sababu unapata ile ladha ya maneno kwa matamshi.

Sasa hivi nasikitika sana kama vijana wetu wengi mpaka hizi redio nyengine za kina Zenji FM na wengine bado wana matatizo sana katika kutamka maneno kwa usahihi, gha zinawashinda, wanaweka mahali sipo wakati mwengine huwa nasikiliza sana hata taarifa za habari za Bara, wao siwalaumu sana kwa sababu ndivyo wanavyokwenda hivyo hivyo na ndivyo wanavyotokea pengine na matamshi yao. Juzi moja ilikuwa kali sana nilimsikia akimtaja marehemu baba wa Taifa nikacheka sana maana yake kwa kawaida wanaweza wakakosea kila kitu lakini huwa hawakosei kumtaja baba Nyerere lakini huyu wa juzi yeye alitoa kali hasa kwa kumwita baba Nyerele, nikaona hii hatari.

Mhe. Mwenyekiti, hapa sikusudii wao zaidi nakusudia kwenye vyombo vyetu

ambavyo vimo ndani ya Zanzibar. Sisi ndio tunaoonekana kwamba ndio wazungumzaji wazuri wa Kiswahili ningependa kwamba hii Tume ya Utangazaji na pengine hata chuo kijitahidi katika mafundisho na mafunzo wanayowapa vijana wetu basi kuwa na darasa la kutamka sio tu matamshi ya maneno kama haya ninayozungumza ya magharibi na mambo ya ghorofa. Lakini hata kutamka majina ya watu au nchi au mitaa mbali mbali kwa kweli inakuwa haileti picha nzuri, mtu amekaa pale natoa habari lakini anatamka vitu tofauti na vilivyo. Ni vyema wakapata hili darasa kidogo na wakaweza kutoa taarifa za habari ambazo unasikia raha kuwasikia vile wanavyozungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Chuo sasa hivi tumeingia katika mfumo mpya ya *digital* kwa hiyo ni vyema inatubidi tubadilike, utafutaji wa habari usiwe katika mfumo huu tulionao. Tumezoea vijana wetu habari zao wanazipata kwenye matukio pengine matukio ya kuitwa sio ya kutafuta. Hapa nilikuwa napenda kusisitiza kwamba suala zima la habari iwe ni mfumo wa kuzitafuta habari na sio kusubiri mpaka labda uletewe kibarua na ualikwe na vitu kama hivyo.

Tufike paha basi tuwe tunaweza kupata habari kama za wenzetu *breaking news* kimetokewa kitu ghafla kinaelezwa na mambo kama hayo. Wakati huu wa sasa na hasa katika hali hii ya mabadiliko ya tabia ya nchi ni vyema kuweza kujua kila linalotokezea kila wakati, kila pahala katika ulimwengu huu tuliokuwa nao. Si vizuri jambo linatokezea tangu jana sisi tunasoma habari leo, yameshatokea maafa makubwa na vitu kama hivo pengine hatujui yanaelekea upande wetu tukapata kujihami. Hili nilikuwa kujitanabahisha kwa upande wa huo ili na sisi tuweze kuonekana kwamba tunakwenda na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nataka nizungumzie kuhusu Idara ya Utamaduni na zaidi nilikuwa nataka kusisitiza kwamba kuna mambo ambayo tumeyashauri sijui labda kutokana na mambo mengi na wakati wenyewe huu ni wakati wa mchakato, inawezekana hapa mengine ya hapa na pale yanakuwa yanakosekana. Nilikuwa nataka kukumbusha kwamba tulipendekeza kwamba uanzishwe mfuko wa kuwaenzi wasanii wetu. Tulizungumzia sana kwamba kuna wasanii wetu ambao sasa hivi wengine wamestaafu wengine ni wagonjwa. Jinsi ya kuwasaidia, tukapendekeza uwapo huu mfuko ili waweze kuendelezwa kwa sababu wamefanya mengi, tusingeona vizuri kwamba hawa wazee wanakwenda wanaumwa mpaka wakati mwengine wanafikwa na mauti inakuwa wanafanya mambo ya ajabu, wanapita wakiomba omba na vitu kama hivi. Ni vizuri tukawaenzi ka kuangalia yale waliyoyafanya katika nchi yetu kuhusiana na masuala mazima ya utamaduni wa nchi hii.

Pia nisisitize kwamba kuna siku ya “Mkongwe hagewa” nikisema hivi namkumbuka sana almarhum Ali Baramia Mwenyezi Mungu amlaze pema

Peponi ningependa kukumbusha kwamba hii nayo isisahauliwe kwa sababu kwa namna moja au nyengine hawa wenzetu tunawapa moyo lakini pia tunakumbushia enzi lakini pia tunakumbusha na utamaduni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi katika fani nyingi tunakwenda sana na wakati, hata ukenda kwenye vipindi vya tarab, mashairi na vitu kama hivyo tunakuta ule mfumo ambao tulikuwa nao zamani sasa hivi unapotea. Tukiweka vitu kama hivi na tukaviendeleza tutakuwa tunakumbushia kule tunakotoka. Hatuwezi kupingana na wakati kwamba bila shaka mabadiliko yatakuwepo lakini kiutamaduni na kiasili basi vitu kama hivi ni vizuri vikaenziwa kwa sababu pia vinasaidia hata kuingiza pato wakati watalii wanapokuja kufatilia mambo kama hayo.

Mhe. Mwenyekiti katika hili kuna kipengele kinachosema kuendelea kutekeleza sera ya utamaduni Zanzibar kwa kuelimisha jamii kuhusu nini utamaduni wetu. Linagusana na hili ambalo nimemaliza kulizungumza. Nilikuwa napende kukumbushia kwa Mhe. Waziri na Naibu wake wakae tena lakini watuletee kile kipindi cha ndivyo tulivyo. Kipindi kile Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kinatufundisha mambo mengi hata yale ambayo labda wengine tulikuwa hatuyajui tumejua kwamba kumbe kulikuwa na hili kulikuwa na hili. Sasa hivi vijana wetu nafikiri mtoto kuanzia miaka 20 kushuka chini ukimuuliza maswali kama haya sidhani kama utapata asilimia angalau 10% ya wanaoelewa.

Vipindi kama hivi vikiwepo na tukaanza na vile vya zamani alivyokuwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wetu alivyokua akivifanya na Bwana Bakari Abeid pia wakatafutwa watu wengine wenye uelewa, mimi naamini wapo. Lakini tukikaa tukiacha muda ukapotea na hawa watu wakaja wakaondoka basi haya mambo mengine yatapotea kwa sababu pengine rika langu mimi na wenzangu tunaoendelea kuteremsha miaka tutakuwa hatufahamu vizuri. Mhe. Mwenyekiti, wanaotufuata sisi wa juu yetu na wazee wetu wao watakuwa ni wenye kuelewa zaidi.

Kwa hivyo, ni vizuri vipindi kama hivi vikaletwa badala ya vile ambavyo Mhe. Hija alizungumza vikatuni vilivyokuwa havina utaratibu mzuri wa mafunzo. Mhe. Mwenyekiti, hata hizi katuni kwa wenzetu zinawekwa kwa sababu maalum, lakini ili mtoto avutike kupata mafundisho yaliyokuwepo ndani yake ndio yanawekwa namna ile ya vikatuni ili aweze kukaa na ya kuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, katika Baraza la Kiswahili nilikuwa nataka kuzungumzia suala zima la lugha, nimeitaja kidogo hapa katika suala zima la watangazaji lakini na kama BAKIZA bado tuna jukumu la kuona kwamba lugha yetu haipotoshwi. Kuna maneno mengi sasa hivi yanaingia na bahati mbaya kwa

sababu yanaendelezwa na vyombo vyetu vya habari kupitia taarifa mbali mbali za habari na mambo mengine inakuwa wanalifanya hili suala linaendelea na linakuwa kwa kweli halileti mwelekeo mzuri hasa kwa vijana wetu wanaochipukia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa suala zima la viwanja vya watoto. Mhe. Mwenyekiti, sikuona pahala popote kama vimeguswa lakini ningependa sana Mhe. Waziri akija atwambie tuna mpango gani. Najua kuna viwanja labda kama hivi hapa vya Kariakoo wanavyo *ZSSF* au kama mtu yeyote mwengine kama atakuwa amepewa kushughulikia suala hili. Nilikuwa naomba kwamba bado wizara hii iwe ndio waratibu na wasimamizi wa hili, wale wengine waendeshe lakini wizara iwe ndio ambayo inasimamia na kuona kwamba haki za watoto katika hili linapatikana lakini pia na mazingira ya nchi yawe yamekaa sawa. Mhe. Mwenyekiti, nina mengine lakini kwa kuheshimu muda wako nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza jioni hii ya leo. Kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyotuletea, tumeisoma, tumeifahamu na sasa ndio tunaichangia. Aidha, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa moyo wake mshupavu kabisa wa kushiriki katika hiki kinyanganyiro cha kugombea Urais wa Zanzibar namtakia kila la kheri katika mchakato huo.

Vile vile nampongeza tena yeye na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa wizara hii kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kuongoza na kuendeleza mbele maendeleo ya wizara hii. Nampongeza kwamba ni mmoja katika wizara chache sana ambazo zimeamua kwa makusudi kujenga afisi zao zikawa afisi mpya na kuhama katika majengo makongwe yaliyoko Mji Mkongwe. Kwa kweli huu ni mfano mzuri wa kuonesha kwamba tunaendelea na tunasonga mbele. Vile vile nampongeza sana kutokana na hii Idara ya Michezo na Sanaa kwa kupata ofisi zake, hii ni hatua nzuri na ni ya kupigiwa mfano kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba sasa nichangie haya yafuatayo. Suala la kwanza ni kuhusu Uwanja wa Amani. Mhe. Mwenyekiti, bado nampongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa juhudi kubwa walizochukua kuona kwamba Uwanja wa Amani umefufuliwa ambao ulikuwa katika hali mbaya sana. Kwa kweli hii hakika ni kipimo kikubwa sana cha utendaji wa kazi kwani uwanja umebadilika kabisa hata ile mandhari yake imekuwa ni mpya kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa kiwanja hiki kitatumika inavyotakiwa hasa kinaweza

kikaingiza fedha nyingi katika nchi hii, tusiangalie fedha za kiwanja tu lakini nchi kikiwa kiko *very active* na kikiwa katika hali ya *stability* basi watalii wengi kutoka nchi za jirani wataingia kwetu, mahoteli yatajaa, biashara zitakwenda vizuri, maboti yatajaa, ndege zitajaa. Kwa hivyo, mapato mengi yatapatikana katika nchi kutokana na kiwanja hiki ikiwa kitafanya kazi zake vizuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kiwanja hiki kina hoteli nzuri mimi naijua ramani yake ni safi kabisa na kiwanja ni kizuri mno. Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu kwa wizara ione ipo haja ya kiwanja hiki kukodishwa wafanyabiashara kwani serikali itapata mapato mengi kabisa na *quality* ya hiki itabikia kuwa pale pale kwa sababu serikali itakuwa ina *monitor* na inaangalia mikataba yake namna gani kiwanja hiki kinakwenda. Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba ikiwa kiwanja hiki atakodishwa mfanyabiashara na akakitumia vilivyo basi kwa mwaka mmoja kutakuwa na mechi hamsini mpaka sitini.

Kwa kweli hiyo ndio njia pekee itakayoweza kufanya hiki kiwanja kikawa kizuri kwa sababu ni kizuri basi ikiwa kitakaa tu hakifanyi kazi kitapoteza haiba yake. Mimi ushauri wangu ndio kama huo nilivyosema akodishwe mfanyabiashara ambaye atakuwa na *experience*, atakuwa na uwezo wa kuweza kuki-*maintain* na kuweza kufanya *marketing* na kuleta tija kubwa katika nchi yetu. Hili ni pendekezo la kiwanja pamoja na hoteli yake. Mhe. Mwenyekiti, naamini kabisa wakitolewa tangazo wafanyabiashara wakubwa kabisa watajitokeza na wakatumika kiwanja hiki kwa maslahi na maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ningeomba niende katika suala la michezo. Idara ya Michezo mimi nakumbuka zamani Zanzibar ilikuwa na michezo mingi sana na watu wetu walikuwa wachezaji wakenda katika mashindano kwa mfano mashindano table tanis wakenda mpaka China, mashindano ya kuogelea. Kwa hivyo, nasema kwamba hii michezo imekufa kabisa umebakia mpira na huo mpira una fufuka fufuka lakini hii michezo mengine ni kama imedharauliwa kabisa. Mhe. Mwenyekiti, nahisi kwamba ipo haja ya kuona kuwa Zanzibar wako vijana wengi sana ambao wana vipaji vya kutosha katika michezo, na kihistoria michezo mingi ilianzia hapa katika *East Africa*.

Kwa hivyo, suala la michezo bado Idara ya Michezo haijafanya kazi ya kuonekana angalau kuona mtu mmoja kutoka Zanzibar kafika katika *Olympic*. Nafikiri hii ni *challenge* kuanzia sasa hivi hebu tuangalieni watu wangapi kutoka Zanzibar watafika katika mashindano ya *Olympic* katika miaka ijayo.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika Idara ya Uchapaji ni kwamba hiki kiwanda ni kizuri cha kuchapa lakini kwa bahati mbaya hakifanyi kazi zake kibiashara

ndio maisha kinahitaji kipate msukumo. Kwa hivyo, ningeomba ifanywe *physibility study* ya kiwanda hiki na kuona kwamba mahitaji yake yote yapewe halafu kiwe kinafanya kazi zake kibiashara. Kazi Zanzibar ni nyingi sana za kuchapa, watachapa mpaka watashindwa wenyewe, hapa tumeona watu walioanzisha uchapaji na kiwanda kidogo sasa hivi wameshakuwa na kiwanda kikubwa na wanachapa mahala mingi na faida kubwa inapatikana na wameajiri watu wengi. Kwa hivyo, naamini kwamba hatuwezi kushindwa na sisi Idara ya Uchapaji ikaweza kufanya kazi hiyo na kweli kazi ni nyingi na biashara iko kubwa na kila siku biashara inazidi kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, tukija katika suala la gazeti letu la Zanzibar Leo na TVZ na Sauti ya Tanzania Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, ipo haja ya kuona kwamba yanakwenda kibiashara. Mhe. Mwenyekiti, tuangalieni leo wenzetu Tanzania Bara walioanza katika masuala haya ya televisheni na magazeti. Kampuni ambayo ilikuwa na gazeti moja sasa hivi ina magazeti manne au matano na kampuni ambayo kwamba ilikuwa na televisheni moja sasa hivi ina televisheni nyengine mbali mbali, kwa sababu wanaendesha vituo vyao kibiashara. Mimi ningeomba zote timu tatu hizi zikashirikiana na wafanyabiashara wa Zanzibar kuona namna gani wafanyabiashara wa Zanzibar wanaweza kutumia kuleta matangazo yao.

Mhe. Mwenyekiti, maisha mfanyabiashara anaangalia ile televisheni au gazeti au chombo ambacho kinapendwa na watazamaji na wasomaji, ikiwa gazeti halina wasomaji basi mfanyabiashara anatafuta gazeti lenye wasomaji anapeleka tangazao lake. Mhe. Mwenyekiti, tuangalie utafiti kabisa ni njia gani za kuweza kuyafanya magazeti yetu yakawa yanaweza kuwa very *attractive* na televisheni yetu pamoja na redio zetu. Mhe. Mwenyekiti, ili wafanyabiashara waweze kuvinyanyua vyombo vyetu hivi basi ni lazima tuviboreshe vyombo hivi viwe vya kileo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuchangia suala la hilo sasa hivi niingie katika suala la viwanja vya watoto. Nakumbuka zamani ilikuwa inazungumzwa viwanja vya watoto, Tibirinzi Pemba na hapa Kariakoo. Mhe. Mwenyekiti, tumezoea watoto kila mwisho wa wiki tuwapeleke katika viwanja kama hivi, tunatarajia kwamba viwanja vizidi kuongezeka zaidi hapa kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine tunaona kwamba ikifika wakati wa sikukuu viwanja vyote vinajaa watu wengi kwa hiyo watoto huwa wanasongana katika viwanja mbali mbali. Utakuta hakuna utaratibu mzuri wa kuona kwamba viwanja vya kufurahishia watoto vinaangaliwa na vinapewa umuhimu kwa sababu watoto wetu lazima tuone kwamba tunachukua juhudi ya kuweza kuwafurahisha na kuona kwamba na wao wana nafasi ya kucheza kama watoto wengine wote katika ulimwengu wa leo. Wanaona katika televisheni, wanaona katika

michezo lakini wakiangalia katika nchi yao kabisa bado hawapewi umuhimu tutakwenda wapi ikiwa hatuoni kwamba hili suala tunalifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika suala la utamaduni. Mhe. Mwenyekiti, katika jambo ambalo kwamba watalii wanakuja katika nchi yetu, huwa wanakuja kuangalia vile vile utamaduni wetu, na upo hasa utalii wa utamaduni wa asili, watu wanakuja wanakaa katika vijiji ili kuona utamaduni wa nchi ile. Utamaduni wa Mzanzibari bado haujapewa hadhi yake unayostahili kwani bado haujafanyiwa utafiti wa kina wa kuonekana kama huu ndio utamaduni wa Mzanzibari na watalii watakapokuja hapa wakaweza kuonesha ule utamaduni wa Mzanzibari.

Mimi nilikuwepo katika *member* wa *ZIF* tuliona namna gani tulipoanzisha ile *ZIF*, namna gani walivyokuwa wanakuja watu mbali mbali na wakifika pale walikuwa wanavutiwa na mambo ya Zanzibar. Lakini kila anayekuja huwa anataka kujua na kuona utamaduni wa Mzanzibar. Kwa hivyo, ningeomba hii *indication* ya utamaduni wa Zanzibar ni nini na uko wapi na ni vipi lazima mtalii akija apate *information*, apate kuona *vision*, apate kuona *film* na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nimeona habari moja wametoa katika televisheni ya *Capitals* mambo ya taarab kina Ustadhi Iddi Farahani nimewaona jamaa wako nyanganyanga wamechoka wanaeleza ile habari ya udi na mambo mengine. Lakini ukiwaona ni wachofu kabisa, kile kipindi ni kizuri lakini wale waliowatoa kwenye kile kipindi wote ndio wenye ujuzi ule naona watakufa nao ule ujuzi. Nasema kwamba wasanii wetu tusiwadharau tuwape kipaumbele kwani wamefanya kazi kubwa sana katika nchi hii.
Kwa kweli hali zao ni mbaya sana na hatujui tutatumia njia gani lakini nafikiri angalau ipatikane ile *appreciation* kwamba sisi tuna-*appreciate* kwa kazi kubwa waliyoifanya. Namna gani hawa watakapoondoka wao nani anarithi ili kuendeleza utamaduni huu, kwa kweli masuala haya ya wasanii ni muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Tanzania Bara walikuwa hawana wasanii mambo haya ilikuwa ni hapa Zanzibar, lakini sasa hivi kule Bara filamu zao utaona zinaoneshwa katika *station* za Nigeria.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niunge mkono hotuba hii.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi 1/07/2010 saa 3:00 asubuhi)